ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa

10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni

20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	N/ Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28. Mhe. Ali Mzee Ali	Uteuzi wa Rais
29.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
30.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
34. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani

35.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
37.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
47.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
48.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
49.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
50.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe

76 Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 18 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Asha Bakari Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 155

Tatizo la Usafiri

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na usumbufu mkubwa wa usafiri wa baharini kati ya Unguja na Pemba, jambo ambalo linatia wasiwasi juu ya uhakika wa usafiri na usalama wa wananchi wengi wanaotumia usafiri huo na mali zao unaotokana na uchache na ubovu wa vyombo vya kwenda na kurudi Pemba na Unguja.

(a) Ni lini Unguja na Pemba itapata usafiri wa uhakika na usalama kama ilivyo kati ya Unguja na Dar-es-Salaam.

(b) Kwa nini vyombo ambavyo vinaonekana wazi kwamba ni vibovu vinaruhusiwa kubeba abiria.

(c) Je, serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha chombo/mamlaka ya kudhibiti ubora wa vyombo vya usafiri wa baharini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 155 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaendelea kufanya juhudi kubwa kusaidia upatikanaji wa vyombo vyengine, mazungumzo yanaendelea. Mhe. Naibu Spika, kuna takriban kampuni nne ikiwemo ya *Infit Group* (Italy) imeshaonyesha nia hiyo ya kutusaidia na tunawategemea kufika Zanzibar siku ya leo kwa ajili ya kuendeleza mazungumzo hayo. Vile vile Kampuni za Uturuki na Kampuni ya *Sazana Co-operation Inc* ya Ingland na Kampuni ya MTKN ya Abudhabi nazo pia zimeonesha nia ya kutaka kusaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutandua matatizo ya usafiri kwa Visiwa vya Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Naibu Spika, safari za boti zinaratibiwa nyenendo zake na kudhibitiwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini. Boti au meli ni kama chombo chengine hupata matatizo ya kiufundi mahala popote, hali ya bahari nayo huchangia usumbufu na kupunguza mategemeo ya kufika kwa wakati kwa vyombo hivi.

(c) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaazisha chombo chenye kuitwa Mamlaka ya Usafiri Baharini kilichotokana na uasisi wa sheria ya mwaka 2006 hadi mwaka 2009 kuanzishwa kwake kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba vyombo vya usafiri vinavyokwenda Pemba mara kwa mara huwa vina matatizo, hasa juzi Noora ilizimika taa mara mbili usiku. Je, huoni hali hiyo inahatarisha maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli nakubaliana na Mhe.. Mwakilishi kwamba kuna baadhi ya vyombo vinavyokwenda Pemba vinatokezewa na matatizo wakati wa safari. Lakini Mhe. Naibu Spika, napenda kulieleza tena Baraza lako tukufu kwamba,

Mamlaka ya Usafiri Baharini wajibu wetu ni kuvikagua na kuthibitisha kwamba chombo hiki kiko salama kwa kufanya safari kati ya Unguja/Pemba au kwengineko.

Uwezekano wa kutokezea matatizo kwa chombo hicho kama vilivyo vyombo vyengine vya kiufundi huwezekana kutokea wakati wowote, lakini napenda tena kumthibitishia Mhe. Mwakilishi chombo chetu hiki na taasisi yetu hii tutahakikisha kwamba vyombo hivyo vinakuwa makini na salama zaidi ili kuhakikisha maisha ya wananchi wetu yanakuwa katika hali nzuri zaidi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa vyombo vingi vinamilikiwa na watu binafsi, kampuni hizi zinakuwepo na kufa, lakini baadhi ya vyombo vinamilikiwa na serikali na serikali huwa haifi inaendelea. Ni sababu zipi za msingi iliyoifanya Shirika la Meli kuwa vyombo vyake vyote zimekuwa vichakavu kabisa kabisa bila ya kupatikana vyengine.

(b) Lakini ikiwa hilo limetokezea na masuala aliyozungumza Mhe. Naibu Waziri ni mambo ya muda mrefu. Je, wizara yake ina mpango gani wa muda mfupi wa kuiokoa hali ambayo ni ya usafiri baina ya Unguja na Pemba hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba vyombo vyetu vya usafiri hasa hivi vya serikali navyo vimekuwa vikuu kuu na vya muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sehemu kubwa meli zetu hizi za serikali zilikuwa zikiendeshwa kwa zaidi kwa mfumo wa kutoa huduma kuliko mfumo wa kibiashara, pamoja na kwamba wananchi walikuwa wakilipa nauli, lakini hakukuwa na utaratibu mzuri ambao ulikuwa ukiratibu shughuli hizi kwa mfumo wa kibiashara. Ni imani yangu kwamba Shirika la Meli baada ya kukamilisha utaratibu wa kupata sheria mpya itakayoweza kuongoza shirika hilo mfumo huu utabadilika na tutakuwa na mfumo mzuri utakaoweza kutoa tija na maslahi mazuri zaidi kwa wananchi lakini pia kwa upande wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, kweli mipango yetu ya serikali ni mipango ambayo inaweza kuchukua muda pengine mwaka, miaka miwili na kuendelea. Lakini kwa muda mfupi tunaendelea kufanya mazungumzo na mashirika na makampuni yetu yalioko ndani waone umuhimu wa kuongeza ruti

ya Unguja/Pemba ili kuokoa huo usumbufu tunaosema. Makampuni yapo na tunaamini kwamba na wao wataliona kwa uzito huo kama tunavyouona sisi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa kuna kampuni zimekuja kuangalia hali ya bandari na zikashindwa kufanya kazi kutokana na ufinyu wa bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie swali lake Mhe. Mwakilishi sikulisikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa kuna kampuni zimetaka kuja kuwekeza kwenye vyombo kama hivyo alivyovitaja hivi sasa, lakini kutokana na usalama na ufinyu wa bandari wameshindwa kuwekeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, anayoyasema Mhe. Mjumbe sikubaliani nayo.

Nam. 158

Ucheleweshaji wa Marekebisho ya Mishahara ya Walimu

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Kiutaratibu watumishi wote wanaporudi masomoni na ikiwa wamefanikiwa katika Kiwango cha Diploma na Shahada ya Chuo Kikuu hufanyiwa marekebisho katika mishahara yao. Hata hivyo kuna taarifa kwamba marekebisho ya mishahara ya walimu huchukua muda mrefu.

(a) Mhe. Waziri, kuna sababu gani zinazofanya walimu kuchelewa kurekebishiwa mishahara yao wanaporudi masomoni.

(b) Mhe. Waziri huoni kwamba kucheleweshwa kwa malipo hayo ni kuwanyima haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 158 lenye vifungu (a) na (b), lakini kwanza nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa walimu waliomaliza masomo ya Shahada na Stashahada na kufanikiwa kupata vyeti wanastahiki

kufanyiwa marekebisho ya mishahara yao. Pia, ni kweli kuwa baadhi ya walimu waliomaliza masomo wamechelewa kufanyiwa marekebisho ya mishahara yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Marekebisho ya mishahara ya baadhi ya walimu imechelewa kutokana na sababu zifuatazo:-

- Walimu kuchelewa kuwasilisha ushahidi wa vyeti vya kumalizia Stashahada au Shahada baada ya kumaliza masomo

- Baadhi yao wanalazimika kurudia mitihani kwa baadhi ya masomo na hivyo kutostahiki kufanyiwa marekebisho hadi watapofaulu somo walilorudia na kupata cheti

- Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuchelewa kutoa kibali cha kufanyiwa marekebisho ya mishahara ya walimu na ambayo nayo ina wajibu wa kuhakiki vielelezo vyote vinavyowasilishwa ili kuzuia udanganyifu wa aina yoyote.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara haiwanyimi walimu haki yao kwa kuchelewa kuwafanyia marekebisho ya mishahara yao kwani walimu wanaochelewa kufanyiwa marekebisho wanalipwa *arrears* za mishahara yao kwa muda wote waliostahiki. Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zinahakikisha kuwa walimu wanaomaliza masomo na kufaulu wanafanyiwa marekebisho ya mshahara yao katika kipindi kifupi baada ya kuwasilisha taarifa zote muhimu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Licha ya uzalendo wa walimu hao. Je, huoni ndio sababu inayowasababisha wasirudi skulini mwao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, inawezekana kwa sababu kila mtu na uzalendo wake, uzalendo unapishana hauwi sawa. Lakini naomba kama nilivyosema wazalendo wazidi kuwa wazalendo kwa sababu hii haki hainyimwi wanalipwa pesa zao na kwa mujibu wa *arrears* toka siku ambayo wanamaliza mafunzo yao. Lakini Mhe. Naibu Spika, tulilolizungumza hapa ni kuwa hii kazi si ya Wizara ya Elimu tu, ni wizara tatu ambazo tunashirikiana kuhakikisha walimu hao wanapata haki zao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kuna walimu ambao wamemaliza masomo karibu miaka mitatu nyuma, na kwa kuwa tayari wameshawasilisha vyeti vyao wizarani, na kwa kuwa taaluma ya sheria inatueleza kwamba, haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa.

Je, kuendelea kuwanyima walimu hawa mafao yao sikwenda kinyume na haki za binadamu.

Pili, Mhe. Naibu Waziri anaweza kunieleza ni lini hasa watawalipa walimu hawa waliokwishapeleka vyeti vyao wizarani na mwisho kabisa. Je, wizara itakuwa tayari kulipa *arrears* zao za miaka mitatu nyuma tangu wamalize masomo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, hatwendi kinyume na haki za binadamu kwa sababu nia ya kuwalipa tunayo, kwa taarifa yake ni kwamba kuanzia mwezi Mei, 2011 jumla ya walimu 141 tumeshawalipa malimbikizo yao kwa kutumia jumla ya shilingi 38,170,397,000 na tunajitahidi kuwalia na kuahidi kwamba, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha tutawamaliza walimu wote waliobakia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara ni sehemu inayokwenda kwa mipango si kama sokoni. Je, tatizo lililotokea wizara nyengine kutiwa adabu walimu huoni kwamba wizara yenyewe inawajibika katika suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, sijamfahamu vizuri.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba, waliokwenda masomoni ni walimu na kwa kuwa wizara ni sehemu iliyo na mipango ya kupanga kila kitu. Je, kuiachia wizara nyengine ikaamua mambo

ya walimu bila ya wenyewe kushughulika huoni kwamba hii ni uzaifu wa wizara yenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu ni moja katika wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kama ambavyo nilizungumza kwamba tunafanya kazi serikalini ki-*team work.* Sisi kama wizara tuna wajibu wetu ambao tunautimiza, lakini na Wizara ya Utumishi nao wana wajibu wao wa kuhakikisha lile ambalo tumewapelekea liko sawa, kwa hivyo na wao ni lazima wapitie.

Wizara ya Fedha pia wanayo dhima hiyo juu ya kuhakikisha kama pesa ambayo inatumika basi inatumika vilivyo. Kwa taarifa yake Mheshimiwa ni hivi karibuni tu, tumekaa na wenzetu wa Wizara ya Utumishi kuhakikisha kwamba huu urasimu mkubwa ambao upo unapungua ili kuhakikisha kama walimu wetu wanapata pesa zao kwa wakati wanaporudi katika masomo yao. Ahsante.

Nam. 177

Wafanyakazi wa Huduma za Upasuaji *"Theatre"*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wafanyakazi wa "*theatre*" katika Hospitali Kuu ya Mnazi mmoja wanafanya kazi katika mazingira magumu na kuhatarisha kwa afya zao. Kwa mfano: wana sare moja tu ambayo kama wataifua katika kipindi hiki cha mvua hawataweza kupata nguo ya kufanyia kazi siku ya pili, hawana viatu vya kutosha vinavyofaa kwa ajili ya kazi za "*theatre*" na kadhalika.

(a) Je, serikali inaielewa hali hii.
(b) Kama inaielewa ina mpango gani ili kunusuru afya za wafanyakazi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 158 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna upungufu wa sare ikiwemo viatu vya *theatre*, lakini si kwa kiwango cha kauka nikuvae.

(b) Katika mpango wa wizara kwa Mwaka huu wa Fedha suala la sare na vitendea kazi vyenginevyo kwenye Idara hiyo ya Upasuaji vimepewa kipaumbele ingawa inategemea na upatikanaji wa fedha kutoka serikalini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kujua hii kauka nikuvae maana yake ni nini. Taarifa niliyokuwanayo kutoka kwa wafanyakazi wa *theatre* katika kamati tulipokagua walikuwa na kilio cha kuwa na sare moja tu na *pair* ya viatu. Je, kwa maana hiyo haijatosha kuwa ni kauka nikuvae hiyo.

Pili, wizara yake ina mpango gain wa kuondosha tatizo hili sugu.

Tatu, saa kumi na moja jana jioni kulifanywa operesheni *theatre* kukiwa kiza, sijui taarifa hiyo unayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la kwanza na la pili kwa sababu hayo ndio naona yana uhusiano na hili suala mama. Suala la umeme kuwa kiza hilo halina mahusiano hapa kwa hivyo, hilo sitojibu.

Mhe. Naibu Spika, *theatre* nguo zinazotumika pale ni nguo ambazo zinafuliwa kila siku na zinavaliwa mara moja, zikishavaliwa mara moja inabidi zifuliwe, zichemshwe kwa kutumia moto mkali ili kuuwa wadudu. Madhumuni ya nguo za *theatre* ni kuhakikisha kwamba mgonjwa anayepasuliwa hapati maambukizi kutoka kwa mgonjwa mwengine. Kwa hivyo, ni operesheni nyingi zinazofanyika kwa siku moja achilia mbali operesheni ambazo zinafanyika kwa dharura. Huwa tuna nguo nyingi na zinavaliwa na madaktari wengi kwa sababu kule ni *team.* Kwa hivyo, zinapotumika inategemea siku inavyokuwa, zinaweza zikamalizika kulingana na wingi wa wale watu waliopo sio kwamba ni nguo moja, kama ingekuwa ni nguo moja tu basi ingefanyika operesheni moja tu kwa siku. Kwa hivyo, hilo sikubali kwamba kuna nguo moja, nasema nguo zipo isipokuwa hazitoshi.

Lakini kitu chengine ninachokiona ni kwamba kamati ilikwenda kule na yeye Mhe. Jaku akiwemo anajua kwamba hilo tatizo lipo. Sasa yeye Mhe. Jaku kama mfanyabiashara, kama mzalendo, haoni basi akaisaidia serikali wakati anatuona na wanaokwenda kule ni watu wetu. Mimi nina imani kwamba uwezo huu unao tuletee majora tutashona tuisaidie serikali pale ambapo imepungukiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa maelezo ya ziada kwa Mhe. Jaku kwamba masuala haya tumeyachambua na kuyaeleza kwa urefu

wakati wa bajeti na moja katika suala tulilosema kwamba vitu hivi tutavishughulikia. Nilitegemea angesema kwamba suala lake angeliondoa kwa sababu mjadala wa bajeti tulishayaeleza, lakini pamoja na hayo tunaomba kumueleza kwamba tutatekeleza mwaka huu, sasa angoje atuulize tena mwakani kwamba ziko moja au mbili.

Nam. 170

Sababu za Mgao wa Umeme

Mhe. Asha Bakari Makame - Aliuliza:

Ni takriban miezi miwili sasa tangu ulivyoanza mgao wa umeme hapa Zanzíbar. Kutokana na mgao huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa ratiba maalum ili kuwasaidia wananchi kuweza kujua ni wakati gani umeme huo utazimwa.

(a) Je, Mhe. Waziri mgao huo wa umeme umetokana na nini.

(b) Kwa kuwa ratiba maalum imeandaliwa ni sababu gani zinazopelekea kutokufuatwa kwa ratiba hiyo.

(c) Kwa kuwa umeme umekuwa ukikatika ovyo na wananchi kutokupewa maelezo juu ya ukatikaji huo, na kupelekea baadhi ya vifaa vya Watumiaji wa umeme kuungua. Je Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani kwa kuwalipa fidia Watumiaji wa Umeme wanaopata hasara ya vitu vya kuharibika kutokana na matatizo ya umeme ambayo yako nje ya uwezo wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 170 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa mgao huo wa umeme umetokana na kuzidiwa kwa uwezo wa kubeba mahitaji ya umeme kwa waya uliokuwepo baharini ambao yanapindukia megawati arubaini tu.

(b) Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa sababu inayopelekea ratiba ya mgao isifuatwe, ni kuongezeka matumizi ya umeme yanayopindukia uwezo wa waya kabla ya miundombinu kunakopelekea umeme kukatika kutokana na hitilafu.

(c) Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa mara nyingi umeme unapozimwa kwa makusudi, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme huwaarifu wateja wake kwa kutumia vyombo vya habari, pia iwapo mteja itatokezea ataharibikiwa kifaa chake kwa sababu ya hitilafu ya umeme na mafundi wetu wanapothibitisha hulipwa fidia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moa la nyongeza lenye a na b.

(a) Je, Mhe. Waziri atawahakikishiaje wananchi wa Unguja na ni lini watapata umeme wa uhakika bila ya mgao.
(b) Kwa kuwa tunaelewa majenereta ya umeme yapo na hayatumiwi. Je, Mhe. Waziri hanoi kuwa kuna hatari ya kufa na kuharibika na kupoteza mamilioni ya fedha bila ya kutumiwa majenereta haya.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, majenereta yapo yana uwezo wa kutoa MW. 20 ambazo kwa matumizi ya Zanzíbar haitoshi, lakini majenereta hayo gharama zake ni kubra sana tunatumia shilingi 245-50 kwa kila *unit* moja kuizalisha, lakini sisi tunauza shilingi 137 kwa *unit* moja. Kwa hivyo, kuna pengo Kubra sana ambalo tuliomba *tariff* yetu ya umeme iongezeke ili tuweze kuziba pengo hili na mapengo mengine. Hiyo kazi inafanywa kutafuta *price bid-up* ili tuweze ama kukubaliwa ama kukataliwa. Kwa hivyo, mpaka hapo ambato tutakubaliwa na mpaka hapo tukikataliwa serikali itapolipia gharama japo chache za kuzalisha umeme kwa jenereta kwa kweli shirika litashindwa kuzalisha umeme kwa jenereta.

Mhe. Naibu Spika, jibu (b) mgao wa umeme utaendelea mpaka pale tutakapomaliza shughuli za kuweka waya wa umeme utakaozalisha megawati 100. Vyenginevyo kuzitumia megawati 40 kwa kuzilazimisha tunaweza tukapata tatizo ambalo limeshawahi kutokea la kukaa kizani. Kwa hivyo, tunawaomba wananchi watusaidie kustahamili mpaka hapo tutakapolaza umeme mpya wa megawati 100.

Nafikiri tatizo la mgao wa umeme halitamalizika, lakini tunagawa umeme kwa saa moja nusu na inaelekea wananchi wameshatukubalia, wameshazoea. Sasa tunaendelea kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba watusaidie kutustahamilia mpaka hapo waya mpya utakapomalizika kutengenezwa na kuulaza katika bahari.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali mama amesema kwamba tatizo la mgao wa umeme uliopo ni kwa sababu ya waya ulioko baharini hauwezi kubeba umeme wa kutosheleza Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Tanzania Bara ambako tunachukua umeme wana mgao tena wa kudumu wa umeme na hawajajua lini tatizo hili litaondoka. Sisi tunachukua umeme kutoka Tanzania Bara na hivi sasa tuna waya unaobeba umeme megawati 45 na sasa hivi kuna mpango wa umeme wa *MCC* ambao una uwezo wa kuchukua umeme megawati 100. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Tanzania Bara wana mgao wa kudumu na sisi bado tunachukua tena umeme kule kule ambako wao hauwatoshi.

(a) Je, ni lini hasa watatuondoshea tatizo hili la kuchukua umeme Tanzania Bara na kuwa umeme wetu wa kudumu ili kuweza kuhudumia wananchi wa Zanzibar.

(b) Je, atakubaliana na mimi hivi sasa wawekezaji ambao wanataka kuweka viwanda na mambo mengine hawawezi kuja wakawekeza kwa ajili ya umeme tulionao wa mgao na hivi sasa sisi wenyewe haututoshi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana nae kwamba wenzetu ambao wanatuletea umeme na wao wana mgao. Sababu za wao kuwa na mgao mimi silijui, lakini nafikiri umeme walionao ni mdogo kuliko matumizi ya wananchi. Sasa tutategemeaje sisi kupata umeme wa kututosha wakati wao wenzetu wanaotupa umeme wana mgao.

Sisi tunahitaji megawati 60 kwa hivi sasa, lakini tumenunua waya na tutaweka waya wa megawati 100 kwa ajili ya mahitaji ya baadae yatakapoongezeka. Tumeandikiana mkataba na wao watalazimika kutupa megawati tunazohitajia alimuradi tu tunalipa bili zao.

Kwa hivyo, mimi sioni kama kuna uhusiano wa wao kuweka mgao na sisi kupata umeme. Hivi sasa wao wako tayari kutupa umeme tunaohitajia wa megawati 45, lakini tuna hofu tukichukua umeme wa megawati 45 tutaunguza waya wetu na kwa hivyo tutalala kizani kwa siku nenda siku rudi. Kwa hivyo, mimi sina wasi wasi alimuradi tukilipa bili za umeme kama tunavyolipa sasa hivi kila mwezi basi tutapata umeme kwa mujibu wa mikataba tuliyoandikiana na wenzetu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali madhumuni ya kununua majenereta haya ni kwa ajili ya kuyatumia wakati tunapokuwa na matatizo ya umeme katika nchi yetu. Ikiwa serikali inasema sasa hivi majenereta hayo yana gharama kubwa kuyaendesha na inaonekana sasa serikali inashindwa kuyaendesha majenereta hayo kwa gharama kubwa.

(a) Je, majenereta hayo yaliigharimu kiasi gani serikali katika kununua kwake.

(b) Kwa nini serikali ikanunua majenereta ambayo kwa kweli kuendesha kwake yatakuwa na matatizo katika nchi. Je, huo si ufisadi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, swali (a) naomba nilijibu kwa maandishi kwa sababu sina takwimu za kutosha hapa nilipo.

Mhe. Naibu Spika, jibu (b) majenereta haya tumeyanunua wakati wa shida na dhiki pale ambapo tulikuwa waya wetu wa umeme umeungua kwa muda mrefu wa miezi mitatu. Walipotuletea *proposal* ya kutupa majenereta haya labda tulivutiwa zaidi na kuwa na majenereta zaidi kuliko zile *condition* za majenereta haya. Majenereta haya yanatumia mafuta ya *diesel* ya *sulphur prim* yaani *diesel* ambayo haina *sulphur content.* Ni *diesel pure* na ni ghali sana. Sasa kama ni kosa limefanyika kwa sababu tulivutiwa na hiyo haja ya kuwa na majenereta wakati ule wa dhiki, lakini serikali itafika wakati tutazungumza kwa pamoja na kutafuta suluhu. Suluhu ni mbili, ama serikali itupe fidia au itupe ruhusa ya kuongeza *tariff* za umeme. Moja katika hilo likitendeka majenereta yatawashwa na kutakuwa hakuna tatizo.

Nam. 180

Tatizo la Maji Mjini na Vijijini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Tatizo la maji bado ni sugu katika Mji wa Zanzibar na maeneo mengi ya nchi yetu. Katika kufuatilia kwangu nimegundua kuwa visima vingi ingawa havitoshi vinafanya kazi nzuri, isipokuwa ikitokea mtambo wa kisima kuharibika kunahitajika *crane* ambayo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hawana. Inaonekana tatizo la maji sio mjini tu lakini kwenye Mikoa na

Wilaya suala hili linaonekana kuwa kubwa zaidi na kibaya zaidi ni kuwa hakuna wataalam wa kusaidia endapo tatizo limetokea.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupata kifaa hicho muhimu kwa ajili ya kupunguza tatizo la maji Zanzibar.
(b) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa tatizo hilo linaweza kupungua endapo Serikali itafungua Ofisi za Wizara ya Maji kwenye Mikoa na Wilaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 180 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, *ZAWA* hivi sasa ina upungufu wa vitendea kazi na wataalam. Mhe. Naibu Spika, *ZAWA* ina *crane* moja ambayo ni kongwe sana. Hata hivyo, katika mikakati ya wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inategemea kununua crane nyengine moja mpya pamoja na kuwasomesha wafanyakazi wake kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali halijamalizika kwa sababu liko (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza swali hili lilikuja kama ni ushauri si swali lililokamilika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri ameyajibu maswali haya kwa mpigo (a) na (b) kwa pamoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba hiyo *ZAWA* hawana *crane* wana sanamu tu kwa muda huu. Mhe. Naibu Spika, swali (b) hawaoni kuwa sasa hivi wakati umeshafika wa kujitegemea wenyewe na wasitegemee msaada kwa muda mrefu. Je, hiyo *crane* itanunuliwa lini na hizo mbio sijui zinaanzia wapi mpaka wapi kwa sababu kwa muda mrefu hapa majawabu yako tunapata wizara iko mbioni na hili tatizo limekuwa sugu kwa muda huu.

Mhe. Naibu Spika, swali © Mhe. Naibu Waziri alisema ni jukumu lako kipindi kifupi kuwa kila mwananchi atapata maji. Tunakaribia katika mwezi mtukufu wa Ramadhan kuna majimbo hata maji hawajayaona. Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia hao kutatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, serikali kwa jumla ina jukumu la kuwapatia wananchi wake maji safi na salama. Serikali imekasimu kazi hii kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kusimamia shughuli hii. Wizara inajua kwamba kazi hii ni ngumu, wizara inajua kwamba nchini kuna matatizo ya maji sio kila mwananchi anapata maji safi na salama. Pia nilipokuwa nasoma bajeti yangu nilisema angalau asilimia zaidi ya 70 wananchi wanapata maji safi na salama. Kwa kipimo kama hicho kwa nchi za Kiafrika nchi masikini ni kipimo kikubwa sana. Tumeweza kunufaika na kubahatika na kuweza kutoa maji safi na salama kwa wananchi wetu wengi.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikisoma bajeti yangu pia nilisema tatizo hili mwaka 2013 litaondoka. Sasa ukiniuliza leo, leo bado ni mwaka 2011 haujafika mwaka 2013. Naomba tuwe na subira tusaidiane ili tatizo hili tulimalize. Lakini kupiga makelele wakati haujafika tatizo hili haliwezi kuondoka.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba Wazanzibari kwa sasa zaidi ya asilimia 70 wanapata maji. Je, anaweza akatwambia ni Wazanzibari wangapi kwa Mjini Magharibi wanapata maji ili na wale wa Kusini na Kaskazini Pemba waone kwamba kweli asilimia 70 ya Wazanzibari wanapata maji.

Mhe. Naibu Spika, swali (b) Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wana mpango wa kununua *crane* mpya. Je, Wazanzibari wawaamini vipi kwamba wanaweza wakanunua *crane* mpya yenye kiwango wakati wameshindwa kununua majenereta 32 yenye kiwango.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi ametaka nimpe takwimu za wananchi wangapi wanapata maji Mjini Magharibi, wananchi wangapi wanapata maji Kusini na Kaskazini Pemba. Takwimu hizo zipo na nitamletea kwa maandishi za Zanzibar nzima sio za Kusini na Kaskazini Pemba, Mjini Magharibi Unguja na kadhalika.

Lakini jibu (b) hakuna uhusiano hata kidogo kati ya jenereta, uendeshaji wake, ulipiaji wake wa gharama na ununuzi wa *crane* moja mpya. Ununuzi wa *crane* pesa zake ziko katika bajeti hii, tukimaliza bajeti tunanunua *crane* ya kutolea hivyo visima vitakavyoharibika na kadhalika. Hiyo haitaki mafuta wala haitaki umeme, *crane* ikinunuliwa wataalam wapo wataitumia. Majenereta ni shughuli za umeme, shughuli za mafuta na kadhalika. Vituo hivyo viwili Mhe. Naibu Spika, havilingani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mabadiliko ya tabia nchi hupelekea vyanzo vya maji yetu kupungua sana na maji kutoka ardhini vile vile kupungua. Kwa kuwa kuna baadhi ya nchi ambazo uchumi wao ni wa kawaida tu kama hivi Zanzibar wanamudu kupata maji kupitia maji ya bahari. Kwa kuwa sisi Zanzibar visiwa vyote viwili vimezungukwa na maji ya bahari.

Je, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo kwa kweli inaongozwa na safu ya wataalam itafikiria kuanzisha kufanya *distillation* ya yale maji chumvi ili tukapata maji safi ya kunywa na hata chumvi ya kutumia. Ni lini serikali ina mpango huo jambo ambalo litapunguza hata matumizi ya serikali katika kutafuta maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi ameuliza ni lini serikali itafikiria kuyageuza maji ya bahari yawe maji ya kutumia kwa wananchi. Nasema haja itakapotokea. Kwa hivi sasa akumbuke nilivyosema juhudi iliyochukuliwa na Serikali ya Watu wa China kutusaidia kuondosha tatizo la maji, kutuchimbia visima 32 pamoja na hayo mabadiliko ya hali ya hewa.

Sasa baada ya kumaliza juhudi hizo na bado matatizo ya maji yapo upungufu upo, serikali itaanza kufikiria kufanya hili suala la *distillation* ambalo amelizungumza. Wazo ni zuri wenzetu walioko jangwani wanatumia kazi hiyo, bahati nzuri sisi hatuko jangwani na bado matatizo madogo madogo ya maji tukiweza kuyakabili na kuyaondosha nadhani tutalimaliza suala la matatizo ya maji.

Mhe. Naibu Spika, iwapo mpaka hapo bado matatizo ya maji yatakuwepo tutaweza kuliangalia suala lile alilolizungumza. Ni suala muhimu, ni jambo ambalo linafanywa na wenzetu, lakini nadhani akubaliane na mimi kwamba bado sisi hatujafika katika kiwango hicho.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante tunaendelea lakini kabla ya kuendelea pana tangazo kidogo. Waheshimiwa Wajumbe juzi Jumamosi kulikuwa na mashindano ya mpira wa miguu, kufukuza kuku, kuvuta kamba, sasa naomba nitaje *list* na matokeo yaliyotokea. *List* yetu ya wachezaji iliwakilishwa na namba 1 Mhe. Jaku Hashim Ayoub, namba 2 Mhe. Abdillah Jihad Hassan, namba 3 Mhe. Subeit Khamis Faki, namba 4 Mhe. Mohammed Said Mohammed, namba 5 Ndugu Amour Moh'd Amour, namba 6 Mhe. Abdalla Mohammed Ali, namba 7 Mhe. Omar Ali Shehe, namba 8 Mhe. Hamza Hassan

Juma *(Captain)*, namba 9 Mhe. Ali Abdalla Ali, namba 10 Mhe. Ali Mzee Ali na namba 11 Mhe. Salum Amour Mtondoo.

Reserve walikuwa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ambaye alicheza kidogo, wa pili Mhe. Ali Salum Haji nae alicheza, wa tatu Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) alicheza na yeye, wa nne Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nae alicheza, wa tano Mhe. Salim Abdalla Hamad, wa sita Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, wa saba Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), wa nane Mhe. Mussa Ali Hassan, wa tisa Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, wa kumi Mhe. Hassan Hamad Omar, wa kumi na moja Mhe. Ussi Jecha Simai, wa kumi na mbili Ndugu Faki Suleiman Abdalla na wa kumi na tatu Ndugu Fuad Rashid. Kocha wetu alikuwa Mhe. Juma Duni Haji (Babu). Waheshimiwa wanawake waliofukuza kuku ni Mhe. Sira Ubwa Mamboya, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Waheshimiwa wanaume waliofukuza kuku ni Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Subeit Khamis Faki na Ndugu Faki Suleiman Abdalla. Mchezaji bora ni Mhe. Abdalla Mohammed Ali kapata medali ya dhahabu kwa hivyo tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mgeni rasmi alikuwa Mhe. Mgeni Hassan Juma. Waheshimiwa wahamasishaji kwa mchezo huu wa kwanza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Matokeo ya mpira wa miguu dakika zote 90 tumetoka *draw* magoli mawili kwa mawili. Kwa hivyo, tukaingia kwenye matuta wenzetu wakapata penalti 6 sisi tukapata 5, wao ndio walioshinda. Uvutaji kamba mara zote mbili tumeshinda Baraza la Wawakilishi na tumepata kikombe. Kufukuza kuku wanawake kashinda Mhe. Kazija Khamis Kona. Upande wa wanaume hatukupata kitu. Taarifa hizi zimeletwa na Mlezi wa Timu yetu Meneja Mkuu Mhe. Omar Yussuf Mzee. Naomba kuwasilisha.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunikirimu pumzi zake zenye kunipa uhai na uzima.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Magharibi ambao wamenileta kwenye Baraza lako hili tukufu niwawakilishe.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu kwa hawa wafuatao kwa sababu bajeti hii ni ya mwanzo tangu kupata uteuzi wa kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ni kwa Wilaya yangu ya Magharibi Unguja kunipendekeza kuwa Mwakilishi wao wa Nafasi za Wanawake na Baraza Kuu la Taifa la CUF kuniteua kuwa mwakilishi. Nawaahidi sitowaangusha. Mhe. Naibu Spika, pia nakushukuru wewe, Spika, pamoja na viongozi wako ambao wanakusaidia Wenyeviti wako na Mwenyezi Mungu atawalipa kheri katika kazi ngumu mnayoifanya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, pia natoa shukrani zangu kwa viongozi wangu wakuu wa chama kwanza Mwenyekiti wangu Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Makamo Mwenyekiti Mhe. Machano Khamis, Katibu Mkuu wa chama changu Maalim Seif Sharif Hamad kwa mashirikiano yao wanayonipa ya kazi zangu katika Wizara lakini pia kazi zangu za uwakilishi za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, pia namshukuru sana Waziri wangu kwa miongozo na mashirikiano yake anayonipa ili kufanikisha kazi zetu za wizara.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali baada ya kupendekezwa na chama changu. Namuahidi sitomuangusha nitafanya kazi kwa bidii na maarifa kwa maslahi ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mwisho si kwa umuhimu naishukuru sana familia yangu mume wangu mpenzi, mama na baba yangu, watoto wangu, ndugu zangu kwa mashirikiano, miongozo na maliwazo wanayonipa ambayo yananisaidia sana pale ninaposhindwa na kazi za ujenzi wa taifa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba sasa nianze Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi. Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe ambao walichangia idara hii ni kama wafuatao:

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
3. Mhe. Omar Ali Shehe

4. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
5. Mhe. Subeit Khamis Faki
6. Mhe. Ashura Sharif Ali
7. Mhe. Raya Suleiman Hamad
8. Mhe. Nassor Salim Ali
9. Mhe. Mussa Ali Hassan
10. Mhe. Mohammed Said Mohammed
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Salim Abdalla Hamad

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mhe. Issa Haji Ussi, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Asha Abdu Haji na Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Naibu Spika, katika idara hii Waheshimiwa Wajumbe walitaka tuangalie vizuri utaratibu wake wa kuanzishwa na kuendeleza skuli hizi za maandalizi kwa kuwapatia walimu vifaa vya kutosha vya mafunzo, pia kupunguza mzigo wa kuchangia kwa vile hali ya wananchi iko chini sana.

Mhe. Naibu Spika, pia tulielezwa ni kwa nini skuli za maandalizi za serikali ni chache mno kulingana na za watu binafsi. Mhe. Naibu Spika, katika eneo ambalo wizara imejipanga kulishughulikia ni pamoja na elimu ya maandalizi. Kisera elimu ya maandalizi ni sehemu ya elimu ya lazima, hivyo katika utekelezaji wake ni kweli kumejitokeza changamoto nyingi zikiwemo upungufu wa walimu wenye sifa, uhaba wa vifaa na skuli yenyewe.

Hata hivyo, niwashukuru wananchi kwa mchango wao mkubwa katika hili ambapo skuli nyingi za binafsi zimeanzishwa ambako sera yetu ndivyo inavyoeleza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuimarisha hili tunatatua matatizo kama hivi ifuatavyo. Kuwapatia mafunzo walimu kupitia vituo vya *TC* zetu za maandalizi zilizopo Michakaeni Chake Chake, kituo cha maandalizi Saateni Unguja, kituo cha *Zanzibar Madrassa Resource Centre* Unguja, vyuo vya ualimu vya Mazizini na Micheweni kutoa taaluma hii kwa wanafunzi wanaosomea ualimu.

Mhe. Naibu Spika, pia uko mpango mkubwa wa kuwapatia walimu katika miaka mitano hii juu ya mafunzo ya maandalizi kupitia redio na TV. Mpango huu unajulikana kama *Zanzibar Upgrading Through Radio (ZUTRA).*

Mhe. Naibu Spika, sera ya elimu inahimiza na kuhamasisha wananchi na taasisi nyengine mbali mbali kufungua skuli hizi ili kusaidia serikali yao. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe tushirikiana ili sera hii itekelezeke.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya kuporomoka kwa nidhamu ya wanafunzi kunachangia zaidi mfumo wa sasa wa matumizi wa adhabu mbadala maskulini. Mhe. Naibu Spika, suala la nidhamu katika malezi ya watoto linamgusa kila mtu katika jamii. Tukubali kuwa mabadilko ya ulezi yamejitokeza kutokana na kuwacha utamaduni, silka na hulka zetu kutokana na mabadiko ya maendeleo ya dunia ikiwemo utandawazi.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa kutumia adhabu mbadala katika taasisi zetu na jamii umelenga zaidi kujenga mahusiano mema baina ya watoto wetu, wazazi na walimu na sivinginevyo Waheshimiwa Wajumbe. La muhimu na la kuangalia sio bakora kuwa ni suluhisho la kuhakikisha nidhamu, lakini ni kuona ni kwa kiasi gani watoto wetu tunawapa malezi sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, skuli za maandalizi ni sehemu ambayo bakora au lugha chafu na kadhalika ni marufuku, tunaonaje nidhamu za watoto wetu hawa, tuangalie vigezo hivyo. Tuhimizane kubadilika na kushirikiana kwa kuona kuwa adhabu zenye kumfunza mtoto nimuhimu kuliko adhabu zenye kujenga uhasama baina ya wazazi, walimu na wanafunzi. Kuadhirika kimwili na kisaikolojia tunapunguza hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kulikuja hoja ya kutaka kujua ni kwa nini baadhi ya skuli huchukua hatua za kuwafukuza watoto skuli na kuwarejesha majumbani kwa sababu tu hawajachangia fedha za skuli. Suala la michango ya maendeleo iwe ya huduma ya elimu, maji au afya ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Hakuna michango maalum kwa wananchi kuchangia maendeleo ya skuli na elimu kwa jumla.

Kila mwananchi au taasisi inawajibu wa kuhakikisha watoto wetu wanapata haki ya elimu katika mazingira bora na rahisi. Hata hivyo kutokana na vurugu za maskuli kuchangia michango bila utaratibu mzuri, Baraza lako tukufu lilieleza wizara kwa umuhimu wake kuunda muongozo maalum utakaowezesha utaratibu kwa wazazi kuchangia. Wizara ilitekeleza hilo na kuandaa muongozo uitwao, muungozo wa kazi nambari 10 juu ya sera na utaratibu wa uchangiaji wa gharama za elimu katika skuli za serikali. Muongozo ulieleza aina na kima cha mchango wa fedha tena mara moja kwa mwaka na kwa ngazi ambazo mwanafunzi yuko, iwe ni maandalizi, msingi au sekondari au vyuo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa michango hii inasaidia sana katika kuendesha maskuli yetu na kupunguza mzigo mzito pamoja na kuipa fursa na kushughulikia mambo mengine ya kijamii, sio busara utaratibu huu ukafutwa. Kasi iliopo ni kubwa tuunge mkono, wizara itaendelea kuhakikisha usimamizi na matumizi bora ya michango hii kwa kushirikiana na kamati za skuli.

Mhe. Naibu Spika, walimu ni sehemu ya jamii na zaidi walimu ni kiyoo na kigezo kwa kauli na vitendo vyema kwa jamii, iwe ya wanafunzi, wazazi na kadhalika. Kwa hivyo, tendo la kuchangia maendeleo ya skuli na elimu kwa jumla ni haki na fursa na ni wajibu wao pia.

Baadhi ya skuli walimu kwa hiyari zao huamua tu kuondoa kero zao mbali mbali ama za binafsi au za kiskuli kwa kuchangia fedha au vifaa kwa makubaliano yao ya pamoja. Wizara haina ukalifishaji wa walimu katika michango. Michango wanayotakiwa ni ile ya makubaliano ambayo walimu hupaswa kuchangia mara moja tu kwa mwaka. Michango hiyo yote kwa jumla haizidi Shs. 5,000/- kwa mwaka.

Michango yenyewe ni tamasha la elimu bila ya malipo ni Shs. 1,000/-, juma la elimu ya watu wazima ni Shs. 1,000/- maendeleo ya vituo vya walimu 90 ni Shs. 1,000/-, siku ya walimu duniani ni Shs. 1,000/- na michango ya mwenge ni Shs. 1,000/- hutegemea na wilaya. Kama walimu kuchangia Shs. 5,000/- kwa mwaka ni mzigo, basi naomba Waheshimiwa Wajumbe tuungane katika kuhamasisha na kuelimisha jamii zetu majimboni, kuhusu kuchangia maendeleo yetu.

Suala la wanafunzi kuchangia elimu kupitia kwa wazazi na walezi wao ni suala la wajibu. Wizara haijatoa agizo la kuwafukuza au kurarejesha wanafunzi nyumbani ambapo wazazi wao hawajatoa michango. Hilo Mhe. Naibu Spika, ni kosa. Walimu Wakuu watumie busara kama muongozo ulivyoeleza ili michango ipatikane. Aidha, nawaomba wananchi kuwa karibu na skuli na kamati zao za skuli katika kutatua changamoto la migogoro inayojitokeza maskulini.

Mhe. Naibu Spika, wazazi kuchangia ni wajibu wao, moja ya malengo yetu ya Mapinduzi matukufu ni kujenga nchi yetu hii sisi wenyewe. Hoja ya maadhimisho ya sherehe za walimu upangwe utaratibu maalum na uwe ni kila mwaka. Mhe. Mwenyekiti, sherehe hizo ni pamoja na tamasha la elimu bila malipo na siku ya walimu duniani na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya wakati muda mwingi unatumika pamoja na harama kubwa ya uendeshaji. Ushauri wa kupangilia utekelezaji tunaupokea

na tutaendelea kuufanyia kazi. Hata hivyo, kuwa na tahadhari kubwa katika utaratibu huu kunatokana na ile ladha ya sherehe na lengo la upatikanaji wa vipaji vya watoto wetu katika fani za michezo na utamaduni.

Mhe. Naibu Spika, pia kulijitokeza hoja ya baadhi ya skuli kuwa na upungufu mkubwa wa walimu unaosababisha kukosa haki ya elimu kikamilifu na kusababisha utoro kwa baadhi ya wanafunzi. Mhe. Naibu Spika, wizara imeelewa hali ya upungufu wa walimu katika skuli zetu za majimboni. Kwa mfano Matemwe, Pwani Mchangani, Ukongoroni, Mwachealala, Jambiani, Michamvi, Charawe, Micheweni, Mtoni na skuli nyenginezo. Tunawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba jitihada ya kuziba mapengo haya katika zoezi linaloendelea sasa la uhamisho na baadae kutegemea ajira itakayofanyika katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la kuwahamisha walimu katika mikoa yetu tunalizingatia sana kwa masafa ili walimu wasipate usumbufu mkubwa na pale inapobidi basi posho ya walimu zitolewe hasa katika zile sehemu ambao hakuna nyumba za kuishi walimu.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ni kuombwa wizara kuvipitia vyuo vya Kurani na madrasa na kuvipa nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Mhe. Naibu Spika, kisheria vyuo vya Kurani kuvisajili na kuuendeshaji viko chini ya Afisi ya Mufti wa Zanzibar. Kama Waheshimiwa Wajumbe walivyoeleza, kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inawajibika katika kuhakikisha elimu nchini inakwenda kama taifa tunavyotegemea. Basi kwa njia moja au nyengine ni wajibu wetu kushughulikia na ndio maana wizara yangu imeweka sehemu maalum na maafisa wake wanashughulikia elimu hii.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yetu kuwa tumetoa mafunzo kwa walimu 800 na kwamba mwaka huu tutaendelea hivyo hivyo na walimu wapatao 1,000 hali itakavyoruhusu. Aidha, tunategemea kuwatafutia vifaa kwa kupitia wahisani mbali mbali. Suala la posho ni mzigo kwa wizara, ila inaendelea kuwaomba wananchi na hasa wale wenye uwezo waendelee kuchangia hatua za kuwasaidia walimu wetu. Kutoa huku hatupotezi ile tunawekeza katika maisha yetu ya kudumu huko Akhera.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya elimu mjumuisho iliyoanzishwa na skuli zetu ni mzigo kutokana na changamoto nyingi zilizozikabili skuli. Wanafunzi wenye ulemavu na wazazi wenyewe, wizara ikabiliane na wizara hili ili kutoa fursa kwa watoto wote kufaidika na haki elimu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na sera yetu ya elimu ya hapa kwetu Zanzibar itatolewa kwa wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote wa rangi, dini, kabila wala eneo analotokea mtoto. Uwezo wa aina ya ulemavu hii ndio zana ya elimu mjumuisho. Ni kweli kwamba changamoto zipo katika uendeshaji wa zana hii ikiwemo upungufu wa walimu waliobobea katika sifa ya kufundisha.

Mhe. Naibu Spika, watoto mchanganyiko ni mahitaji ya upungufu wa vifaa na gharama msongamano wa watoto madarasani nakadhalika. Hata hivyo, wizara imefanikiwa kuzikabili changamoto hizo katika nyanja mbali mbali, zikiwemo kuwapatia mafunzo walimu katika fani mbali mbali kama uoni, lugha ya alama, ulemavu wa akili na kadhalika. Kupata misaada mbali mbali ya utaalamu na uendeshaji kutoka jumuiya na mashirika ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kuanzisha mafunzo ya ualimu na elimu mjumuisho katika Chuo cha Kiislamu Mazizini. Kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa wanaosimamia elimu mjumuisho. Kuanzisha sera ya elimu mjumuisho ambayo iko katika hatua nzuri, sera hii itakapofika hatua na maelezo ya ufanisi namba wananchi tuwe na subra.

Mhe. Naibu Spika, kwa nafasi hii nachukua fursa ya kuwashukuru washirika wa Jumuiya zote za kimataifa na za kitaifa zinazoendelea kutusaidia katika uendeshaji wa sera yetu hii. Tunaahidi kutumia misaada hii kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia ilijitokeza hoja ya kwamba timu yetu ya wanafunzi walioshiriki mashindano ya Umisenta baada ya kurejea na ushindi mnono. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inashughulikia kikamilifu suala la safari ya wana michezo kama inavyofanya miaka yote. Sisi kama wizara tunagharamia safari hii kwa gharama ya Shs. 17,000,000 kama ifuatavyo.

Safari ya ZNZ/Kibaha/ZNZ,
Posho ya wanafunzi,
Posho ya walimu na makocha,
Posho ya viongozi,
Posho ya madaktari,
Gharama za madawa,
Gharama za vifaa na mavazi na fedha za dharura.

Aidha, Baraza letu la Michezo la wizara walianguka kutafuta vifaa ghali vya wahisa. Kwa hili nachukua fursa hii kwa jumuiya kuwashukuru watu wa Korea kwa kuwapatia washiriki wetu 117 viatu na T. Shirt vilivyosaidia katika huduma za wanamichezo hawa.

Pia kulizuka hoja ya kuwa kumezuka mtindo wa baadhi ya walimu kuwahamisha watoto katika skuli wanazowafundishia na kuwapeleka skuli nyengine ili kutafuta fursa ya kufaulu mchipuo.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya suala la uhamisho wa mtu yeyote awe mwalimu au raia mwengine ni fursa iliyowazi katika misingi na sababu inayokubalika. Aidha, tukubali kuwa skuli zetu zinatofautiana katika mazingira ya kiutendaji na hivyo wazazi kushawishika kutafuta maeneo yenye tija.

Mhe. Naibu Spika, sisi kama wizara tunahimiza na kuhakikisha kuwa skuli zetu ziko katika ugawaji sawa katika fursa ya kutoa elimu iliyo bora. Niliwataka tu walimu wafanyekazi kwa kujituma, maarifa, uadilifu na uzalendo ili sura kama hii iliyoelezwa isijitokeze tena.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya wanafunzi wenye ulemavu kupunguziwa michango ya skuli. Mhe. Naibu Spika, suala hili tayari limeshaelezwa kwa walimu wetu maskulini pamoja na kamati za skuli, ambao ni wasimamizi wetu huko. Tunaendelea kuwakumbusha walimu wetu pamoja na kamati za skuli kuchukua hatua hizo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Hapa kulijitokeza hoja ya walimu ambao wamemaliza masomo ya cheti kuajiriwa. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa sasa inafanya upembuzi yakinifu kwa kujua mahitaji halisi ya walimu maskuli. Zoezi hili litakapomalizika litasaidia kujua kwa undani, ni skuli ngapi hasa zinahitaji walimu na ni walimu wa aina gani.

Tuna matumaini kuwa walimu hawa waliomaliza masomo kwa ngazi ya cheti, wanatarajiwa tutawaajiri hatua kwa hatua kutegemeana na mahitaji ya walimu kwa maskuli, pia kutegemea uwezo wa serikali kupata fedha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hoja ya hatimiliki na kuvamiwa maeneo ya skuli. Wizara yangu kwa sasa imeanza mikakati ya kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda maendeleo ya skuli kwa kupitia kamati za skuli. Hasa ukizingatia kuwa mahitaji ya skuli yanaongezeka siku hadi siku.

Vile vile tumeanza mazungumzo ya awali na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kuona ni njia gani nyepesi na kwa gharama nafuu katika kupatikana kwa hatimiliki zetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wanashirikiana na skuli katika kupata hatimiliki.

Mhe. Naibu Spika, hoja kuhusu utaratibu wa upatikanaji kwa marimbikizo ya walimu kwa upande wa Pemba. Tayari wizara yangu imeanza kulipa malimbikizo kwa walimu waliomaliza masomo kwa ngazi mbali mbali. Tumeanza toka mwezi wa Mei, mwaka 2011 hadi sasa jumla ya walimu 141 wameshalipwa malimbikizo yao. Jumla ya Shs. 38,170,397 zimelipwa. Wizara yangu itajitahidi kulipa malimbikizo ya walimu waliobakia katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu muundo wa utumishi wa walimu. Wizara imetengeneza muundo wa utumishi kwa walimu kwa mwaka 2010 na kuridhiwa na serikali. Kwa sasa wizara inasubiri muundo ambao umetengenezwa na wizara ya utumishi wa wafanyakazi wote ili kuangalia kwa kiasi gani walimu watanufaika na muundo huo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Idara ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliochangia katika hotuba yetu ambao wamegusa idara hii ni wawili. Nao ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Mohammed Haji Khalid. Mhe. Mohammed Haji Khalid alizungumzia mafunzo ya kompyuta na *internet* katika skuli zote, huku baadhi zikikosa huduma ya umeme. Je, wizara itatusaidiaje suala hili.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuweka umeme maskulini ni suala ambalo linashughulikiwa na kamati za maskuli na wananchi kwa kupitia michango inayopatikana hapo, pamoja na kushirikisha viongozi wote wa majimbo. Wizara kwa upande wake inasaidia viongozi hao kuwaunganisha Shirika la Umeme ili kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa.

Sambamba na hilo wizara kwa mashirikiano na washirika wa maendeleo kama vile *USAID* inafikiria kuweka umeme mbadala *solar power*, kwa sehemu ambazo itakuwa ni vigumu kufikia *grade* ya taifa. Vile vile utunzaji wa vifaa hivyo na kuhakikisha kuwa vyumba ambavyo ni salama kwa kuweka vifaa hivyo itabakia kuwa ni suala la msingi la kuwapatia vifaa hivyo. Suala hilo lipo kwenye dhima ya uongozi wa skuli.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumaliza suala hilo napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa mafunzo ya kompyuta kwa walimu yanatolewa kwa kupitia vituo vya walimu Unguja na Pemba, ambapo vyote vinatoa huduma ya umeme.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alisema kuwa vyama vyote vya CCM na *CUF* wakati wa kampeni vilieleza dhamira ya kuhakikisha kwamba kila mtoto anapata kompyuta. Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kukubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi, kuwa baadhi ya viongozi wetu walieleza dhana hii ya kila

mtoto kupatiwa kompyuta. Hata hivyo, wizara yangu kwa mashirikiano na washirika mbali mbali wa maendeleo itahakikisha kuwa kila skuli ya serekali inapatiwa kompyuta na sio kila mwanafunzi kama ilivyosemwa.

Sambamba na hili wizara yangu itahakikisha idadi ya makopyuta maskulini inaongezeka kwa kadri hali itakavyoruhusu. Wizara pia itazipatia kompyuta vituo vyote vya ualimu vya *TC* zetu pamoja na vyuo vya ualimu vya Unguja na Pemba. Vile vile wizara yangu inashirikiana na *NGOs* kama *Computer for Zanzibar Schools*, husaidia kompyuta katika skuli zetu. Aidha, skuli mpya za kiwilaya ambazo ujenzi wake utamalizika hivi karibuni, pia skuli zetu hizo zitakuwa na kompyuta.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Shirika la Huduma za Maktaba. Waheshimiwa Wajumbe ambao walichangia hoja hii ni wawili nao ni Mhe. Said na Mhe Ismail Jussa Ladhu. Tulishauriwa kuanzisha maktaba za wilaya. Mhe. Miongoni mwa malengo ya wizara imeelezwa kuwa katika sera ya elimu ni kuwashawishi uanzishwaji wa maktaba za wilaya. Kwa kuanza wilaya imeanzisha maktaba katika vituo vya walimu ili walimu na wanafunzi pamoja na wananchi kwa jumla wapate huduma za maktaba. Vituo hivyo vipo Dunga Kitogani, Mkwajuni, Kiembesamaki, Bububu na Kituo cha Taifa cha Walimu kilichoko Beit Al Ras Unguja na Mizingani, Michakaeni, Mitiulaya na Wingwi Pemba.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kulijitokeza suala la uhaba wa vitabu. Ni kweli katika baadhi ya masomo, vitabu ni kidogo ambavyo wanafanya "*O level*" na "A level" wanatumia kwa kuhakiki. Shirika la Huduma za Maktaba litaendelea kununua vitabu hivi ili kupunguza tatizo hili. Pia shirika linatoa huduma za *internet* ambapo zinawawezesha watumiaji wa maktaba kuu kuweza kusoma vitabu na majarida mbali mbali katika mitandao mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuwaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi nyengine nije kusimama hapa na kufanya majumuisho ya michango ya wajumbe mbali mbali wa Baraza hili tukufu walioitoa. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba michango yao ilikuwa ni ya maana sana na kusema kweli imefanyakazi ya kuizindua wizara yangu katika baadhi ya maeneo na imekumbusha kwa yale ambayo pengine tulikuwa hatukuyaweka kwenye hotuba yetu, lakini michango ya wajumbe wetu wameiweka.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliochangia katika wizara hii ni 24 na waliochangia kwa maandishi ni wajumbe 10, hivyo jumla wote ni 34. Napenda kuchukua nafasi hii kuwataja majina yao. Kwanza ni;

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman
3. Mhe. Panya Ali Abdalla
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Omar Ali Shehe
7. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
8. Mhe. Subeit Khamis Faki
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Ashura Sharif Ali
11. Mhe. Mohammed Haji Khalid
12. Mhe. Fatma Mbarouk Said
13. Mhe. Raya Suleiman Hamad
14. Mhe. Mussa Ali Hassan
15. Mhe. Nassor Salim Ali
16. Mhe. Mohammed Said Mohammed
17. Mhe. Hija Hassan Hija
18. Mhe. Hassan Hamad Omar
19. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
20. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
21. Mhe. Salum Abdalla Hamad
22. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi
23. Mhe. Professor Ali Mzee Ali
24. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni;

1. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
2. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
3. Mhe. Abdi Mosi Kombo
4. Mhe. Waziri Asiyekuwa na wizara maalum (Mhe. Haji Faki Shaali)
5. Mhe. Asha Abdu Haji
6. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
7. Mhe. Salma Mohammed Haji
8. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
9. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
10. Mhe. Assa Othman Hamad, mchango wake huu kaniletea hivi sasa nanyanyuka kuja hapa kufanya majumuisho.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyoanza Mhe. Naibu Waziri ni kwamba tumeamua kuyajibu masuala haya kwa kupitia katika idara. Kila mjumbe alipochangia katika idara ile basi ndio tunapita kujibu katika idara ile tukimaliza tunakwenda kwenye idara nyengine. Kwa hivyo, napenda kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kwanza nitoe ufafanuzi juu ya Idara ya Elimu ya Sekondari, kwa sababu idara tatu au nne tayari zimeshazungumzwa na Mhe. Naibu Waziri, kwa hiyo mimi naanza na Idara ya Elimu ya Sekondari.

Mhe. Naibu Spika, hapa limechomoza suala kupata ujauzito kwa wanafunzi wa kike na kutaka juhudi za kunusuru wanafunzi hao kupata ujauzito zichukuliwe. Kwa hivyo, wizara yangu itaendelea kuchukua juhudi za kuelimisha wanafunzi wote pamoja na wazazi kuhusu athari kwa wanafunzi kupata ujauzito.

Wizara yangu imeanzisha Kitengo Maalum cha Ushauri Nasaha, ili kuwanasihi wanafunzi wasijiingize kwenye mambo yanayopelekea kupata ujauzito. Mhe. Naibu Spika, wanaomba Waheshimiwa Wawakilishi kushirikiana na wizara yangu pamoja na jamii kwa jumla kupiga vita njia zote zinazopelekea wanafunzi wetu wa kike kupata ujauzito na wale wote watakaobainika kuwapa mimba wanafunzi wa kike, basi hatua haki wizara inaahidi kuzichukua dhidi yao pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, lakini tatizo hili wizara peke yake haitaliweza, sasa wazee majumbani wanatakiwa wachukue hatua za kuhakikisha kwamba wanawashughulikia watoto wao pamoja na kuwaangalia katika nyendo zao.

Hoja nyengine ilikuwa ni upungufu wa walimu wa Sayansi na Hesabati. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inalitambua suala hili na tayari imeshaandaa mikakati ya kutatua tatizo hili. Mikakati hiyo ni pamoja na:

1. Kutoa mafunzo kwa walimu wote wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hesabati kwa kupitia katika Vituo vya Walimu.

2. Kuajiri walimu wa muda waliomaliza kidatu cha sita kwenye masomo ya Sayansi na Hesabati na
3. Kuanzisha mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya Kisayansi Ualimu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Vile vile hoja nyengine katika suala hili ilikuwa ni kutumiwa kwa neno *International* miongoni mwa majina katika skuli binafsi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya skuli za Watu Binafsi zimeanza kutumia neno *International*

ikiwa ni miongoni mwa jina la skuli, wizara yangu kwa kupitia Afisi ya Mrajis wa Skuli imeanza kutoa elimu kwa Skuli Binafsi namna ya kutumia majina yanayoendana na hadhi ya skuli yenyewe.

Hivyo, ili skuli iitwe kwa jina la *International* inabidi itumie mitaala ya Kimataifa. Kwa mfano, ichukuwe wanafunzi wa mataifa mbali mbali hasa wale watoto wa Mabalozi, Maafisa wa Mashirika mbali mbali ya Kimataifa na kadhalika. Pia katika Skuli za *International* kunapatikana mafunzo ya *music*, *drama* na kadhalika kwa wanafunzi. Sasa kama skuli haitimizi masharti hayo haiweze kutumia jina la *International School*.

Mhe. Naibu Spika, skuli kama hiyo iwe na huduma zifuatazo:-

(i) Bwawa la Kuogelea;
(ii) Maktaba iliyokamilika na
(iii) Walimu kutoka ndani na nje ya nchi wawepo pale katika skuli.

Hoja nyengine ilikuwa walimu wenye sifa ya kufundisha Skuli za Msingi kufundisha madarasa ya Sekondari. Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu uliopo sasa wale walimu wa Msingi wenye sifa na uwezo basi hupendekezwa kufundisha madarasa ya Sekondari kwa yale masomo ambayo yanaupungufu ya walimu. Walimu hawa wa Msingi wanaofundisha Sekondari hukaguliwa katika kipindi cha majaribio cha miezi sita kabla ya kuthibitishwa kuendelea kufundisha katika ngazi ya Sekondari kwa masomo husika.

Wizara yangu huwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo kwa kupitia Vituo vya Walimu kwa Unguja na Pemba, yaani huwa tunawapeleka kwenye zile *Teacher Training College (TTC)* kwa ajili ya kupata uzoefu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja moja ilitolewa kuhusu Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Nungwi ambaye alishindwa kuhudhuria katika hafla fupi ya kukabidhi vifaa vya *computer* pamoja na vitabu vya Skuli ya Nungwi, hoja hii imetolewa na Mhe. Subeit Khamis Faki na mimi nimeipokea kwa mikono miwili. Kwa hivyo, nataka nichukue hatua ya kumwita Mwalimu Mkuu huyo kwa suala hili, ili niweze kulifanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa wito mmoja, ili matatizo kama haya yasitokee kwa Waheshimiwa Wawakilishi wanapotaka kwenda kwenye skuli zetu kwa ajili ya kufanya shughuli yoyote ile kama vile kutoa zawadi au msaada basi ni vizuri waijuilishe wizara kabla ya kufeli ule utaratibu wenyewe.

Sasa wizara itakapopata taarifa basi bila ya shaka itachukua hatua ya kumtaka pengine mimi mwenyewe naweza kuhudhuria kwenye hiyo au Mhe. Naibu Waziri ama Katibu Mkuu au Naibu Katibu Mkuu anaweza kuhudhuria na wizara itamjuilisha yule mwalimu mhusika kwamba hapo kwamba kutakuwa na ugeni au zawadi fulani inaletwa na Mheshimiwa fulani na hii itasaidia sana katika kuondoa matatizo kama haya ili yasitokee.

Mhe. Naibu Spika, napenda kufurahi sana kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mara nyingi anapopeleka hayo madeski kwenye skuli zake, basi huwa anatupa taarifa sisi wizara na ndio maana maafisa wangu wanahudhuria katika shughuli hizo. Kwa hivyo, hili ni suala la msingi na ni muhimu kabisa tulifanye katika njia hiyo. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa na hoja ya ufundishaji wa masomo ya ziada. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kumeibuka vituo vinavyosomesha masomo ya ziada kwa wanafunzi katika majengo ya skuli na nje ya skuli wakati wa saa ambazo si za masomo. Wizara yangu imeliona tatizo hili na kutoa dokezo maalum kupitia vyombo vya habari kwa ajili ya kuwaelimisha wazazi, walimu pamoja na wanafunzi wenyewe kuhusu taratibu za kuwa na madarasa ya ziada.

Mhe. Naibu Spika, naomba kueleza kwamba masomo ya ziada katika skuli zetu lazima yaridhiwe na Kamati za Skuli pamoja na wazazi wenyewe. Kwa hivyo, napenda kuchukua fursa hii kutoka wito kwa Walimu Wakuu wote kufuata utaratibu huu na kutoruhusu masomo ya ziada yasiyofuata utaratibu niliyoeleza.

Hoja nyengine ambazo nitajibu hivi sasa zinahusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA)*. Mhe. Naibu Spika, katika suala hili wajumbe 10 walichangia masuala haya nao ni:-

1. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla;
3. Mhe. Saleh Nassor Juma;
4. Mhe. Omar Ali Shehe;
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said;
7. Mhe. Mohammed Said Mohammed;
8. Mhe. Hija Hassan Hija;
9. Mhe. Ali Mzee Ali na
10. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii)

Masuala yanayohusu Chuo Kikuu yalikuwa karibu 15 ni haya yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Chuo Kikuu,
(ii) Hatimiliki ya maeneo,
(iii) Uwiano wa wanafunzi kati ya Shahada ya Sanaa na Sayansi,
(iv) Wanafunzi wanasoma *physics* kutokufanya *practical*,
(v) Hali mbaya ya Dakhalia ya Nkurumah,
(vi) Walimu kuondoa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kujiunga na vyuo vyengine Tanzania Bara,
(vii) Chuo kutokuwa na Makamu Mkuu wa Chuo,
(viii) Chuo kuwa na wahadhiri wengi wa muda,
(ix) Mfanyabiashara kuvamia eneo la chuo katika *Campus* ya Nkurumah na kujenga karakana,
(x) Walimu kuganda katika ngazi ya wahadhiri bila ya kupanda daraja,
(xi) Sifa za walimu wanaotaka kujiunga kuwa wahadhiri katika Chuo Kikuu,
(xii) Tafiti za wizara zote zipewe Chuo Kikuu cha Taifa,
(xiii) Kuanzisha Kigoda cha Mhe. Hayati Abeid Amani Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar,
(xiv) Kuwekeza katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na
(xv) Lini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *Campus* ya Vuga, Nkurumah na Tungu watakaa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, haya ndio mambo muhimu ambayo yamezungumzwa.

Kwa kweli kuhusu suala la Chuo Kikuu cha Taifa kuwa na bajeti ndogo ambayo ni 3.6 bilioni ambayo ndio wameipa safari hii. Mhe. Naibu Spika, Chuo Kiku cha Taifa hujitahidi kueleza mahitaji yao na katika hili sisi huwa tunashirikiana na Wizara ya Fedha na kufanya mjadala na Wizara ya Fedha juu ya suala hili, ili waongezewe fedha, kwa sababu tunataka Chuo Kikuu kisiende kama inavyokwenda Skuli ya Sekondari ya Lumumba au skuli nyengine yoyote, yaani tunataka kiende kama ni Chuo Kikuu chenyewe.

Tatizo lilitokea inakuwa ni suala la fedha kuweko katika Mfuko Mkuu wa Hazina, yaani hilo ndio tatizo.

Lakini pia kuna masuala mengine ambayo mara nyingi watu wa fedha huwa wanataka walijue nalo makusanyo ya Chuo Kikuu yako kwenye kiwango gani. Katika hili tunafanya jitihada ya kutaka kupeleka *auditors* pale, ili tuweze kujua hasa makusanyo katika Chuo Kikuu ni kiasi gani.

Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka huu watustahamilie na mwaka ujao tunategemea kwamba tutakuja vizuri zaidi, kwa sababu tulikuwa tumeshajua kuwa chuo chenyewe kinakusanya kiasi gani na ndio maana Wizara ya Fedha na pengine Wizara ya Fedha ina vigezo vyao wanavyotumia katika kutoa kiwango hicho na hilo tutakuja kulifanya kwenye bajeti ijayo mwakani.

Vile vile kuna suala la hatimiliki maeneo ya Chuo Kikuu cha Taifa hayana Hatimiliki. Mhe. Naibu Spika, hali hii inaonekana katika vyuo pamoja na skuli nyingi za serikali na juhudi za kuomba hatimiliki zinafanywa. Chuo Kikuu cha Zanzibar *SUZA* kimeomba hatimiliki kwa maeneo hasa ya Tunguu hadi leo hatimiliki hiyo bado haijapatikana. Lakini wizara yangu imo kwenye mazungumzo na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ili tuweze kupata hatimiliki kwa lengo la kumiliki hasa na kuweza kuzuia uvamizi.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri *site plan* tunazo na tatizo ni ile hatimiliki, kwa sababu hatimiliki tunaweza kuweka sisi na hata kama hatukuweka sisi basi ikiwepo hatimiliki katika *Baitllmal*, yaani katika udhibiti wa kitaifa wa mali za serikali pia itatusaidia sisi kufika katika Mahakama. Kwa hivyo, hili ni tatizo la tunaendelea nalo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha kuliondoa baada ya muda pengine sio mkubwa.

Halafu kuna suala la uwiano wa wanafunzi kati ya Shahada ya Sanaa na Sayansi, yaani kuna uwiano usioridhisha wa wanafunzi wa shahada ya Sanaa, Sayansi na *Computer*. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Abdalla Juma Abdalla kwamba uwiano wa wanafunzi wanaosoma *SUZA* wa Shahada ya Sanaa, Sayansi na *Computer* ni mkubwa.

Kwa kweli wanafunzi wengi wanasoma Shahada ya Sanaa na hili ni endeleo la wanafunzi walivyo katika skuli za sekondari hasa baada ya mitihani yao darasa la kumi na mbili, kumi na nne au kitado cha sita, kwa sababu wanafunzi wengi wanafaulu katika masomo ya sanaa na kushindwa kwenye masomo ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili linasababishwa na *mindset* ya wanafunzi wetu, yaani wanaamini kwamba sayansi ni ngumu na ukimwambia mwanafunzi achukue *Physics* au *Math* anakwambia aa! Hiyo mimi siiwezi, bora nichukue Kiswahili, Dini na hilo ndilo tatizo ambalo tunalo. Kwa hivyo, kuna haja ya kujenga *mindset* wanafunzi wetu kuelekea kwenye sayansi. Kwa mfano, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe humu ndani ya Baraza walinijia wakaniletea malalamiko yao, kwamba wazee wanataka watoto wao wasome *science*, lakini watoto hawataki na wanataka wasome masomo ya *art*.

Kwa hivyo, tunayo kazi sisi Mhe. Naibu Spika, pamoja na walimu wangu wote skuli kujenda *mindset* na pengine mindset itajengeka vizuri sana wakati tutakapopata vifaa vya *science* maana wakati huo wanafunzi wana-*enjoy* kuona hasa ile *science* maana yake nini wakati tutakuwa na maabara na kila kitu katika skuli zetu. Vile vile kuna suala la wanafunzi wa *Physics* kukosa kufanya *practical* zao mwaka 2010. Mhe. Naibu Spika, ni kweli wanafunzi hao hawajafanya *practical* zao kutokana na ukata wa fedha kama watakosa kufanya *practical* hawatamaliza *program* yao na hivyo hawatahitimu. Kwa hivyo, wanafunzi hao watakwenda kumaliza *practical* zao *University of Dar-es-Salaam* mwaka huu.

Pia chuo kimepata msaada wa vifaa vya maabara kutoka kwa wahisani wa nje. Mhe. Naibu Spika, tatizo letu ni vifaa vya kufanyia hizo *practical* zenyewe. Lakini tunashukuru kwamba Benki ya Dunia imetengeneza *package* ambayo ndani yake kuna vifaa vya maabara kwa ajili ya Chuo Kikuu, ambapo vile vile *tender* kwa ajili ufunguzi wa vifaa vya *Science* kwa *Campus* yetu ya Tunguu tayari imeshafunguliwa.

Kwa hivyo, tunategemea mwakani tatizo hili litakuwa halipo, kwa sababu tayari tutakuwa tumeshapata vifaa ambavyo wanafunzi wetu hawa watafanya hizo *practical* zao.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Dakhalia ya Nkurumah iko katika hali mbaya na chuo kinaelewa hali hiyo na kimepanga kufanya yafuatayo:-

(a) Kwanza kimefanya mchanganuo wa gharama za matengenezo ya ukarabati wa Dakhalia hiyo nazo ni shilingi milioni 150/-,

(b) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*), *ZSSF* na *UTT* Dar-es-Salaam zinatayarisha mpango wa kujenga Dakhalia mpya Tunguu. Tayari mazungumzo na matayarisho wa Dakhalia hiyo yanaendea.

Hoja nyengine ilikuwa ni walimu kuondoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kujiunga na vyuo vyengine Tanzania Bara. Mhe. Naibu Spika, walimu wanaondoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kwenda vyuo vyengine vya Tanzania Bara kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kufuata maslahi, yaani malipo ya Chuo Kikuu cha Dodoma yako juu kuliko malipo ambapo tunayolipa hapa *SUZA*.

Lakini tunayo matumaini kwamba mwaka huu mishahara hii itarekebishwa. Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema anao wasi wasi katika hali hii ya bajeti tuliyonayo kweli tutaweza kupandisha mishahara.

Kwa kweli Wizara ya Fedha mwaka huu imetenga fungu maalum kwa suala la kurekebisha matatizo kama haya ya mishahara, tena liko kwenye kasma yao na tutakapofika kwenye Wizara ya Fedha tutakuta fedha zimekusanywa nyingi sana kwa ajili ya kuja kupambana na matatizo haya baadaye. Kwa hivyo, maelezo ya serikali kwamba mishahara safari hii itanyanyuliwa, basi yatatekelezwa kwa sababu Wizara ya Fedha wameshaweka hizo fedha, isipokuwa bado hayawaja-*allocate* moja kwa moja katika mawizara.

Kwa mfano, ziko wizara ambazo zina matatizo kama vile Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika basi litajichomoza, lakini Wizara ya Fedha wanasema tusiwe na wasi wasi na hilo kwa sababu fedha ziko mahala katika kasma ya Wizara ya Fedha zimewekwa kwa ajili ya kuja kukidhi matakwa haya.

Vile vile hoja nyengine kuhusu Chuo Kikuu kutokuwa na Makamu Mkuu wa Chuo. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu Chuo kwa sasa hakina Makamu Mkuu wa Chuo, hata hivyo hivi karibuni atapatikana Makamu Mkuu wa Chuo, kwa sababu iliundwa kamati kwa ajili ya kupendekeza majina na ilipendekeza majina matatu ya Makamu Mkuu wa Chuo na kamati hiyo tayari imemaliza kazi yake.

Kwa hivyo, majina yaliyopendekeza yatawasilishwa kwenye Baraza la Chuo ambalo litakutana tarehe 21 mwezi huu wa Julai, 2011 na baada ya hapo atapelekewa Mkuu wa Chuo ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi rasmi wa jina moja.

Hoja nyengine kuhusu chuo kuwa na wahadhiri wengi wa muda. Mhe. Naibu Spika, kutumika kwa wahadhiri wengi wa muda katika chuo si jambo geni, walimu kutoka chuo kimoja na kwenda chuo chengine kufundisha ni jambo la kawaida, walimu wa kawaida huchukuliwa kwa sababu ya umahiri wake katika somo au kwa kukosa muhadhiri kama yeye katika chuo.

Kwa kweli *SUZA* inayo upungufu wa wahadhiri ndio maana inawachukuwa walimu hasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Lengo kuu ni wanafunzi wapate kusoma na kuweza kumaliza *programs* zao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya tisa kwamba mfanyabiashara kuvamia eneo la chuo katika *Campus* ya Nkurumah na kujenga karakana. Suala hili ni kweli, lakini

chuo kimemshitaki mfanyabiashara huyo na kesi iko Mahakamani. Sasa hali hii inanifunga mimi kuzungumza mambo mengine zaidi, kwa sababu kesi ikiwa Mahakamani vizuri tusubiri uamuzi wa Mahakama. *(Makofi)*

Walimu kudanga kwenye ngazi ya wahadhiri bila ya kupanda daraja za taaluma. Mhe. Naibu Spika, kupanda ngazi kwa wahadhiri katika Chuo Kikuu kunafuata utaratibu maalum. Katika utaratibu huu pamoja na mambo mengine umezingatia mchango wa kitaaluma wa mwalimu. Kwa mfano, kazi zake za utafiti (*research)*, kusomesha (*teaching)* na ushauri elekezi (*consultation*).

Kwa hivyo, kuna nukta zinatumika katika kutathmini vipengele hivi, kuanzia na *Commission for University (TCU)* imetoa muongozo katika kutekeleza suala hili. Kwa mfano, kama mwalimu atakuwa dhaifu au atachelewa kufanya hayo na kupanda ngazi kwake kutachelewa hivyo hivyo. Kwa maana hiyo, suala hili tunataka walimu wetu hawa tuwawezeshe katika kufanya *research*, yaani tuwashirikishe kwenye *research* mbali mbali, ili tuweze kuona matunda yao na waweze kupanda ngazi au daraja ya taaluma.

Sifa za walimu wanaotaka kujiunga kuwa Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, wote wanazo sifa moja awe anatoka nje ama ndani ya nchi kiwango cha chini cha kujiunga na Chuo Kikuu ni kuwa na *Degree* ya Pili, (*Master Degree*) tena inafuata *PhD*, kwa wale waliowahi kuandika na kuchapisha iwe kitabu au matokeo ya utafiti huwa wana kipaumbele kwa kupata nafasi ya kuajiriwa.

Tafiti za wizara zote zipewe Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, wizara imepokea ushauri huu na pia itategemea wizara nyengine kukubali ushauri huo na *SUZA* haina matatizo na hilo.

Kuanzisha Kigoda cha Mhe. Hayati Abeid Amani Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, pia imeupokea ushauri huo na utauzingatia. Vile vile kuhusu suala la kuekeza katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, inawezekana kuekeza katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Kwa mfano, kujenga Dakhalia nzuri na kuwakodisha wanafunzi na kipato kikirudi kwa kuwekezaji na hapo ndipo fedha zake zitakaporejea.

Kwa hivyo, hali hii tuwashawishi wafanyabiashara wetu au wenye uwezo waekeze katika Vyuo Vikuu kwa kujenga hizi Dakhalia karibu na hivi vyuo au pengine wanashirikiana na wizara wakapatiwa kiwanja humo ndani ya chuo na kujenga Dakhalia, halafu wakarejesha matumizi yao pengine na faida kidogo na kama watakubali wanaweza kukiachia chuo na kuendesha wenyewe na hilo linawezekana.

Suala jengine ambalo linawezekana ni kukunua vitabu na kukipa chuo, ili kufundishe wanafunzi wake. Pia wawekezaji wanaweza kukipatia chuo vifaa vya maabara na hata kujenga maabara zenyewe, hivyo wawekezaji wanakaribishwa katika hatua hii kwenye vyuo vyetu.

Mhe. Naibu Spika, lini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, yaani *Campus* ya Vuga, Nkurumah na Tunguu watakaa pamoja. Mhe. Naibu Spika, wanafunzi hawatokaa pamoja, isipokuwa *campus* zote zitatumika kwa wakati mmoja na kila *campus* itakuwa na shughuli zake za kimasomo.

Kwa mfano, *Campus* ya Vuga itakuwa na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Taasisi ya Elimu Endelevu pamoja na Idara ya *Computer*, kwa upande wa *Campus* ya Nkurumah itakuwa na Diploma ya *Management* ya Elimu na Uongozi, Diploma ya *Science* pamoja na hiyo Dakhalia na *Campus* ya Tunguu itakuwa ni Kitivo cha Elimu, Sanaa na *Science*, Kitivo cha Uhandisi pamoja na Makao Makuu ya Utawala. *(Makofi)*

Kuna hoja hapa ambayo imeulizwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba majengo yaliyokuwa Chuo cha Ualimu yaliyokuwa Beit-el-Ras yarejeshwe kwa Chuo cha Ualimu. Mhe. Naibu Spika, majengo yaliyokuwa Chuo cha Ualimu cha Nkurumah cha Beit-el-Ras yamekabidhiwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na *programs* zilizokuwa zikifundishwa chuoni hapo hasa diploma zimehamishiwa Chuo Kikuu cha Taifa za Zanzibar.

Kwa hivyo, baadhi ya walimu waliokuwa na sifa za kufundisha Chuo Kikuu walichukuliwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na wasiokuwa na sifa walirejeshwa wizarani na kupelekwa taasisi nyengine. Hivyo, lengo ni kuwafanya wanaosomea ualimu wafike shahada ya kwanza (*first degree*) na kuwa walimu bora tangu msingi hadi *secondary*. Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa waombaji wa kusomea ualimu wanapata kusoma diploma na shahada ya kwanza basi hilo halina tatizo na linatekelezwa na hizi *university* zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hapa nataka nizungumze kitu kidogo, tunapokuwa tunataka kuikuza hii taaluma ya kufundisha ualimu, basi tuendane na tabia zinazofanya duniani na wenzetu. Kwa mfano, ni kweli pale Dar-es-Salaam kuna Chuo cha Ualimu Chang'ombe, Chuo cha Ualimu Kleruu kule Iringa, lakini vyote hivi sasa viko chini ya *University of Dar-es-Salaam* na kwa hivyo ndio maana Chuo cha Ualimu cha Nkurumah kikawekwa chini ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA)*, kwa ajili ya kufundisha mafunzo ya ualimu hapo hapo. Sasa

hii kukuza tunapoanza inakuwa na matatizo, lakini baadaye watu wakeshakuzoea itakuwa hakuna matatizo tena.

Kufutwa kwa *Pre University Program*. Mhe. Naibu Spika, kufutwa na *Pre University Program* kunatokana na *Tanzania Commission for University* kupunguza sifa za kuingia chuoni. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2011 muombaji mwenye pass mbili za masomo mawili tofauti na kiwango cha chini cha E anapata kuingia na kusoma shahada ya kwanza.

Hivyo, mpango huu ni kuwezesha waombaji wengi waweze kuingia vyuoni moja kwa moja. Kwa maana hiyo, hakuna haja ya kuchukua wanafunzi kwa *Pre University Program*.

Mhe. Naibu Spika, Chuo kama Chuo Kikuu cha Zanzibar (*SUZA*) kinachukua wanafunzi kutoka Malawi na Kenya, wanafunzi hao wanao mfumo tofauti na wa kwetu, yaani wao hawana kitado cha sita. Kwa hivyo, huhitaji masomo ya mwaka mzima ya *Pre University*, ili kuwekwa sawa na wenzao wa Tanzania, basi mara hii Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilitakuwa kiombe *TCU* kwa barua ili kiruhusiwe kuchukua wanafunzi hao.

Chuo hicho kimeruhusiwa kwa mwaka huu na *TCU* imeeleza kwamba itaweka utaratibu maalum kwa wanafunzi wenye mfumo tofauti na wetu. Mhe. Naibu Spika, hali hii imekuja kwa kufuata utaratibu huu wa *TCU* katika suala la kulinda zile *accreditations* zetu za vyuo.

Nikiendelea na majumuisho yangu sasa nataka nizungumzie kuhusu Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Mhe. Naibu Spika, idadi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba ya bajeti na kugusia masuala yanayohusiana na Idara ya Mafunzo ya Ualimu ni tisa ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii),
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman,
3. Mhe. Panya Ali Abdalla,
4. Mhe. Abdalla Juma Abdalla,
5. Mhe. Subeit Khamis Faki,
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu,
7. Mhe. Mohammed Haji Khalid,
8. Mhe. Raya Suleiman Hamad na
9. Mhe. Mohammed Said Mohammed

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wako watatu ambo ni Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Panya Ali Abdalla wamezungumzia suala la kuendeleza mafunzo ya walimu. Kwa mfano, Mhe. Amina Iddi Mabrouk alieleza kwamba bajeti haikuweka wazi kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar ya kutoa kipaumbele suala la mafunzo ya ualimu na nyumba za walimu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia Idara ya Mafunzo ya Ualimu wizara imeandaa mipango kabambe ya kuendeleza mafunzo ya ualimu kama ilivyoelezwa kwa muhtasari katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 46 hadi 49. Miongoni mwa mambo yanayotekelezwa ni haya yafuatayo: -

Idara imeandaa Sera ya Mafunzo ya Ualimu na sera hii itatoa muongozo, utoaji na uendeshaji wa Mafunzo ya Ualimu Vyuoni na Kazini kupitia Vituo vya walimu. Vile vile idara inashirikiana na mashirika ya ndani na yale ya kimataifa kuendesha miradi inayosaidia utoaji wa mafunzo kwa walimu walioko kazini na vyuoni. Kwa hivyo, baadhi ya miradi inayotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Mradi wa Benki ya Dunia. Kwa kweli mradi huu umetuwezesha kufundisha makundi mbali mbali ya walimu walioko kazini, kama vile mafunzo kwa walimu wanaosomesha Lugha ya Kiingereza kwa madarasa ya msingi, yaani darasa la 5, 6 na 7 hadi sasa walimu 720 tayari wameshapatiwa mafunzo na ifikapo mwezi wa Septemba walimu 220 waliobakia watapatiwa mafunzo hayo.

- Pia mafunzo kwa walimu wa *Secondary* wanaosomesha masomo ya *Science* na *Math* jumla ya walimu 350 tayari wameshapatiwa mafunzo hayo kwa mwaka 2010/2011.

- Mafunzo kwa Skuli za Msingi wanaosomesha Madarasa ya Msingi ya juu, darasa la 5, 6 na 7 kwa masomo ya *Science* na Hesabati, basi walimu hao wapatiwa mafunzo ya kutumia Kiingereza kwa mawasiliano katika ufundishaji wa masomo hayo kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006.

- Mradi wa TZ 21 unadhamini wa *USAID* na kuendesha na *Creative*. Katika mradi huu walimu wanaosomesha Masomo ya Kiswahili, Kiingereza, *Science* na Hesabati katika madarasa ya Msingi ya chini, darasa la 1, 2, 3 na 4 watapatiwa mafunzo ya kutumia *computer* na namna ya kuandaa somo na mbinu za ufundishaji kwa kutumia teknolojia za kisasa.

- Vile vile *SIDA* itasaidia kuwadhamini walimu watakaochukua masomo yafuatayo:-
  (i) Walimu wa Vyuo 15 watasoma Elimu ya Shahada ya Uzamili kupitia mpango maalum utakaoshirikisha Chuo Kikuu Teule. (*Teller made Master Degree Course*),

  (ii) Walimu 20 wa Maandalizi watapatiwa nafasi ya kujiunga na masomo ya Diploma ya Maandalizi yanayotolewa na Chuo Kikuu cha Dodoma,

  (iii) *British Council* nao wanasaidia wizara kutoa mafunzo ya utumiaji wa Kiingereza cha mawasiliano kwa walimu wanaofundisha Skuli za *Secondary*. Mafunzo hayo yanatolewa kwa awamu, awamu ya kwanza imewahusisha wanafunzi 22, ambao sasa watakwenda kuendesha katika mafunzo kwenye vituo vya walimu kwa walimu teule kutoka kila skuli nao wakirejea katika skuli zao, basi watafundisha walimu wanaosomesha Somo la Kiingereza.

  (iv) Ubalozi wa Marekani hapa nchini ulifadhili mafunzo ya Lugha ya Kiingereza kwa walimu 90. Walimu 50 walihudhuria mafunzo hayo katika Kituo cha Ualimu Dunga Unguja na walimu wengine 40 walihudhuria katika Kituo cha Ualimu Wingwi huko Pemba. Ubalozi umeahidi kuendesha mafunzo zaidi baadaye.

Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye anahimiza walimu wetu kufundishwa kutumia Kiingereza katika kufundisha. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo juu juhudi za kuwafundisha walimu wetu wa ngazi zote Somo la Kiingereza na Kiingereza kwa mawasiliano zinafanywa.

British Council kwa kushirikiana na Sauti ya Tanzania Zanzibar wanaendesha vipindi maalum kila siku ya Jumapili usiku kinachofundisha walimu wetu mbinu za ufundishaji Lugha ya Kiingereza. Pia tumeona hapo awali namna ya mashirika mbali mbali yanavyotusaidia kuendesha mafunzo ya Kiingereza cha mawasiliano.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, avute busira kidogo ataona mabadiliko katika skuli zilizopo kwenye jimbo lake. Mhe. Panya Ali Abdalla alitaka kujua Wizara imechukua hatua gani kupunguza tatizo la walimu wa masomo ya sayansi, pia Mhe. Abdalla Juma na yeye ameuliza kwa nini kuna uhaba wa wanafunzi wanaosomea masomo ya sayansi katika Chuo Kikuu cha Taifa yaani *SUZA* na Chuo cha Kiisalam. Nawajibu wote kwa pamoja kwa maelezo yafuatayo. Wizara imehamisha michepuo kwa

sayansi katika skuli za sekondari za Lumumba, Benbella na Fidel Castro hali kadhalika imeanzisha madarasa maalum katika Skuli ya Sekondari ya Benbella kwa wanafunzi wa kike waliofaulu kitado cha tatu na mwenye uwezo wa kusoma masomo ya sayansi. Pia Wizara imezidi kusisitiza kuwa wanafunzi wa kidato cha tano waliofaulu masomo ya sayansi na hesabati waendelezwe na kuwazuia wasibadilishe masomo hayo

Kama tulivyoona katika mradi wa Benki ya Dunia walimu 350 wamepatia mafunzo ya mbinu ya ufundishaji wa masomo ya sayansi, kwa kushirikiana na Agakhan Foundation wizara imeweza kuendeleza walimu wa *grade 3A* ambao hufundisha masomo ya sayansi katika madarasa ya sekondari, mradi huu uitwao *Teachers Advance Program* umewezesha kufundisha mbinu za kufundisha madarasa ya Sekondari kwa walimu 74 wanaume 50 na wanawake 24. Mafunzo hayo yaliendeshwa katika vituo vya walimu vya Kiembesamaki, Dunga kwa Unguja na Michakaeni kwa Pemba baadhi ya wahitimu hao wameweza kujiunga na masomo ya juu.

Kwa zaidi ya mwezi mmoja mafululizo Idara ya mafunzo ya ualimu na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *SUZA* kilitoa matangazo katika sauti ya Tanzania Zanzibar ya wito wa kujiunga na Dipoloma ya Sayansi, idara ya mafunzo ya ualimu ilitoa tangazo maalum la wito wa kujiunga na Diploma ya sayansi katika vyuo vyake, katika gazeti la Zanzibar Leo la Jumatatu tarehe 4/7/2011 bahati mbaya mwitiko bado ni mdogo, sasa nataka walimu wajue kwamba hii nafasi ipo na wajichomoze kwa ajili ya kwenda kufanya.

Mhe. Panya Ali Abdalla anapendekeza Wizara ianzishe chuo cha ualimu wa michezo hapa kwetu Visiwani ili tuache kuwapeleka walimu wetu huko Tanzania Bara, napenda kumkumbusha Mhe. Mheshimiwa kwamba Chuo cha Ualimu Nkurumah palikuwa pakiendeshwa mafunzo ya Diploma ya michezo, kozi imehama baada ya kuhama wanafunzi, wanafunzi wanachukua Diploma ya michezo hutakiwa kusoma somo la michezo ni somo moja la kufundishia pamoja na masomo ya ualimu na si rahisi, hivyo Wizara itajipanga upya na kuona uwezekano wa kurudisha Diploma ya michezo katika vyuo vyetu vya ualimu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman ameiomba Wizara isiue historia ya Chua cha Ualimu cha Nruma na tatizo lake ni kuwa chuo Kikuu kitakapokuja kuhamia katika majengo yake ya Tunguu Chuo cha Ualimu cha Nkurumah kianze upya, Nachukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa kuwa historia ya Chuo cha Ualimu cha Nkrumah bado ipo na itaendelea kuwapo, mabadiliko yaliyopo ni kukituza kama ilivyotokea kwa vyuo vya ualimu vya wenzetu huko Tanzania Bara, ambako Chuo cha Ualimu cha Chang'ombe Dar es Salaam na chuo cha

ualimu cha Kleruu Iringa sasa vimekuwa vyuo vikuu shirikishi na unatoa mafunzo ya ualimu kwa nagazi ya shahada.
Wizara itaendelea na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah kwa kukiita Nkrumah *compass* na masomo yote yaliyokuwa yakitolewa na Chuo cha Ualimu cha Nkurumah kama vile Diploma ya uongozi na Diploma ya Sayansi, yatatolewa hapo hapo na kuengeza kodi nyengine hali kadhalika kumbu kumbu zote za wanafunzi waliosoma Nkrumah zipo na zimehifadhiwa hapo hapo mtu atakayetaka cheti au taarifa yoyote ya Chuo cha Ualimu Nkurumah atazipata.

Mhe. Subati Khamis Faki yeye ni muwakilishi wa jimbo la Micheweni anataka ufafanuzi kuhusu Chuo cha Kiislam, kwanza yeye anataka kujua kama jina la Chuo cha Kiislam Zanzbar limebadilishwa. Hata hivyo hakututajia hilo jina jipya analolijua yeye ila hapa amekuwa akikiita chuo cha Kiislam Mbweni hii ni bahati mbaya tu. Lakini alichokusudi ni Chuo cha Kiislam kilichopo hapo Mazizini.

Jambo ambalo hufanya baadhi ya watu hupita Chuo cha Kiislam Mazizini kama wanavyopita Chuo kiliopo Pemba Chuo cha Kiislam Kiuyu au Chuo cha Kiislam Micheweni ni mazoea tu namjulisha rasmi kwamba jina rasmi la chuo chetu ni chuo cha Kiislam Zanzibar, lakini suala lake la pili anataka kujua sababu za msingi zinazopelekea Chuo cha Kiislam Pemba kutokuwa na gari, zahanati na msikiti.

Suala hili alilileta katika kikao hiki na kujibiwa lakini inavyoonyesha bado anaendelea kulifanyia kazi zaidi ili apate jibu muwafaka, namuomba Mheshimiwa awe mstahamilivu fedha tunazopata za maendeleo kidogo na ndio maana imetuchukua muda mrefu kukamilisha ujenzi wa chuo hicho nategemea yeye atakuwa shahidi wa kueleza maendeleo ya ujenzi yaliyokamilishwa chuoni hapo mwaka 2010/2011 yanayojengwa bweni la wasichana na ujenzi wa holi na vyumba vya ofisi.

Namhakikishia kwamba mwaka huu wa Fedha Chuo kimepangiwa Shs. 50 milioni za maendeleo Shs. 30 kwa matumizi ya kawaida, kutokana na hicho kidogo kilichopatikana basi tutajaribu kupunguza baadhi ya kero ziliopo chuoni, wizara inawajali wanafunzi hao na inataka wapate kila kitu ili mazingira ya Chua na afya za wanafunzi ziwe nzuri.

Namuomba Mheshimiwa asaidie na uongozi wa chuo kutafuta wafadhili ili tuweze kuharakisha upatikanaji wa zahanati pamoja na msikiti, yeye alitaka kujua kwa nini chuo cha Walimu Micheweni hakina wapishi na mlezi wa kike yaani *metron*, namjulisha rasmi kuwa juhudi za kumpata mpishi na mlezi wa kike zimefanywa na hivi karibuni tu wataajiriwa, lakini hata hivyo habari

nilizozipata leo ni kwamba tayari kuna wapishi wawili wameshaajiriwa. Mmoja anaitwa Biasha na mmoja anaitwa Bifatma. Vile vile wapo metron wawili mmoja Biasha na mmoja Bifatma na wapishi wamo wawili mmoja anaitwa Binusura na mwengine mwanamme jina lake sijalipata vizuri lakini tayari wameshaajiriwa.

Kwa hivyo Mheshimiwa nadhani ataridhika kwamba hiyo jitihada anaendelea nayo na kama itabidi kuongeza tutaongeza, katika suala ambalo amelizungumza yeye katika suala la gari pale nalo pia tutalifanyia kazi, ile gari ambayo ipo pale tumeijenga bodi ili wanafunzi wanapoingia mle wasivujiwe lakini hata hivyo sio kwamba ndio mwisho wa juhudi zetu, juhuzi zetu zitaendelea kuona kwamba inapatikana ile gari kubwa ambayo iliyopo pale na pia kutafuta gari ambayo ya wastani ambayo itaweza kutoa huduma ndogo ndogo tofauti na ile kubwa iliyopo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu Muwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe anaiomba Wizara kuiangalia upya bajeti ya idara ya mafunzo ya ualimu kwani inazidi kupungua mwaka hadi mwaka, napenda kumjulisha Mheshimiwa kwamba kinachofanyika sasa ni kutenganisha kasma za vyuo vyetu kutoka bajeti ya Idara, hivyo vyuo vimetengewa bajeti yake. Pia fedha nyingi za msaada zimeelekezwa katika Idara ya Mafunzo ya ualimu kwa kutumia miradi tuliyoitaja hapo kabla.

Mhe. Raya Suleiman Hamad anaiyomba wizara itafute mwalimu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum hasa wale wenye mtindio wa ubongo, ombe lake tumelipokea namuahidi tutaendelea kushirikiana na jumuiya za watu wenye ulemavu kutafuta wataalam hao, hivi sasa yupo mtaalam kutoka Marekani kwa ajili ya viziwi, mtaalam huyo ametafutwa na *CHAVIZA* nae tumempangia vipindi katika madarasa ya elimu mjumuisho yaliyopo chuo cha Kiislam Zanzibar. Pia uamuzi tulioupitisha ni kuwa kuanzia wanafunzi wapya waliojiunga mwaka huu kwa masomo ya Diploma ya dini na kiarabu, Diploma ya sayansi kati na sayansi msingi nao pia watapatiwa mafunzo ya msingi ya elimu mjumuisho kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wenye kuelewa mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu.

Mhe. Moh'd Said Muwakilishi wa jimbo la Mpendae ameeleza kuwa Chuo cha Kiislam cha Zanzibar kimepoteza haiba yake, sababu alizotoa ni kuwa chuo kina walimu wachache na walimu wazuri wengi wameondoshwa, napenda kuelezea hali halisi katika chuo hiki. Wizara imeamua kwa makusudi kukipandisha hadhi chuo na wala sio kukipunguzia hazi, kilichotokea ni kuondolewa walimu wenye taaluma ndogo na kupeleka walimu wenye taaluma na uzoefu mkubwa, walimu wengi waliopangiwa hapo ni wenye shahada ya

udhamili yaani Master degree ambao hapo kabla wakisomesha skuli za sekondari na wenye taaluma mbali mbali zinazosomeshwa chuoni hapo. Hivi sasa chuo kina walimu wenye shahada za udhamili *master degreei 24 na* mmoja ana dhahada ya udhamili ya *PHD* ambae ndio mkuu wa chuo kwa sasa Maalim Siasa ukienda utamkuta pale.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka nizungumzie juu ya habari ya bodi ya mikopo hoja ni kwa nini wanafunzi wa Zanzibar hawapatiwi posho la makaazi University. Mhe. Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti ya bodi ya mikopo imepelekea wanafunzi wanaosoma hapa Zanzibar wasipatiwe mkopo wa posho la makaazi na chakula kama wale ambao wanasoma nje ya Zanzibar. Hiyo imepelekea Chuo cha *Zanzibar University* kuchukua wanafunzi wengi zaidi tofauti na vyuo vyengine. Mhe. Naibu Spika, hali ya fedha itakaporuhusu wanafunzi wanaosoma vyuo vikuu vya Zanzibar watalipwa posho la makazi na chakula.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suali kiwango gani cha kufaulu ili mwanafunzi apate akopo, vigezo vinavyotumika ni mwanafunzi apate mkopo kwa ajili ya kusoma elimu ya juu ni kama ifuatavyo. Mwanafunzi kufaulu kiwango cha 4.5 kwa masomo ya sanaa yaani *art*, masomo ya sayansi ni 2.5 itategemea fani anayoomba. Kwa sasa kipaumbele ni *medicine, engineering, functions, IT na pressure men and supply*.

Kuna kauli kwamba fedha za mikopo ni kidogo lakini huchukuliwa vijana zaidi mara mbili ya wale wanaoweza kuhudumiwa, Ni kweli kuwa fedha za mikopo ni kidogo lakini waombaji waliofaulu mitihani yao vizuri ni wengi ambao wamekubaliwa kujiunga na vyuo vikuu mbali mbali, hada katika fani za uhandisi, utaktari na biashara.

Napenda kulijulisha Baraza hili tukufu ni kwamba pamoja na kwamba tunasema vijana wetu wanafeli wanaanguka kwenye Divisheni for lakini kwa mwaka 2010/2011 waombaji 1300 walijitokeza kuomba kuingia vyuo vikuu na walikuwa na sifa, lakini hatukuwaweza wote ndio maana wakachukuliwa 653.

Kwa mwaka huu wa fedha ambao tunapitisha kasma hii leo tayari tuna waombaji 1,365 kwa ajili ya kusoma elimu ya juu na bajeti yetu ni 4 bilioni ambazo hazikizi haja kwa wanafunzi hao walioko masomoni sasa hivi wanaoendelea, kwa hivyo hawa waombaji wapya tunafikiria tuwasaidie vipi itabidi tukate puwa tuunge wajihi angalau tupate 150 tuwape nafasi ya kuendelea katika masomo ya elimu ya juu. Kwa sababu wote hawa 1,365 wana sifa za kujiunga na Chuo Kikuu tunayo bahati ya kupata kwamba wanafunzi etu

wanaojiunga na Chuo Kikuu ni wengi kama ingelikuwa wanapasi wote sijui hali ingekuwaje hili ndio tatizo ambalo tunalo katika sekta yetu ya elimu.

Kuna hoja ya urejeshaji wa fedha za mikopo taratibu za kurejesha malipo zimeshaanza kwa kuorodhesha wakopaji wote na kiasi cha fedha zalichokopeshwa wahusika, takwimu kwa ajili ya suala hili zimeshakamilika na utekelezaji wake utaanza si muda mrefu. Aidha kanunu za ukopeshaji na urejeshaji wa mikopo zitatayarishwa upya kwa mujibu wa sheria mpya ya bodi, tathmini kwamba fedha hizi zikirejeshwa tunawakopesha wengine hivyo wizara yangu itatoa taaluma kwa wanafunzi na wananchi ya kurudisha fedha zinazokopwa ni kweli tunataka fedha hizi ziwe zinarudi wale wanaomaliza masomo wawe wanatulipa.

Mhe. Naibu Spika, uhaba wa vikalio mnamo mwaka wa fedha 2010/2011 wizara ilifanya ufuatiliaji katika skuli zake za msingi na sekondari na kugundua upungufu wa vikalio, imeonyesha kwamba kuna upungufu wa vikalio 30,000 katika mwaka huu wa fedha wizara imepata madawati jumla ya 2,430 ambapo Unguja ni 1,560 na Pemba 870 na seti za meza na viti 1,254 Unguja 810 na Pemba 804 tuna tuna tamaa ya ahadi tulizopata kutoka katika mashirka mengine mbali mbali kwamba tutapata tena zaidi ya vikalio 4,316 ambayo itafanya kwa sasa hivi tuna vikalio ambavyo tumeshavipata ni kama 8,000.

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imekusudia kuchonga madawati 5,000 kwa wanafunzi 15, 000 wa skuli za msingi, aidha skuli zote mpya za sekondari zitafunguliwa Januari, 12 vitakuwa na vikalio kamili kwa walimu na wanafunzi hizo zitakuwa na vikalio vyake kabisa iko katika *package* moja. Wizara pia imealika miradi yaani *propose* ya kuomba msaada kwa wahisani na washairiki wa maendeleo kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Uchumi na Mipango ya maendeleo katika kutafuta ufadhili huo, ikiwa haya yatafanikiwa yataondosha tatizo la vikalio katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2011 Jumla ya madarasa yaliyoezekwa lakini bado kukamilishwa kazi za sakafu, plasta, rangi, milango, madirisha, umeme na vikalio ni 62 Unguja 27 na Pemba 35. Aidha madarasa ambayo yashafika hatua ya kuezekwa ni 308 Unguja 136 na Pemba 172 katika majengo haya pia zipo ofisi 52 na ghala 26 vyumba vya maabara 5 vyumba vya maktaba 4 na vyumba vya kompyuta 3 na kumbi za mikutano na kufanyia mitihani 3.

Kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 Wizara inataka kukamilisha majengo 200 kati ya hayo yatakamilishwa yale ambayo yameshaezekwa 200 na ambayo hayajaezekwa 138 tuna nia hii kwa mwaka huu kutekeleza hayo, tutakwenda kidogo kidogo lakini nawaomba wananchi wasivunjike moyo kwa sababu bado

tunataka kupunguza idadi ya wanafunzi katika madarasa wasikaliane kama wanavyokaliana sasa hivi waendelee kama wanaweza kujenga madarasa mapya wajenge na sisi kama wizara tutachukua juhudi zza kuyaezeka, ili tupunguze na tutoe elimu.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mwaka huu ni kuimarisha na kutoa elimu iliyo bora ndio nia yetu hasa kusema kweli, halafu kuna uhaba wa hifadhi ya maabara. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa vya maabara ilinunua vifaa vya maabara kwa ajili ya skuli 17 kwa kuanzia kupitia mradi wa Benki ya Dunia na kugaiwa kama ifuatavyo.

Unguja Skuli ya Sekondari ya Lumumba, Benbella, Haile Selassie, Chuo cha Kiislam Mazizini, Kituo cha Taifa cha Walimu *NTCR*, Kituo cha Ualimu Bububu, kituo cha Ualimu Kiembesamaki, Kituo cha Ualimu Kitogani, Kituo cha Ualimu Mkwajuni, Kituo cha Ualimu Dunga. Pemba ni Chuo cha Kiislam Micheweni, Chuo cha Ualimu Benjamin Wiliam Mkapa, Skuli ya Sekondari Konde, Kituo cha Ualimu Mizingani, Kituo cha Walimu Michakaeni, Kituo cha Ualimu Mitiulaya, Kituo cha Ualimu Wingwi.

Aidha hivi sasa Wizara yangu inafanya tathmini ya ununuzi wa vifaa vya maabara kwa skuli mpya 16 nilizozitaja za sekondari ambazo ni Matemwe, Muwanda, Chaani, Dole, Uzini, Paje, Mtule, Tunguu na Dimani kwa Unguja. Wingwi, Shamiani, Kiwani, Mauwani, Ngwachani, Mauani, Pandani, Konde, Chwaka, Tumbe na Utaani kwa Pemba. Pia chuo kipya cha ualimu kinachojenga Mchanga Mdogo Pemba kimo katika awamu hii.

Mwaka 2012/2013 Wizara yangu imekusudia kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya skuli mpya tatu za Unguja yaani kwa Mtipura, Kiembe Samaki na Mpendae, pia skuli sita zimefanyiwa ukarabati mkubwa yaani za Tumekuja, Hamamni na Forodhani kwa Unguja na Utaani, *Fidel Casto*, na Uweleni kwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika safari hii nataka kusema kwamba tutakuwa tumepata bahati tukipata hivi vifaa vya skuli 16 kwa sababu ukitizama hizi skuli mara nyingi zimekaa karibu na skuli za sekondari zile za asili ambazo tulizianzisha pale, kwa hivyo ni rahisi kwa wanaosoma Chaani kupata mafuzo ya *practical* kwa skuli mpya iliyopo pale pale Chaani, kwa wanaosoma Kombeni ni rahisi kupata *pretical* zao pale pale katika skuli mpya ya Kombeni, na skuli nyengine hata vile Utaani vile vile pamoja na kwamba Utaani hii itafanyiwa marekebisho na itapata vifaa vyake lakini pale vifaa itakuwa tayari na watawaza kufanya *pretical* zao pale. Itakuwa tumelipunguza sana hili tatizo Mhe. Naibu Spika.

Kuna hoja kwamba kampuni zinazopewa zana za ununuzi wa vifaa vya ununuzi vifaa vinakuwa havina hadhi.

Mhe. Naibu Spika, manunuzi yote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanafuata muongozo wa Serikali wa mwaka 2005 miongozo ya mradi husika kama mradi unafadhiliwa, bodi ya dhabuni ya Wizara yenye wajumbe 15 inapitia taratibu zote za manunuzi, kitengo cha ununuzi na ugavi ndicho kinachoshughulikia utayarishaji, utangazaji na uuzaji wa dhabuni hizo, zabuni zote zinafunguliwa mbele ya wajumbe wa bodi ambapo pia wawakilishi wa zabuni husika wanakuwepo.

Bodi ya zabuni inateua kamati ya tathmini ambayo mwenyekiti wake huwa ni mjumbe wa bodi, ripoti ya tathmini inawasilishwa na kujadiliwa na bodi na kukubaliwa au kukataliwa bodi ikisharidhika inatoa mapendekezo ya uteuzi wa washindi wa wadhabuni husika na kupelekwa ka katibu Mkuu kama ni mradi wa wafadhili basi hupelekwa kwa wafadhili ili kupata no, *objection* ndipo baada ya hapo mdhabuni husika anasaini mkataba na wizara. Kwa utaratibu huu sio rahisi kwa kiongozi mmoja wa Wizara kuwa na mauzo ya upendeleo kwa mdhabuni mmoja.

Tokea mwaka 2007 ilipoundwa bodi ya Wizara kumefanyika manunuzi mbali mbali ya kuwemo ya ujenzi na vifaa mbali mbali kama vitabu, vifaa vya maabara, magari, vifaa vya kompyuta n.k Kutokana na wizara yetu kuaminika na makandarasi washauri wamekuwa wakijitokeza kwa wingi zabuni zote zilikuwa hazikosi kampuni nane na kuwasilisha zabuni zao, tokea mwaka 2007 ilipoanzishwa bodi ya Wizara hatujapata malalamiko yoyote kutoka kwa wazabuni. Naomba kuchukua nafasi hii kwa kuwatoa wasi wasi waheshimiwa wawakilishi kwamba utaratibu wa zabuni kwa wizara ya elimu unakwenda vizuri na kama kuna lalamiko yamejitokeza basi watujulishe na sisi tutayafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa skuli tatu za ghorofa Mjini Magharibi chini ya mradi wa elimu ya lazima unaofadhiliwa na serikali ya Benki ya Dunia unakusudia kujenga skuli tatu za ghorofa za sekondari katikamaeneo yafuatayo, Hapa naomba kumuomba Mhe. Moh'd Said asiwe na wasi wasi na skuli yake ya Mpendae skuli hizi ni tatu Kwamtipura, Kiembesamaki na Mpendae.

Hizi tumezizungumza sana kwenye ilani ya chama cha mapinduzi kwamba tutazijenga, kwa hivyo ujenzi wa skuli katika maeneo haya yanatokana na kuwa ni maeneo ambayo yana watu wengi na hakuna skuli kubwa kama alivyosema Mhe. Moh'd Said. Wizara ilitarajia kutiliana sahihi mkataba na makandarasi

tarehe 31/8/2011 na ujenzi unatarajiwa rasmi kuanza tarehe 28/9/2011 kwa skuli ya Mpendae na Skuli za Kiembesamaki na Kwamtipura.

Wizara inatarajia kutiliana saini mikataba ya ujenzi tarehe 31/8/2011 na ujenzi kuanza tarehe 28/9/2011 muda ujenzi wa skuli ya Kwamtipura na Kiembesamaki ni wiki sitini na Mpendae ni wiki arubaini na tano tu, hiyo ndio kazi ambayo itafanyika hivi karibuni. Hivi sasa wizara iko katika hatua ya tathmini na zabuni za ujenzi hizo zimeshafunguliwa.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imefanya mabadiliko ya muundo wa mfumo wa ukaguzi kwa mujibu wa sera mpya ya elimu ya mwaka 2006 na moja wapo ya mabadiliko ni kurudisha ukaguzi wa ngazi ya wilaya ili kuweza kuwafikia skuli zote za serikali na binafsi zilizosajiliwa, ombi hili Mhe. Panya Ali Suleiman limezingatiwa, hivyo tuna matumaini ya kuwa mabadiliko haya yataweza kunyanyua kiwango cha elimu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka kuzungumzia juu ya mamlaka ya mafunzo ya amali, mamlaka ya mafunzo ya amali wajumbe walioigusia hii ni Mhe. Rashid Seif, Mhe. Abdalla Juma, Mhe. Salehe Nassor, Mhe. Ashura Sharif na Moh'd Said je vyo vya amali ya ufundi vinafanya kazi zake kama inavyosatahiki ndio suala hilo, jibu ndio na wako vijana wengi walioweza kupata ajira baada ya kumaliza mafunzo yao katika vyuo hivyo na wengine kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwajulisha wajumbe kwamba katika mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya amali ni mengi, ikiwemo masuala ya ofisi, pamoja na *house keeping* mambo ya mahoteli na mengineyo, hivi juzi sisi huwa tunawapeleka wanafunzi wetu kufanya *practical* katika mahoteli, basi tumepeleka wanafunzi katika mahoteli hawakurudi hata mmoja wameajiriwa huko huko wameshapata kazi moja kwa moja. Na hili ndio tulikuwa tunakusudia kwamba wawe wanapata ajira kupitia katika njia hiyo.

Mafunzo ya Amali kuwa yapewe vipaumbele na ulingane na ule wa elimu za msingi, kuendesha skuli za amali kuna gharama kubwa sana pamoja na umuhimu mkubwa wa mafunzo ya amali kwa maendeleo ya nchi na upatikanaji wa ajira, uwezekano wa kuwa na vyuo vya amali kama skuli ni mdogo ikiwa vituo vya amali vya kila mkoa vitaimarishwa ipasavyo kwa kuongeza vifaa na fani zinazohitajika katika soko la ajira basi tutapiga hatua kubwa sana.

Hata hivyo tunashajihisha watu binafsi wafungue vituo vya amali hasa katika maeneo ya vijijini, pia tunatarajia kufanya hivi sasa katika mitaala mipya ya

elimu ya msingi ni kuanza kufundisha mafunzo ya amali ya awali, kabla ya kujiunga rasmi na mafunzo hayo baada ya kumaliza elimu ya lazima.

Mafunzo ya amali yapo katika maeneo mengine juzi juzi nilikuwa nazungumza na Mhe. Said Ali Mbarouk waziri wa Mifugo na Uvuvi nikamwambia bwana kama utakwenda Vitongoji tayari utakuta mabanda kwa ajili ya mifugo yapo yashajengwa, lakini hatujayatumia kwa hivyo kama Mhe. Said Ali Mbarouk atashirikiana na wizara yangu katika kuhakikisha hili linafanikiwa na watu wakapata mafunzo ya mifugo pale pale itatusaidia sana.

Hali kadhalika ukienda Mkokotoni vile vile maeneo kwa ajili ya mifugo yapo yameshajengwa, isipokuwa kwahala kwenyewe ni mbali huwezi kumchukua ng'ombe ukenda kumuweka kule bila ya kuwa na ulinzi asubuhi humkuti, pengine utakuta ngozi pale na miguu na kichwa ndio tutakavyokuta pale. Hii ndio hali halisi nimekusudia kufundisha mengi na hata ya uvuvi nitafundisha pale, pale watu wanafundishwa mambo ya *electronic, uchoraji* hata watu wanaochora piko zinazoingia pale wanachora mambo kama hayo.

Kwa hivyo watoto wetu wanapata ujuzi pale wanapata kushona, kuna kompyuta, kuna ufundi bomba, kuna fundi umeme wote wanafundishwa kazi hizi wakitoka pale wajipatie ajira. Wengine wameshafungua *work shop* zao za mafriji unajua mafriji sasa hivi Unguja ni mengi sana kwa hivyo vijana wale wamefapata kazi zao sasa hivi imepunguza tatizo la ajira na hilo ndio lengo la kuanzisha vituo vya mafunzo ya amali.

Halafu kuna hatua iliyofikiwa katika kuwalipa fidia mazao wananchi wa eneo kilipojengwa kituo cha mafunzo ya amali Vitongoji. Tunasubiri mamlaka husika kufanya tathmini ya mazao watuletee kwa vile ya mwanzo ilikuwa hailingani na mazao yaliyokuwepo.

Hata hivyo wananchi hao wanavuna mazao yaliyopo hatujawakata kuvuna tunawaruhusu wavune, pale Vitongoji wa mivinja wavune wenyewe hatujawakata kufanya hivyo waendelee kuvuna lakini tathmini ya kwanza ilikuwa ya ajabu ikanikumbusha ile tathmini iliyojengwa msikiti mahala fulani, pale kila nyumba haikupungua milioni 40 aliyopelekewa mjenzi.

Yule mfadhili akasema nyie mna uwezo mkubwasana bwana mnaweza kujenga nyumba za milioni 40 jengeni wenyewe msikiti, sasa hapo tena ndio ikabidi tathmini ikapunguzwa na wanaohusika na baadae ndio yule mjenzi akakubali.

Sasa nachelea kwamba na hii tathmini ya Vitongoji ilikuwa kubwa sana kiasi ambacho sasa hivi mamlaka ile inafanya tena tathmini sasa hivi, naahidi

kwamba tukiipata tutawalipa. Jee Wizara inayo habari ya kuungua kabisa vifaa vya dakhalia kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni, wizara inayo habari kamili ya tokeo hilo la kusikitisha hata hivyo hakuna chumba kilichoteketea kabisa kutokana na moto huo, vilivyoteketea ni baadhi ya vifaa vya wanafunzi tena katika chumba kimoja tu na kuharibika katika sehemu ya jengo kutokana na moshi. Baada ya uchunguzi wa kina kufanyika wanafunzi wawili walihusika na tukio hilo.

Hatua ya mwanzo iliyochukuliwa ilikuwa ni kuwafukuza kabisa kituoni na dakhalia lakini baada ya wazee wao kufika vituoni na kuomba vijana wao wasamehewe na vijana wenyewe kuomba radhi, walirejeshwa kituoni na dakhalia na kutakiwa walipe sehemu ya hasara waliyosababisha yakiwemo magodoro na wao pamoja na wazee wao wamekubali kufanya hivyo. Unajua watoto walichokozana wenyewe kwa wenyewe hawa .

Matunzo ya Amali katika Zanzibar yanatolewa kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Amali na Mafunzo ya mwaka 2005 Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 8 ya mwaka 2006 kama ilivyorekebishwa sheria Nam. 11 mwaka 2007.

Vyuo vyote vinavyotoa mafunzo ya amali hapa Zanzibar lazima visajiliwe kwa mujibu wa sheria iliyotajwa hapo juu. Na kwa mujibu wa kanuni za usajili wa vituo vya mafunzo ya amali zilizotayarishwa kutokana na sheria hiyo. Vituo vingi vimeshachukua fomu za maombi na kutaka usajili wao. Lakini hadi hivi sasa ni vituo vinane tu ndivyo vilivyokamilisha ujazaji wa fomu hizo na kuzirejesha mamlaka. Mamlaka iko katika mayarisho ya kwenda kuvikagua rasmi vyuo hivyo ili kuona maelezo yao katika fomu yanakubaliana hali halisi na hatimaye kusajili rasmi. Ukaguzi utafanywa na Kamati za ushauri za mamlaka zinazoundwa na wataalamu kutoka sekta mbali mbali za binafsi wakiongozwa na msajili mkuu wa mamlaka.

Vyuo vyote vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya Shahara na kuendelea tunavishauri moja kwa moja kuomba usajili kwa NEKTA kwani mamlaka yetu haina mamlaka ya kusajili katika viwango hivyo vya elimu.

Kuna taasisi ya elimu Zanzibar, waliochangia ni Mhe. Rashid Seif ambao wasaidizi wa maabara waajiriwe na wafundishwe. Mhe. Spika, ni kweli kuna upungufu wa wasaidizi wa maabara, Wizara imeliona tatizo hilo katika bajeti hii itaajiri wasaidizi wa maabara na itaandaa mafunzo maalum kwa ajili ya wasaidizi wa maabara. Hii mtusaidie katika kupiga kempeni. Walimu wengu sijui kwa nini wanakuwa hawapendelei sana kufanywa kama wasaidizi wa maabara. Labda itabidi kutizame kiwango cha mshahara, huwenda pengine

tukafanikiwa katika hali hiyo. Mara nyingi walimu huwa hataki, kufanya kazi *labor assistance*.

Mhe. Rashid Seif, Mhe. Panya Ali, Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Salma Abdallah, Mhe. Salma Muhammed, wameuliza katika Skuli za Sekondari hakuna uwiyano wa kuwepo vifaa vya maabara. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba zipo baadhi ya skuli za secondary hazina vifaa vya maabara vya kutosha na nyengine hazina hata maabara. Nyengine zina maabara na upungufu wa vifaa. Hata hivyo wizara yangu ilianza kuchukua hatua hivi karibuni, imesambaza vifaa kama nilivyokwisha kusema pale mwanzo.

Mhe. Abdalla Juma aliuliza Wizara ina mpango gani ili kuhakikisha mtoto akianza darasa la kwanza awe ameshapitia maandalizi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba sera ya elimu ya mwaka 2006 imeelekeza watoto wote wakianza darasa la kwanza wawe wamepitia skuli za maandalizi. Utekelezaji wa sera hii unakwenda hatua kwa hatua. Hivi sasa wizara imetoa maelekezo kwa skuli za msingi kufanya utaratibu wa kuanzisha madara ya maandalizi. Baadhi ya skuli wameshaanza kujenga madarasa ya maandalizi.

Mhe. Abdalla Mohammed wa Mkoani, kwa nini wanafunzi hawaanzi *specialization* kuanzia kidatu cha kwanza katika mkondo wa sayansi au sanaa ili kuwapunguzi mzigo. Ni kweli kwamba utaratibu uliopo hivi sasa wanafunzi wa kidatu cha kwanza na cha pili wanasoma masomo yote yaani *specialization* ya masomo ya sayansi au sanaa inaanza kitadu cha tatu. Hii ni kwa sababu kuna mambo ya msingi ambayo wanatakiwa wanafunzi wayaelewe kabla ya *specialization*. Hata hivyo wizara inauchukua ushauri huo wa Muheshimiwa na ufatanyiwa kazi baasa ya kushauriana na wataalamu.

Mhe. Ismail Jussa ameuliza kwa nini vitabu vilivyoandikwa na Wazanzibari havipewi nafasi kutumika katika skuli. Ni kweli kwamba waandishi wa Zanzibar wameandika vitabu katika viwango mbali mbali ambavyo havijaingizwa katika mtaala kwa matumizi rasmi katika skuli za Zanzibar. Hata hivyo taasisi ya elimu ya Zanzibar tuyari imeshawasiliana na Baraza la Kiswahili la Zanzibar tangu tarehe 5/5/2011 ili kupata nakala za vitabu hivyo ili ifanyiwe tathmini na kuthibitishwa kabla ya matumizi rasmi kutumika. Mhe. Spika, vitabu ni vingi karibu vitabu vyote vilivyokwisha kuandikwa na Wazanzibari ni 90. Kwa hivyo hili nalo tunalifanyia kazi Ishallah.

Mhe. Mwanaidi Haji, anasema vipindi vya masomo vya Kiingereza viongezwe. Nafikiri nimeshakujibu ni kweli kuwa kwa mujibu wa mtaalamu mpya wa elimu ya msingi masomo ya darasa la kwanza ni kama ifuatavyo. Kuna suala

hapa nimeuliwa kwa nini darasa la kwanza wanasomeshwa masomo manane nayo ni Kiswahili, kiarabu, *English*, dini, hisabati, sayansi jamii, sayansi ya michezo. Masomo haya yalipendekezwa na watafiti wakati wa ukusanyaji wa maoni ya idadi na aina ya masomo yanayofaa kufundishwa wanafunzi wa darasa la kwanza. Utafiti ulifanywa na ndiyo yakapendekezwa masomo yale yasomeshwe. Hata hivyo ushauri wa Mhe. Mwanaidi Haji tunauchukuwa na utazingatiwa wakati wa kufanya mapitio ya mtaala. Hawa kwa kuwa yeye ni mwalimu analifahamu vizuri suala hili. Kwa hivyo Mheshimiwa tunalipokea hili suala ishallah.

Mhe. Fatma Mbarouk anauliza vipi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewawezesha walimu kuvitumia vitabu vilivyoandikwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani. Mhe. Spika, mafunzo kwa walimu juu ya matumizi ya vitabu vya *Biology, chemistry, physics* na *mathematics* kupitia mradi wa *teaching learning material program* uliofadhiliwa na Shirika la Misaada la *USLA* alitolewa mwaka wa 2007 kwa kupitia vyuo vya walimu.

Mhe. Said Ali anasema mitaala yetu iingize masuala yenye maslahi katika nchi yetu kama vile elimu ya mazingira na madawa ya kulevya. Mitaala ilenge kwenye uchumi wa nchi, yasomeshwe masomo ya kilimo, utalii na uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, mtaala mpya wa elimu ya msingi umeingiza masuala ya mazingira na madawa ya kulevya katika masomo ya sayansi, darasa la kwanza mpaka darasa la sita. Maeneo mengine kama vile mazingira na stadi za maisha masuala mtambuka yamefanyiwa uwiyano na sio masomo kamili.

Ni kweli ni muhimu mtaala unaofundishwa katika skuli zetu ulenge katika kuinua uchumi wa nchi na kusomesha masomo ya kilimo, utalii na uvuvi katika maskuli yetu. Ushauri wa Mhe. Said Ali Mbarouk, nauchukua kwa kushirikiana na wataalamu wangu na tutaufanyia kazi kama alivyoueleza hapa.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Upiamaji na Tathmini. Hii ndiyo ile Mheshimiwa mmoja aliniuliza siku moja mbona hakuna bodi ya mitihani hapa. Kwetu sisi tunaita Idara ya Upimaji na Tathmini katika Elimu, Hatuiti bodi ya mitihani kama ile ya Jamhuri ya Muungano. Katika eneo hili amelizungumza

Mhe. Rashid Seif, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Abdalla Juma, Mhe. Ashura Sharifu Mhe. Fatma Said, Mhe. Fatma Mbarouk, Mhe. Salim Abdalla Hamad

Mhe. Naibu Spika, ni kweli matokeo ya mtihani wa darasa la saba na kidatu cha pili hayachapishwi kama yale ya darasa la kumi na mbili. Malengo ya mitihani ya darasa la saba na kidatu cha pili ni tofauti nay ale ya kidatu cha

nne. Lengo letu ni kuteuwa vijana kuendelea na masomo ya kidatu cha kwanza na kidatu cha tatu. Si busara kuingia hasara za kuchapisha matokeo ya darasa la saba na kidatu cha pili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu matokeo ya kidatu cha nne, tunakiri kuwa mwaka huu si mazuri sana. Lakini tumepata wanafunzi wa kutosha kuendelea na masomo ya vidatu vya juu yaani *division III* na *division IV*, vile vile na wao wameweza kuendelea na masomo mengine. Kuna vijana wengine wana division IV lakini *combination* yao inawaruhusu kuingia katika Chuo Kikuu, kwa hivyo wanaingia, katika vyuo vikuu.

Halafu malipo ya wasimamizi wa mitihani ni Shs. 10,000/- mbali na hilo wasimamizi wanapatiwa chakula cha mchana na nauli ya kwenda na kurudi katika vituo vya mitihani. Tunakiri kuwa hatujalipa fedha kwa ajili ya wasimamizi wa mitihani hiyo mwaka huu. Tunakiri kabisa, lakini tutawalipa, wala hatukiuki haki za binaadamu.

Fomu za mitihani ya kidatu cha nne na kidatu cha sita zinazotumika Zanzibar na Bara ni moja na zinaletwa mapema kama zinavyoletwa mihutasari ya masomo. Suala la mitihani ya kidatu cha nne na kidatu cha sita na ile ya stashahada ya diploma ya uwalimu ni suala la muungano. Hata Baraza la Mitihani ni la muungano. Wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihadi ya darasa la saba, kitabu cha pili, kidatu cha nne, kidatu cha sita wanazawadiwa katika Tamasha la Elimu Bila ya Malipo kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika suala moja gumu kidogo, nazungumzia juu ya uchanganuzi wa fedha za mishahara kwa Wizara ya Elimu na walimu. Kwa mujibu wa bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha upo mchanganuo kama ufuatao.

Mishahara kwa walimu tu tumeiweka pamoja ni bilioni 25,472,392,410 ambayo ni sawa na asilimia 89. Hoja ya fedha zilizotumika kuendesha skuli kwa wanafunzi ni kwamba hadi sasa Wizara yangu inalenga kutumia jumla ya shilingi bilioni 25 kwa ajili ya uendeshaji wa skuli za sekondari na msingi kwa Unguja na Pemba. Matumizi haya yanajumuisha mashahara ya walimu na matumizi ya kazi za kawaida.

Hapo utaona kwamba zinabakia milioni mia tatu na kumi na nne, laki mbili na kumi na sita (314,216) kwa ajili ya kazi nyenginezo ambazo mishahara tutakuwa tumeshaitoa ile bilioni 25. Kufuatana na bajeti yetu gharama halisi kwa mwanafunzi wa mwaka mmoja ni sawa na shilingi sabini na mbili elfu, mia tisa na ishirini na tisa (72,929). Hii ndio hali halisi ya matumizi yetu.

Mhe. Asaa aliandika kwa maandishi lakini amechelewe kidogo amenipa sasa hivi nakuja hapa. Ana michango mizuri angeliitoa ingesaidia sana katika kumbukumbu za wizara yangu. Kwanza nasema kuna mafundi ambayo kuwa wanapewa kazi ya utarishi. Namuahiri kuwa nitalifanyia kazi. Amezungumzia suala la upungufu wa thamani na kusema kwa nini pesa zinawekwa katika safari za nje na safari za ndani badala ya kupelekwa kwenye thamani. Kawaida tunakuwa tunamaliza mwaka pesa hizi kama hazikutumika huwa tunazipeleka huko huko kenye thamani. Ndio maana tukaweza kununua hizo thamani nyingi ambazo nimekwisha kuzitaja pale mwanzo. Ni pesa zile ambazo zimebakia kwenye safari za nje na safari za ndani.

Vijana wanaosoma nje hupewa dola 100 tu kwa kujikimu, anasema hamuonei huruma kwa dola 100 kwamba ndio ajikimu kwa muda wote kwa mwaka mzima. Nitalifuatilia na kuliona ukweli wake kwa ghafla siwezi kulijibu. Lakini nimelipata mwanzo kwenye michango ningeweza kulifanyia kazi vizuri sana na nikajua kwamba hali halisi iko hivyo.

Halafu amesema hutokea wakati mtahiniwa huwa hakubaliani na matokeo yaliyotangazwa na hivyo huwa anapata nafasi ya kukata rufaa. Anapokata rufaa anakuta kumbe amefanikiwa, tofauti na yale matangazo yalivyotoka katika kufanya mitihani yake. Hii nakubaliana nayo ni kweli tatizo hili lipo na ametoa maelekezo mengine ambayo haya nitazungumza mimi na yeye ili tuyafanyie kazi pamoja. Sitakuwa na haja ya kuyataja hapa.

Mhe. Naibu Spika, nimejitahidi sana inaweza ikawa kuna hoja ya hapa na pale nimeiwacha lakini ndio binaadamu. Hakuna binaadamu mkamilifu. Kila binaadamu ana upungufu wake kwa hivyo nakubali kama kuna upungufu itakuwa nimeufanya katika kujibu masuala haya. Natanguliza kusema nisamehewe bajeti yetu ipite ili nifanye kazi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, lazima nichunge nidhamu hasa wakati huu wa kupitisha vifungu. (Vicheko).

Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU - 23 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	15,000,000
Kifungu 0401		

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Napenda kwanza nitoe shukurani sana kwa Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri kwa majibu yao mazuri na ya ufasaha. Lakini wakati nilipokuwa nikichangia kuhusiana na upungufu mkubwa wa vikali maskulini. Nilisema kwamba sera ya Wizara ya Elimu iliyopitishwa mwaka 2006 hapa ilitaja juu ya kila kijana wa Zanzibar kupata elimu na usawa katika elimu.

Katika ukurasa wa kifungu cha 4(223) Cha Sera ya Elimu kinazungumza kwamba kuondoa tofauti za Kimaeneo. Naweza kukisema kwa kiingereza ili tuweza kukielewa kwa sababu ndio alivyotoa kwa Kiingereza. *School maping shall be enforced as a strategy to adverse the disparities between within districts in provide and support planning environment to ensure learning takes place.*

Kwa kuwa wizara kazi yake ni kufuata sera, majibu haya ya upungufu mkubwa wa zana za kukalia yamekuwa yakiripitiwa mwaka kwa mwaka, miye binafsi zaidi ya miaka sita sasa hivi. Mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri sasa aje atupe hasa tarehe kamili ambayo kila mwanafunzi wa Zanzibar atakaa juu ya kiti, ili ule utafauti baina ya huyu anakaa chini na huyu anakaa juu ya kiti hali hiyo iwe imeondoka. Kwa sababu sera siku zote wakati wa utekelezaji wake unamuda wake wa utekelezaji.

Kwa sababu hakuna taarifa kamili ya iliyotolewa kwamba mwaka fulani tunategemea kwamba tatizo lile litaondoka. Kila siku tutakuwa tunaliuliza tatizo hili na wakati wale wanafunzi wengine wanakaa juu ya viti na wengine hawakai juu ya viti. Hii inakuwa ni tofauti katika utekelezaji wa sera yake. Katika maelezo yake yote Mhe. Waziri alikuwa anagusia kuongezwa tu kwa vikalio lakini hajagusia ni lini hili tatizo linatarajiwa kumalizwa. Namuomba Mhe. Waziri atupe muelekeo wa lini kwamba litamalizwa ili kila mwanafunzi aweze kukaa juu ya kiti. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Rashid Seif kwa kuweka mkazo kwenye suala la vikalio. Kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, lengo letu hasa ni kwamba kila mwanafunzi asome kwa kukaa kwenye kiti au deski, lakini ilimradi awe anasoma kwa kukaa na kuandika katika kikalio, hilo ndio lengo letu.

Ni kweli kama alivyotaka yeye sikutoa wakati maalum kwa sababu tatizo lenyewe ni kubwa. Ninezungumzia 30,000 lakini kwa sababu watoto wanaandikishwa na madarasa yanajengwa, kuna uwezekano mkubwa huo uwezekano wa 30,000 kitakaongezeka ukakikuta pengine mwakani kishabadilika kishakuwa sio 30,000 tena, pamoja na jitihada yetu ya kuziba pengo hilo. Lakini niya ya wizara yangu ni kuliondoa tatizo hilo na serikali imetuelekeza kwamba sasa matatizo ya vikalio tuanzishe mradi rasmi, tutengeneze *right up* za mradi rasmi wa vikalio na tuiyuze kwa wafadhili mbali mbali. Ilimradi hizi jitihada zetu za ndani za wizara na miradi hiyo tukishakuiyuza kule tukipata wadhili wakitusaidia mambo yatakuwa mazuri na tutaliondoa kabisa tatizo hili.

Lakini hivi sasa kwa upande wetu kama nivyokwisha kusema tutachonga vikalio safari hii ili kupunguza hicho kiwango. Nataka kumwambia hizi *right up* nyengine tumeshaanza kuziuza. Kwa bahati katika ziara ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alipokwenda Oman na Mhe. Harouna Ali Suleiman aliposhirikiana na Makamo wa Rais na Waziri wa Nchi Fedha walizungumzia masuala haya haya. Oman wameonesha dalili ya kutusaidia katika tatizo hili. Tunamatumaini kwamba pengine wakitekeleza, hatuwezi tukawawekea muda. Sisi kwa pesa zetu za kuweka kwamba tutaweza kwenda kidogo kidogo sio tunawangojea wao. Lakini wakiweza kututekelezea basi bila shaka tatizo hili Ishallah litaondoka kwa muda mfupi.

Oman wakikubali tu kwa sababu walichotwambia hii ni pesa kidogo ni pinati tu hii, tutakutekelezeeni mara moja litaondoka. Kwa hivyo pengine isimalizike hata hiyo miaka mitano ambayo tupo katika serikali hii ikawa suala hilo limemalizika kabisa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mheshimiwa mimi nakubaliana sana na mawazo yake, lakini tulitoa rai mbali mbali hapa. Sikumoja katika kuuliza swali na kupata jibu tulitoa rai kwamba tunazo sherehe zetu sisi za miaka 50 ya Mapinduzi zinakuja mwaka 2014, kwa sababu hili suala ni la kitaifa kila mwanafunzi ni mwanafunzi wa taifa. Kwani waziri ana wasi wasi gani wa kuweka lengo la mwaka 2014 kwamba Sherehe za Mapinduzi tuzisherehekee wakati kila mwanafunzi anakaa juu ya kiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, rai yake ni nzuri na tuliisikia. Lakini rai ambayo utekelezaji wake izungumzwe na serikali kwa pamoja sio Wizara ya Elimu peke yake ndio iseme hivyo. Sisi rai tuliipokea tangu siku aliyoizungumza tumeichukua. Tufike mahali tuone kwamba hapa ndio mwisho wanafunzi wetu kukaa chini badala yake wakae kwenye madawati hiyo ndio shabaha yetu. Mimi kama Waziri wa Elimu kuchukua tu dhamana tu moja kwa moja kwamba 2014 ndio itakuwa tayari tumeshakaa bila ya kulizungumza pamoja na serikali na tukakubaliana hivyo basi itakuwa kidogo sio rahisi.

Hata hivyo kwa upande wa serikali hili suala wameliona na safari hii mkazo tulioambiwa ni vikalio. Ndivyo serikali ilivyotwambia na ndivyo Baraza la Mapinduzi lilivyotwambia. Kwa hivyo tutakachokipata chochote safari hii kinakwenda kwenye vikalio.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali imesikia na Waziri kakubali tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kunipa fursa hii. Mhe. Waziri nilipokuwa natoa hoja yangu kuhusu vifaa vile vilivyopelekwa Nungwi kanijibu lakini majibu yake alivyonijibu ilikuwa yale majili aliyonijibu kwanza bila ya kuongeza mengine nilikuwa nimesharidhika.

Lakini alipoongeza tena ya kuwa muwakilishi anapotaka kutoa vifaa vyovyote vile aende wizarani, sasa tena ndipo aliponiacha tena hoi ikabidi nisimame. Kwa sababu mimi ninavyofahamu Mwakilishi anapochaguliwa katika jimbo lolote lile, akishachaguliwa kuwa Mwakilishi anakuwa ni mwakilishi wa kuwakilisha jimbo lile kwa vyoma vyote, ikiwa ni CCM ikiwa ni CHADEMA, ikiwa ni *CUF* na chama chengine chochote cha siasa kilichopo, huwa mwakilishi ndio yeye anayewakilisha.

Sasa Mhe. Waziri anasema mwakilishi ikiwa anataka kutoa msaada wowote ule anaoupata katika shule yake basi ikiwa mpaka utoe taarifa Wizarani. Ikiwa nataka kutoa vifaa vya afya nimpe babu Juma Duni katika wizara yake taarifa. Nikitaka kusaidia uvuvi nimpe taarifa Mhe. Said Ali Mbarouk. Ina maana mwakilishi hana uwezo wa kusaidia jimboni kwake kitu chochote kama hajatoa taarifa wizarani.

Naona anavyonambia hivyo naona kama anaturudisha nyuma, kama kitu chochote nije Wizarani ndio nitoe kama naona anatuongezea msaada. Nilivyomuomba mimi kwamba kipindi hiki cha Serikali ya Ummoja wa Kitaifa tunahitaji maendeleo, hatutaki tena mtu aturudishe nyuma, kama aidha

muwakilishi yupo chama hiki anakwenda kusaidia kitu, mwalimu mkuu akakosa kukipokea kwa ajili ya kuwa huyu anatoka chama fulani. Kamwambia kwamba kipindi hiki sio kipindi tena cha kurudishana nyuma tunakotoka. Kwa hiyo huyu mtu nataka umuonye. Yeye alikuwa atwambie tu kwamba wizara yake imechukua suala fulani kumuonye huyu mtu kama hatorudia tena. Lakini anaposema kama ukitaka kutoa kitu ni lazima tupige ripoti wizarani. Je, ina maana sisi hatuna mamlaka ya kutoa kitu chochote jimboni kwetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hili suala nimelizungumza hasa kwa faida ya Waheshimiwa Wawakilishi na hasa wawakilishi wenye majimbo. Kwa sababu utakapotupa taarifa tunakutana sisi, miye, naibu waziri, Katibu Mkuu, utakapotupa taarifa sisi tunaandaa hiyo shughuli yenyewe na Mwalimu Mkuu anakuwa anapata habari rasmi kutoka kwenye Wizara yake hapa kuna shughuli fulani itafanyika hapa na Mheshimiwa fulani atakuja kutoa msaada fulani.

Tunamfanyia *promotion* tunamsaidia yeye hivyo, tunamshindikiza katika uchindi wa uchaguzi ujao kenye jimbo lake. Tutaitangaza vizuri kama tulivyoitangaza ya Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwamba leo yupo Fujoni kesho yupo Kitope, kesho yupo Mgambo, shughuli imekuwa nzuri. Sasa Balozi anajulikana, Balozi bwana kwa madawati ni moto wa kuotea mbali, usifanye mchezo. Kweshamiliza kweli skuli zake.

Sisi tunataka misaada ya kompyuta tunataka, misaasa ya vitabu tunataka. Lakini usiende pale kimya kimya, tushirikiane na wizara. Sasa unaweza ukanambia miye, unaweza ukamwambia Naibu Waziri, unaweza ukamwambia Katibu Mkuu, tukatengeneza ile *publicity* nzuri kwa ajili ya kukushindikiza kwenye uchaguzi ujao kwenye jimbo lako. Kwa sababu unafanya mambo mazuri ambayo ndiyo inavyotaka katika ujenzi wa nchi, kwamba wewe mwakilishi una maana kwa wananchi wako na unawashughulikia. Ndio maana yake. Nimetoa kwa nia nzuri kabisa. Ndio maana nikalizungumza suala hilo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakubaliana na yeye kwamba atakuwa anatusaidia siye, lakini kuna misaada mengine wakati sijapita wizarani akisema hivyo, kuna misaada mengine unajua tunaambiwa sadaka ukitoa kwa mkono huu huu usijue. Sasa saa nyengine mimi naweza nikatoa kitu ni kitu kidogo. Sasa kama itakuwa wakitoa kauli kama hiyo walimu watakuwa hawapokei mpaka wapate barua kutoka Wizarani, hilo ndilo ninaloliogopa miye. Kauli hiyo ni nzuri na ni kweli anatusaidia siye, lakini kuna vifaa vyengine unaweza ukawa unataka kutoa kifaa kidogo tu kusaidia, lakini hata hicho kifaa kidogo ninachotaka kutoa mpaka nije wizarani alipo yeye. Naomba aliweke sawa kwa faida yangu miye na wenzangu wengine.

Mhe. Mwenyekiti: Ushauri wako umezingatiwa. Je, tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: tuendelee kwa kauli hiyo.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera ya Utafiti	260,665,000
Kifungu 0701	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na maelezo mazuri kama alivyosema ya Mhe. Waziri nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba umuhimu wa kubagua mafao ya mishahara na matumizi mengine kwa idara tofauti katika wizara. Kama nilivyosema katika mchango wangu kwamba nashukuru wizara imeanza angalau kutusaidia, lakini ni vizuri tunakokwenda badala ya walimu kuweka mishahara mfumo mmoja basi wale wa msingi waekwe mbali, wa sekondari mbali na wa Chuo Kikuu mbali kwa sababu yakupata ule uwiano. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri bajeti ijao tukijaaliwa aweze kuzingatia hilo.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa kuliona hilo lakini namuomba kwamba bajeti ijayo aweze kutuwekea ili tuweze kuona namna gani maslahi ya walimu yanavyosambazwa katika viwango tofauti. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0701	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	24,254,561,000
Kifungu 0702	Baraza la Elimu	30,000,000
Kifungu 0703	Shirika la Huduma za Maktaba ZNZ	237,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	101,000,000
Kifungu 1201	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	176,537,000
Kifungu 1402	Chuo cha Kiislamu Pemba	

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Waziri sana kwamba amejitahidi kunijibu na amefafanua vizuri sana, na kuna baadhi ya mambo ameniambia kama tayari sasa hivi yameshakaa vizuri. Lakini nilipokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Chuo cha Kiislamu nilimwambia Mhe. Waziri kama kipindi kilichopita cha miaka mitano bajeti zote zilizokuwa zikija hapa kila siku nilikuwa napiga kelele na waziri wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman. Sasa na kipindi hiki amepata mzee wangu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban lakini ni kwamba tumeshatabika na hizi ahadi tunazopewa kila siku kuwa hazitekelezwi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniambie kwa sababu ni ukweli usiofichika kwamba liko lile gari la kubebea mizigo, sio gari yakuwa mtu

amepata tatizo akachukuliwa kwa ajili ya kukimbizwa hospitali au kwenda kupata huduma nyengine zozote. Mhe. Mwenyekiti, kama ni mgonjwa hata akifika huko hospitali basi ameshazidi ugonjwa mwengine kwa gari ile ilivyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniambie kuhusu msikiti na gari hasa kule Chuo cha Kiislamu msikiti watajengewa lini kwa sababu wanatumia vyumba vya walimu ndio wanamosalia na gari hakuna. Hivyo aniambie atawasaidia vipi watoto wetu wa Zanzibar kutokana na chuo hicho ili waondokane na matatizo hayo waliyonayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo nilijibu suala la Mhe. Subeit kwamba gari ambayo iko kweli ni kubwa na tunaijenga bodi ili iwe ni gari ambayo wanaweza kupanda wanafunzi. Kabla ya gari hiyo ilikuweko gari ndogo ambayo ilikuwa ikifanya kazi pale, wao wenyewe wakasema gari iliyopo ni ndogo haitoshelezi. Kwa hivyo, sisi tukaondoa gari ile tukawapelekea gari kubwa hiyo wanayosema ni ya mizigo na tumeitoa katika umbile la mizigo ili waweze kupanda wanafunzi. Kwa hivyo, tunaomba watusubirie kwanza watumie hiyo gari iliyopo bajeti ikituruhusu tutahakikisha kama na hiyo gari ndogo kumbe walikuwa wakiitaka sisi tulikuwa hatujui tutawarudishia tena.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemuahidi na ni ahadi yangu ya mwanzo kwake, kwa hivyo asinipime kwa ahadi ya mwanzo muache aje anipe kwa ahadi ya pili. Yaani hii ya mwanzo itakuwa ndio kigezo. Kwa hivyo, namwambia kwamba mimi nitajitahidi wizarani kutafuta wafadhili na yeye atusaidie kutafuta wafadhili atakayefanikiwa mwanzo ndio msikiti utajengwa. Mimi napenda ujenge msikiti pale kwani ni sadakatul jaria na ninaomba Mungu nifanikiwe mimi ili iwe ndio benki yangu huko ninakokwenda. Kwa hivyo, hiyo kazi mimi nitaifanya inshaallah Mwenyezi Mungu akipenda namuahidi hilo, nitatafuta wafadhili na nitaujenga.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kauli moja anayoisema Mhe. Waziri imenishawishi kama nimkubalie na nimridhie. Kauli anayosema kama hii ni ahadi yangu ya kwanza mimi kwa hiyo naomba nimkubalie. Kwa hivyo, na mimi kutokana na hiyo kauli anayosema kuwa ni ahadi yangu ya kwanza na ni kweli tunaanza bajeti ya kwanza mwaka huu na inshaallah kama Mwenyezi Mungu akituwezesha mwakani inakuja tena, basi inshaallah na tuendelee namuachia subra.

Kifungu 1402	Chuo cha Kiislamu Pemba	30,000,000
Kifungu 1403	Chuo cha Kiislamu Unguja	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri kuwa Jimbo la Mpendae sasa litaishi katika hali ya matumaini. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Chuo cha Kiislamu Unguja Mhe. Waziri bado hajatueleza chuo kile kimegeuzwa jina au kimebaki vile vile kama kivyokuwa asili yake. Naomba maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Chuo cha Kiislamu hakijageuzwa jina na hata akitizama katika matokeo ya mitihani ya *form four* basi ile inaitwa ni *Muslim Academy* haijaandikwa jina jengine, matokeo yale huwa yanakuja pale kama ni wanafunzi wa *Muslim Academy* Zanzibar. Lakini tatizo pengine linaweza likawa limetokezea pale ni kwamba tuna mchepuo wa Kiislamu ambao wanafunzi tunaowapeleka pale wote ni waislamu, iko ndani ya jengo lile la Chuo cha Kiislamu.

Kwa hivyo ndio wanadhania kwamba tumeligeuza jina, ni kuwa hatujaligeuza jina na kazi inazozifanya ni zile zile kazi ambazo tangu *Muslimu Academy* iliyofanywa pale Forodhani kwenye jumba la watoto kwa sababu mafunzo ya ualimu tangu forodhani jumba la watoto mafunzo ya ualimu wa kiislamu yamekuwa yakitolewa. Kwa hivyo, kazi ile ile mpaka leo tunaendelea nayo katika Chuo cha Kiislamu Mazizini. Kwa hivyo, hatujaligeuza jina kile ni Chuo cha Kiislamu cha Zanzibar ndio jina lake mpaka sasa hivi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nakubaliana naye tuendelee na pia ile asilimia yangu 10 kwa Jimbo la Mpendae namrudishia.

Kifungu 1403	Chuo cha Kiislamu Unguja	30,000,000
Kifungu 1404	Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia	720,000,000
Kifungu 1405	Chuo cha Ualimu Benjamin Mkapa	30,000,000
Kifungu 1406	Chuo Kikuu	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi naomba niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutupa majibu katika masuala mengi ambayo tumeyaibua katika mjadala wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* bado majibu yake mimi hayakunitosheleza.

Nilikuwa naoma maelezo ametujibu kwamba fungu hili bajeti iliyotengwa ya 3.6 haiwezi kulingana na kauli ya serikali kwamba inakusudia kukiimarisha *SUZA*. Nilisema kwamba kilipoanza Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume alisema kwamba anataka hiki kiwe ni *at per* na vyuo vyengine vya Afrika

Mashariki. Nimesema *training* ukiitizama kama miaka mitano iliyopita tumekuwa tuki- *rang* hapo hapo bilioni 2.5, bilioni 3 hatuzidi. Mhe. Waziri majibu yake alitwambia kwamba kuna mapato pale ambayo Wizara ya Fedha haijaweza kuyaweka, sasa hilo mheshimiwa ni tatizo la serikali.

Mimi nilijaribu sana kupekuwa tulipokuwa tunapitia kwenye mapato Wizara ya Elimu *SUZA* haikuwekewa mapato yote, ndio kusema mpaka sasa hivi serikali haijui inapata kiasi gani. Kwa hivyo, mapato ambayo hayajuulikani hayawezi yakawa ndio majibu kwetu sisi kwamba hayo ndio yatafidia labda hili pengo ambalo linaonekana kubwa.

Sidhani hata kama yapo mapato hayo Mhe. Mwenyekiti, kwamba kweli yatawezesha Chuo Kikuu kukabili changamoto ambazo nimezitaja katika mchango wangu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo ya Mhe. Waziri zaidi pengine hili sio lake na bahati mbaya Waziri wa Fedha hayupo lakini tunaizungumzia serikali kwa ujumla wake, kwa sababu inawajibika serikali hapa Barazani kwa ujumla wake. Namuomba Mhe. Waziri atueleze serikali ina mpango gani wakuongeza bajeti hii ili kweli Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kisimamie yale makusudie ambayo yalianzishwa tokea kilipoanzishwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba chuo chenyewe hakiridhiki na shilingi bilioni 3.6, lakini hali halisi hii ni ruzuku na kawaida huwa inatolewa na Wizara ya Fedha. Na kwa sababu hiyo hii Wizara ya Fedha pengine wao wanakigezo chao juu ya kutoa ruzuku hii kwa 3.6 ambayo mimi siwezi kukujibu hapa kwa sababu sikijui kigezo wanachokitumia.

Ila ninajua kwamba tunayo haja ya kukilea Chuo Kikuu cha Taifa kifike kiwango cha kujitegemea kwa muda ambao kimeshafanya kazi. Kwa hivyo, suala la kujua kwamba wanakusanya kiasi gani ni wajibu wa wizara yangu na kazi hiyo ndio hivi sasa hivi ninaifanya nijue hasa kwamba wao wanakusanya kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo vyote sasa hivi vinaelekezwa vijitegemee, hata juzi kama tunakumbuka hapa *S.O.S* walifanya *fund raising* kwa sababu wale wafadhili wao waliwaambia kwamba sasa sisi tutazuia kwa sababu mfikie kiwango cha kujitegemea, ndio kitu tunachotaka sasa hivi. Kwa sababu chuo inakuwa ni kama shirika lazima mfike pahala pakujitegemea, ndio wakafanya *fun raising* ile wakapata walichopata halafu sasa wataongezewa chengine chochote.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Tunguu wameshaambiwa juzi na wafadhili wao kwamba na wao wafike kiwango chakujitegemea. Ndio maana walishtuka sana katika suala la kuondoa hii Pre-University kwa sababu waliona kwamba kuna fedha fulani watazikosa.

Mhe. Mwenyekiti, lengo letu sisi serikali vile vile kwamba hiki chuo kikuu nacho kifike kiwango cha kujitegemea, ruzuku tunaendelea kuwapa lakini na wao watengeneze mipango yakuweza kuongeza mapato. Kwa hivyo, kigezo gani kimetumika anachoniuliza Mhe. Jussa hicho mimi sitokijua kilichotumika, ila ninajua tu kwamba 3.6 bilioni ukifanya chuo kile ni pesa kidogo, hiyo nakubaliana naye mimi sijakataa.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kabisa kama ndio hizi hizi na kama kuna nyengine aniache nifanye hiyo kazi nyengine yakufanyia *auditing* kujua kwamba kwani kule kunaingia mapato kiasi gani? Hicho ndio kitu muhimu nitajua nifanye nini kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, wao wenyewe wanakwenda kujieleza sana kwenye Wizara ya Fedha juu ya masuala hayo, angalau walitaka safari hii wapatiwe angalau bilioni 8, lakini bado wamepata shilingi 3.6 bilioni. Kwa hivyo, nasema kwamba siwezi kumjibu suala lake kuwa kigezo gani kimetumika, lakini nakubali na kama wanavyokubali wenyewe watu wa chuo kwamba wanalalamika kuwa hiki kiwango ni kidogo. Mimi nakubali kwa kuendesha chuo kwa sababu chuo hatuwezi kukiendesha kama tunavyoendesha Sekondari ya Lumumba. Mhe. Mwenyekiti, lakini pengine uwezo wa mapato ndio umetufikisha hapa ili pengine ndio linaweza kuwa ndio tatizo letu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie na nimuhakikishie Mhe. Waziri kwamba namuheshimu sana na nalielewa tatizo alilonalo, ndio maana nikasema hapa serikali inawajibika kwa ujumla wake, nilitegemea waziri anayeshughulikia masuala ya fedha atujibu, lakini kama hayupo atakuwepo japo kaimu wake au kiongozi wa serikali atujibu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwanza hoja ya kwamba vyuo vinatakiwa vijitegemee mimi naikubali, lakini kama alivyosema mwenyewe kwamba vinalelewa na Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* hakijaanzishwa muda mrefu chakuwa tegemeo kwamba kitasoma kwa miguu yake.

Mhe. Mwenyekiti, tunalea mashirika hapa yanatafuna fedha sijui miaka mingapi hayaleti tija yoyote katika nchi na tunaendelea kuyapa fedha, seuze chuo ambacho kinatuandalia vijana wetu kuja kuchukua nafasi muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, hiki ni Chuo Kikuu cha Taifa Wizara ya Fedha ina Chuo cha Fedha Chwaka, ukenda ukitizama bajeti yake

humu imetengewa takriban bilioni 1 na zaidi. Kwa hivyo, nashangaa kwamba hiki chuo kinachosimamia mafunzo fulani tu kina bajeti takriban nusu ya iliyotengewa Chuo Kikuu cha Taifa. Hiki ambacho ndio tunategemea kiwe mlezi wetu na vijana wetu wote ndio kinatengewa milioni 3.6. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema nakubali kwamba kinalelewa lakini hakijafika pahala pakusimama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kauli ya serikali hapa sijui atajibu nani watachaguana wenyewe katika serikali. Lakini kuna mfuko mkuu wa hazina umetengewa katika bajeti hii zaidi ya bilioni 40, hasa tuambiwe kutachomolewa ngapi kule ili zisaidie *SUZA*.

Kwa sababu haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, chuo ambacho kimepeleka bajeti yake bilioni 26 inakatwa mpaka wakapewa bilioni 3 ningeelewa angalau ingekuwa bilioni 15 au 10, lakini inatoka bilioni 26 mpaka bilioni 3, ama kama hatuwezi basi serikali itowe kauli hapa kama inakifunga Chuo Kikuu kwa sababu kuendelea kuwa na chuo ambacho hakitekelezi makusudi yake inakuwa hakina maana. Kwa hivyo, naomba serikali itujibu kwamba inakusudia kutoa kiasi gani ili ipate chuo hiki angalau kiweze kusimama na haya mapungufu waliyonayo yaweze kufikiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwamba ukusanyaji wa mapato umekuwa mdogo ndio maana tukakata pesa hizi 3.6 bilioni, nadhania sina hakika. Lakini pengine Wizara ya Fedha inaweza ikawa ina vigezo vyake alivyovitumia ndio suala nasema mimi siwezi kulijibu.

Lakini kwa upande wangu nataka kujua hasa *SUZA* wanakusanya kiasi gani? Hilo suala mimi nataka kujua kwa hivyo ukiniuliza nitakuwa narejea hapo hapo ili nijue niweze kujenga hoja yangu vizuri. Hili ndio suala ninaloweza kulizungumza mimi.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kwamba chuo kile tumekianzisha ili kutafuta manufaa ya nchi yetu, ili tupate kuwasomesha vijana wetu na alhamdulillahi kinatusaidia maana tumeshatoa vijana wengi na wanatusaidia sana. Tatizo nikuweza kukikimu hilo ndio tatizo nakubali kabisa, lakini hata hivyo najua serikali haitakiacha tu chuo kile kidorore bila shaka serikali itaendelea kukinyanyua chuo kile ili kiweze kufanya kazi ile iliyokusudiwa kama kawaida. Hiyo ndio ninayoijua kusema mimi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimesikitishwa kidogo kwamba kama nilivyosema sitegemei suala hili nijibiwe na Waziri wa Elimu kwa

sababu keshasema mwanzo kwamba yeye hanan majibu, nilitegemea serikali kuu inijibu kwa sababu Katiba hii inasema mawaziri kwa ujumla wake watawajibika katika Baraza hili kwa hiyo nilitegemea nipate kauli ya mwengine anayehusika na masuala ya fedha kwa wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo utaratibu huu tunapitisha vifungu lakini Waziri anayehusika na Masuala ya Fedha au hata kaimu wake hayupo hapa sio utaratibu mzuri katika Baraza lako. Kwa hivyo, nasema kama serikali haina jibu mpaka awepo Waziri wa Fedha nitasema tuendelee kwa sababu sio suala la Mhe. Waziri wa Elimu, lakini nitakuja kumbana Waziri wa Fedha atakapokuja na bajeti yake. Kwa sababu haingii akilini kwamba serikali nzima ikae kimya juu ya hoja hii ikamuachia Mhe. Waziri wa Elimu peke yake kama hakuna jawabu Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuombe Mhe. Jussa akubaliane na yale maelezo ya awali ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ya kwamba ameikubali hoja yake kwamba ni hoja ya muhimu, na hoja ambayo inahitaji kufanyiwa kazi na serikali. Lakini la pili nimuombe vile vile Mhe. Jussa asifikie maamuzi yakuona kwamba serikali inashindwa kutoa kauli kwa sababu tulikuwa hatujafikia hapo Mhe. Waziri muhusika alikuwa mwenyewe anaendelea kujibu hoja kwa mujibu wa mipango yake ya wizara. Lakini haijafika pahala kwamba serikali inashindwa kulitolea kauli juu ya suala lake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Jussa kwamba ni kweli ameonesha kuwa ziko bilioni 40 ambazo ziko kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa na nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba hata hizo bilioni 40 sio zimekaa tu hazijapangiwa mambo isipokuwa ni kuwa zipo kwa sababu serikali haiwezi kuwa haina akiba ya kusema kwamba linatokezea jambo la dharura ikashindikana kabisa serikali kuweza kulifanyia kazi jambo hilo.

Lakini mimi nimuombe Mhe. Jussa kwamba akubaliane na Mhe. Waziri wa Elimu kuwa jambo hili kwanza *SUZA* inakusanya kweli mapato, kilichokosekana hapa kwenye maelezo ya Mhe. Waziri pengine ni kuonekana yale mapato yanayokusanywa ni kiasi gani na yanatumika vipi. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni jambo ambalo nafikiri Mhe. Waziri anaweza akenda akakaa baadae Mhe. Jussa na Baraza lako kwa jumla likaweza kupata taarifa kamili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimuombe Mhe. Jussa akubaliane na maelezo ya Mhe. Waziri au maelezo ninayoyatoa mimi kwamba hili jambo kwa kuwa

limeonesha umuhimu wa *SUZA* kuongezewa kasma ni vizuri aiachie serikali Mhe. Waziri alichukue alipeleke serikalini ili kuona uwezekano huko mbele kama serikali inaweza ikaona uzito wa jambo hilo na ikaweza kulifanyia kazi kwa kuwaongezea kasma kidogo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba aichie serikali kwa sababu hatujui hizi bilioni 40 hasa ziko katika maeneo gani. Kwa hivyo, amstahamilie Mhe. Waziri alichukue na Mhe. Waziri alipeleke serikalini ili kuona uwezekano kama serikali inaweza ikafanya chochote juu ya jambo hilo. Naweza nikasaidia hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, najua unajitahidi kwa upande wa serikali lakini ninachosema ningekubaliana na Mhe. Haji kwa niaba ya serikali, ikiwa serikali itaona uzito ni kama vile haijaona uzito bado juu ya suala hilo. Mhe. Mwenyekiti, suala hili halina tofauti na suala la *ICU* ndio nasema na *ICU* lilipata majibu hapa kwa sababu ilikuwa Waziri wa Fedha alikuwepo, hasa hapa tunapata hiki kigugumizi kilichokuwepo kwa sababu inaonekana mtu mmoja tu ndio anaweza kuijibia serikali. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ukisoma Katiba kifungu cha 43 kifungu kidogo cha 5 kinasema

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wakufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla, na mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi najua tutapigishana kelele hapa hatupati jawabu, lakini ninachosema kwamba siwezi kumkwamishia bajeti yake Mhe. Waziri wa Elimu kwa sababu yeye katika hili ni kama vile ilivyokuwa kesi ya Wizara ya Afya. Yeye ametaka zaidi lakini hakupewa, mimi nakubali kwa kauli moja ya serikali kwamba serikali sio kama haitaona uzito, serikali itupe *commitment* kwa sababu kwa kawaida katika kila bajeti lazima kunakuwa na fungu la kuangalia mambo kama haya ambayo yana upungufu.

Kwa hivyo, mimi naamini katika huo Mfuko Mkuu wa Hazina kama haupo upo katika mashirika ya serikali yanayolelewa miaka 20 au 30 na wala hayazai kitu haiwezekani Chuo Kikuu ambacho tumekianzisha miaka 5 au 7 iliyopita tuweze kusema kishatengewa bajeti yake. Kwa hivyo, naomba nipate kauli ya serikali kuwa hili nakwenda kulifanyia kazi na nitalitafuta popote pengine ili niweze kuwaongezea bajeti angalau kiasi fulani *SUZA* haya mambo niliyoyataja ya kukimbiwa na walimu, yakuajiri maseketeri badala ya wahadhiri na kupata huduma zake za msingi yarekebishwe ili wanafunzi wetu waweze kusomeshwa na kukabiliana na changamoto za dunia ya leo. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kauli ya serikali, tuendelee.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, naomba turudie kwenye kanuni kifungu cha 96 (e) nayo inasomeka kama hivi ifuatavyo:

"Ikiwa baada ya mjumbe kueleza nia yake na sababu zake za kutaka kutoa hoja hiyo waziri anayehusika atashindwa kumtosheleza mjumbe, basi Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza au waziri mwengine yoyote anaweza kutoa ufafanuzi zaidi dhidi ya sababu za mjumbe kutoa hoja hiyo. Lakini kifungu cha (g) kinaendelea kusema kuwa ikiwa baada ya hatua iliyoelezwa katika aya ya (f) haikukubaliwa na mjumbe akashikilia hoja yake basi itapigiwa kura".

Kwa hivyo, Mhe. Mweyekiti, kwa mujibu wa kifungu hiki cha kanuni naomba serikali iwajibike kujibu suala la mjumbe vyenginevyo itabidi tuingie kwenye kura. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kanuni aliyoisema Mhe. Mjumbe hivi sasa haijafika wakati wake kwa sababu kwa mujibu wa utaratibu wakati wa kanuni zetu ni kwamba waziri anayehusika anajibu hoja za mjumbe, na ilivyo ni mara tatu. Lakini waziri mwengine yeyote anaweza akamsaidia waziri anayehusika. Kwa hivyo, hivi sasa kiwango kilichofikia hivi sasa Mhe. Haji Omar Kheir alikuwa anamsaidia Mhe. Waziri husika. Kwa hivyo, hiyo stage hiyo hatujafika wana haraka, mimi naomba wapunguze hiyo haraka yao twende kwa utaratibu halafu hapo ambapo tutafikia *stage* hiyo ndio pengine Kiongozi wa Shughuli za Serikali anaweza akaingilia ambapo *stage* bado haijafika, na kama ikifika huko ndio hapo tena mwisho tunaweza tukapiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kutoa maelezo ya kina juu ya suala hili. Lakini nataka nimuombe sana Mhe. Jussa kwamba waziri yeyote anaposimama hapa anazungumza kwa niaba ya serikali, ndio maana ya mawaziri kuwepo hapa. Kwa hivyo, itakapofika sisi sote tumeshakwama Kiongozi wa Shughuli za Serikali anawajibika vile vile na yeye kutoa kauli ya kwa niaba ya serikali. Lakini waziri yeyote atakayesimama hapa anasema kwa niaba ya serikali. Kwanza utaratibu huo naomba Mhe. Jussa akubaliane na mimi.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema kesi hii ni tofauti na ile kesi ya Wizara ya Afya, kesi ya Wizara ya Afya walikuwa hawakutenga kasma ya lile suala.

Lakini kesi hii ni kwamba bajeti ya *SUZA* ipo lakini tatizo haitoshi, sasa ndio maana Mhe. Ismail Jussa yeye anashauri kwamba serikali ione uzito.

Serikali inaona uzito kwa sababu kama serikali ingekuwa haioni uzito isingesema kwamba hili suala inalichukua na italifanyia kazi. Kwa hivyo, kusema inalichukua na kulifanyia kazi ni kwamba serikali inaona uzito na ndio maana hata hiyo siku Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hakusema atatenga kiasi gain alisema yeye atashirikiana na Wizara ya Afya ili waone kwa kiasi gain serikali itaweza kutenga hizo fedha kwa ajili ya *ICU*.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Jussa akubali kwamba serikali kama alivyosema Mhe. Waziri wa Elimu kama waziri anayesimamia sekta, kwamba analichukua na atalifanyia kazi, kwenda kuiambia serikali kuwa hili jambo lazima lipewe uzito wa aina yake.
Mhe. Mwenyekiti, maelezo yangu ni hayo namuomba sana Mhe. Jussa akubaliane na hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie kabisa rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba sina nia ya kuwa nipate kauli ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nimekisoma kifungu hicho kusema kwamba serikali kwa ujumla wake inawajibika.

Pili, niseme kwamba, niliposema hivyo kwa sababu jawabu lake la mwanzo lilitanguliwa na neno ‘linachukuliwa na serikali kama itaona lina uzito’. Sasa nafurahi kwamba katika maelezo yake ya sasa hivi ndio pamekuja *commitment* ya serikali, kwamba serikali inalichukua na kwa uzito wake kwenda kukaa nalo ili kuona kiasi gani inaongeza fungu. Nakubali tuendelee kwa sababu hiyo tu Mheshimiwa kwamba serikali inalichukua na itakwenda kukaa kuona itachomoa wapi ikiwa kwenye mashirika yaliyokuwa hayatusaidii chochote, ikiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina lakini bajeti ya *SUZA* kuongezeka. Kwa *commitment* hiyo Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati na mimi nachangia hapa juzi nilieleza kwamba Chuo cha *SUZA* kina mpango wa kufungua tawi la kilimo katika Kisiwa cha Pemba, lakini hadi leo hii yaani chuo kinasumbuliwa na mamlaka husika inayohusiana na mambo ya ardhi kupewa ardhi iliyopo Chamanangwe kwa ajili ya kufungua *department of agriculture*. Je, waziri anaweza kunieleza nini katika hili, ni vipi wizara itawasaidia *SUZA* ili kuweza kupata hii ardhi na kuweza kufungua *department of agriculture.*

Jengine ni kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu nilisema ni *Potential Scientist,* wanatakiwa wafanye kazi kupitia vitendo. Kwa bahati mbaya sana mwaka jana wanafunzi wa fizikia pale hawakuwahi kufanya mafunzo ya vitendo jambo ambalo ule ufahamu wao, kwa sababu wanafunzi wanatakiwa wawe *on practical* ili aweze ku-*develop fact thought, understanding and curiosity*. Sasa ikiwa huku mwanafunzi wa science hakuwa *on practical* ile *intellectually honest* ataipataje. Kwa ivyo, ni vipi sasa huyu waziri anaweza akawasaidia *SUZA* wakaamudu pamoja na Serikali Kuu kuongeza bajeti pale, vipi serikali kuu itaongeza bajeti kwa *SUZA* kusudi waweze kumudu mafunzo ya vitendo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nije kwenye hili suala la ardhi, tunalichukua na tumeshaanza kulichukua na kulifanyia kazi kwenye Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya kuweza kupata hicho kiwanja ambacho amekizungumza Mheshimiwa. Hilo suala linaendelea na liko kwenye *pipe line* na Inshaallah Mwenyezi Mungu atatujalia tutafanikiwa.

La pili kuhusu mafunzo ya vitendo. Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwama kwa mwaka huu wanafunzi wa *physics* hawakuweza kufanya *practical* zao kwa sababu ya matatizo ya vifaa vya kufanyia hiyo *practical.* Lakini hata hivyo, safari hii kwa sababu hawajamaliza *program* yao na madhali hawajafanya *practical* ndio maana hawajamaliza *program* yao. Kwa hivyo, safari hii *program* yao watakwenda kufanya Dar es Salaam, lakini kwa mwakani tutakuwa tuna mambo mawili mazuri.

Kwanza *World Bank* wametengeneza *package* ya vifaa vya maabara pamoja na kompyuta ambao wanakusudia kutukabidhi mwaka huu na mwaka 2012 tutakuwa tumeshajipanga vizuri kwenye hilo. La pili tuna *campus* yetu ya Tunguu ambayo itamalizika mwezi wa Disemba tutakabidhiwa na Pemba kwa ajili ya vifaa vya maabara kwa Tunguu imeshafunguliwa tayari. Kwa hivyo, pale pia patakuwa na vifaa vya maabara na tutakuwa na tuna maabara pale Tunguu na tutaziboresha zile maabara zilioko Nkrumah kwa ajili ya wanafunzi wetu kwa hivi vifaa tutakavyovipata kutoka *World Bakn* kwa ajili ya kuondoa tatizo hili. Kwa mwaka huu tutakwenda kufanya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini mwakani tunategemea suala hili litakuwa limemalizika *Inshaallah*.

Kifungu 1406	- Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar	3,600,000,000/-
Kifungu 1407	- Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar	

Mhe. Sale Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia pale katika kipengele hiki cha Mafunzo ya Amali niliipongeza sana serikali kwa kuweza kuanzisha elimu hii ambao inaisaidia sana vijana wetu kupata ajira

pamoja na kujiajiri wenyewe. Lakini nikasema kwamba kuna kile Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichoko *Fidel Castro*, Vitongoji, chuo kile kimejengwa katika ardhi ambayo wananchi walikuwa na mazao yao mengi, huu ni karibu mwaka wa tano wananchi wale mazao yale hawajalipwa fidia. Pamoja na kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais nilimpeleka yeye mwenyewe katika ardhi ile kwenye Chuo cha Mafunzo ya Amali na kuona na kuniahidi, lakini hadi leo hii wananchi wale bado mazao yao hawajalipwa. Sasa nataka anieleze Mhe. Waziri ni lini serikali italipa mazao yale.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu wakati nilipokuwa nikitoa ufafanuzi wa michango mbali mbali ya wajumbe, kwamba makisio kwa ajili ya fidia za Vitongoji yalifanywa mara ya mwanzo lakini yalikuwa makubwa sana. Lakini hata hivyo, wizara ikachukua hatua ikasema kwamba, kwa kuwa makisio yanafanywa tena lakini huku kuna mali za wananchi basi wananchi tunawaachia wavune mali zao. Kuna mivinja pale wananchi wanavuna mivinja yao wala hatujawazuia sisi, lakini fidia yao italipwa baada ya kukamilika utaratibu wa kutizamwa upya na mamlaka inayohusika na kufanya tathmini ya mazao, hili suala linafanywa. Kwa hivyo, namuahidi Mhe. Mjumbe kwamba, tathmini ikimalizika fidia ya watu wale watalipwa, nakubaliana naye juu suala hilo tutawalipa fidia hakuna tatizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika. Kwa sababu ni karibu miaka sita wataalamu tulionao hata ingelikuwa wanatumia hesabu za kuchora kwa kalamu tu, mambo siku hizi ni *computer rise*, miaka sita masikini ya Mungu umemng'olea mihogo yake, migomba na hukumpa sehemu nyengine ya kilimo wewe umemuondosha tu pale. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ningeomba sasa Mhe. Waziri aniambie ni lini. Kwa sababu wanasheria wanatwambia kwambahaki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa.

Hiyo tathmini anayoifanya ni ya miaka sita iliyopita, sasa *rate* watakayofanyia ni ya miaka sita au ni ya leo? Vile vile nataka kujua kwa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, naomba anipe maelezo hayo na anifahamishe ni lini. Kwa sababu bajeti kadhaa zimepita wala hatuoni kwenye vitabu kama mmewapangia hii, hivi nadhani ni kwenda kinyume na haki za binadamu na utawala bora. Wale ni walipa kodi wan chi hii wawa;lipe ili watate nguvu ya kuendelea kulipa kodi ambayo iatendelea hata kutufanya sisi kuendelea katika Baraza hili naomba maelezo ya ziada ya Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama ningelisema kwamba hatutawalipa ningekuwa nimefanya ubabe, lakini

sikukusudia kufanya ubabe kwa sababu najua kuwa nia ya wizara yangu ni kuwalipa fidia zao isipokuwa hesabu zikae vizuri. Ni kweli hivi sasa kazi ile inafanywa kwa kutumia komyupa na mambo gain, lakini sisi sasa mpaka tuletewe na wale wanaohuisika na kufanya tathmini? Hawajatuletea kwa sababu tathmini hatufanyi Wizara ya Elium, tathmini kuna idara makusudi inayohusika na masuala ya tathmini ya mazao hao watuletee.

Mimi nafikiri kwa jitihada yake anayoichukua sasa watu wa tathmini watakuwa wamejua kwama sasa hivi tahmini kwa ajili ya Vitongoji inatakiwa haraka na ikiletwa sisi tutawalipa. Hili tutajitahidi kuona kwamba tunawalipa fidia zao zile.

Lakini bado narejea kusema kwamba, hatwendi kinyume na haki za binadamu kwa sababu hatukuwazuia kuvuna mali zao, mali zao wanavuna wenyewe na wanauza mivinje pale ukipita inavunwa na inauzwa. Kwa hivyo, wanapata mara mbili kwanza wanapata kutokana na mazao yao, pengine tungewalipa tungechukua sisi lakini tumewaambia waache watumie wao halafu baadae vile vile tutakuja kuwalipa hiyo fidia hatuna matatizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna mazao ambayo wameyaacha na kuna mazao ambayo yaling'olewa kwa kupata nafasi ya kuweka hayo majengo. Sasa akisema kwamba kuna mazao tumewaachia wavune wenyewe waziri simfahamu hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Nasaidia kidogo, waziri kasema hivi mambo mawili tofauti kabla. Jambo la kwanza kwamba hao wanaofanya tathmini hawamo Wizara ya Elimu na wamepewa hiyo kazi wanaikamilisha kasha ikishakamilishwa wakipeleka Wizara ya Elimu watalipa. Hiyo ilikuwa hoja moja. Lakini ya pili yale mazao yaliyobaki watu wanavuna na wizara pia inawaachia watu wavune. Kwa hivyo, nadhani bado haki itatendeka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, labda nimalizie tu kwa kusema kwamba, labda Mhe. Waziri awaambie watu wa Vitongoji katika eneo la *Fidel Castro* wakulima kwamba miaka sita yote iliyopita kwa sababu hawajapata fidia yao labda ni kwa uzembe tu wa watendaji, atamke hivyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Mwenyekiti, mimi siwezi kusema kwa uzembe wa watendaji, ninachoweza kusema kwamba tathmini ya kwanza hatukuikubali tunataka tathmini sahihi. Kwa hivyo, watuletee tathmini sahihi tuwalipe hiyo ndio haja yangu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mimi nadhani kwa sababu Mhe. Waziri kasema kwamba wataalamu wanaendelea na kuchakachua basi nakubaliana naye.
Kifungu 1407 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar 1,200,000,000
Kifungu 1408 -

Mhe. Mahammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia katika Mfuko wa Bodi ya Elimu nilisema wanafunzi wengi wanakosa kupata fursa ya kuingia vyuo vikuu kwa sababu ya kukosa mkopo katika bodi hiyo. Katika maelezo ya Mhe. Waziri ameseme ametengewa kiasi cha shilingi bilioni nne ambazo hazitoshelezi. Swali langu liko hapa.
Hawa watoto wa wakulima, wakwezi na wafanyakazi wa nchi hii waliokuwa hawakupata mkopo huu nini wafanye, au wakae tu nyumbani. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Mhe. Mwakilishi ashukuru na aone fahari kwamba serikali sasa hivi imeweza kuwasomesha watoto wengi na mpaka wanafika kupata sifa za kuingia katika vyuo vikuu, hizi ni jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hapo nyuma tulipoanza kutangaza elimu bila ya malipo hao wanafunzi waliokuwa wanakwenda kusoma vyuo vya nje walikuwa hawazidi 20, sana wanafunzi walikuwa 10, 12, 5 kwa sababu hizo skuli hazikuwepo, lakini sasa hivi vyuo vipo.

Unapopata maendeleo basi pia utapata na matatizo ya maendeleo, tumepata maendeleo ya kuweza kuwasomesha vijana wetu hapa na mpaka wakawa wana-*qualify* kuingia vyuo vikuu tuna wanafunzi 1,365 wana-*qualify* kuingia katika vyuo vikuu sasa hivi, lakini tunapata matatizo ya maendeleo nini, uwezo sasa hivi wa kuwapeleka katika elimu ya juu, hilo ndio tatizo. Sasa tunaomba kwamba serikali itajitahidi kwa upande wake na wazee nao wajitahidi kwa upande wao ili hawa watoto wetu wapate kusoma, hicho ndicho cha muhimu kusema kweli, lakini wao wamesha-*qualify* na sifa zao wanazo.

Mhe. Mwenyekiti, watu 1,365 si mchezo ni maendeleo makubwa hayo ambayo tumeyapata hivi sasa. Kwa hivyo, wanaweza wakajiendeleza wanaweza wakaingia katika masomo mengine, sasa namwambia kwamba uwezo wetu safari hii tumepata hizi shilingi bilioni nne tutazitumia kwa ajili ya kuwakopesha vijana katika masomo ya elimu ya juu, tutazitumia, lakini tu-*appreciate* kwamba tumefika mahala hivi sasa kuwa tumeshapiga hatua kubwa sana na Mwenyezi Mungu akitujalia tukipata mafuta tatizo hili halitakuwepo litakuwa limeshaondoka.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri nathamini sana juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini *average* ni ndogo ya wanafunzi ambao wanachukuliwa na wengi wanabaki mitaani tuwafanye nini? Hiki ndio kilio changu na ninataka nipewe maelezo ya kina hapa. Halafu kuna Bodi ya Taifa ya Elimu *average* niliuliza ni ndogo zina uwiano gani wa wajumbe, tunapata wajumbe au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata kuingia wajumbe wangapi kwenye bodi ile. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nafurahi kwa maana ya *appreciate* jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ninafurahi sana, lakini nilisema katika maneno yangu kwamba, unapopata maendeleo unapata pia na matatizo ya maendeleo. Kwa hivyo, maendeleo tumeyapata lakini tunapata matatizo ya maendeleo sasa hivi.

Uwezo wetu wa mapato yetu ni mdogo, kwa hivyo inabidi tujue kwamba hii ni changamoto ambayo sisi tunayo, lakini jitihada ya Baraza hili la kutaka kuongeza vyanzo vya mapato ndio maana Baraza hili limekuwa likitilia mkazo sana suala la sisi kuruhusiwa kama mafuta yapo Zanzibar tuyachimbe ni kutatua matatizo haya. Sasa siwezi kumjibu zaidi kitu chengine isipokuwa najua kwamba sasa tuna matatizo kwa sababu tumeleta maendeleo na ukileta maendeleo ndio unapata matatizo hii ndio hali halisi.

Tuangalie katika utaratibu wa kawaida tu wa namna tunavyoishi hapa, maisha yetu ya zamani na ya sasa tofauti, maisha yetu ya sasa hivi pamoja na hali ya umasikini lakini tunamiliki kula vyakula vya mafuta, vya kukaanga, pilau, biriani, tunakuwa na matatizo, sukari, pressure na mambo mengine kama hayo kensa, ndio maendeleo matatizo yake hayo. Kwa hivyo, tujue tuna matatizo sasa lazima twende na hali hiyo.

Mhe. Mjumbe sasa ajue kwamba nia ni kuwasomesha watu wote lakini hatuwezi kwa sasa, wananchi wananisikia huko kwamba jitihada imefanyika na serikali ina watu elfu moja na mia tatu na zaidi wame-*qualify* hatuwawezi, tushirikiane sasa kama tunaanzisha *NGOs* za kusomesha vijana wetu, tunaanzisha mambo mengine ya kusaidia michango mbali mbali ya kusomeshea vijana wetu ndio tutaweza kupiga hatua hivyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mimi sikubaliani na Mhe. Waziri kusema maendeleo ni kupata maradhi, lakini kwa shingo upande nakubali hili naomba tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, swali langu litakuwa tofauti na Mhe. Mohammed Said, siwezi ku-*demand* kuongezewa zaidi, kwa sababu kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwamba ndani ya kipindi kifupi alichoingia hapa kafanikiwa kui-*convince* serikali kupandisha bajeti ya Mfuko wa Elimu kutokana na nilivyoziona pale shilingi 1.6 bilioni 2.5 bilioni mpaka kufikia shilingi bilioni nne kwa hivyo nataka nimpongeze sana. Lakini suala langu nilipokuwa nataoa mchango wangu nilizungumzia kwamba kuna fununu huko nje kuwa serikali huko nyuma wizara hii ilipeleka wanafunzi zaidi ya uwezo wake katika kuwahudumia. Kwa hivyo matokeo yake kile kidogo kimekuwa kinagawanywa kidogo kidogo mno matokeo yake hakimsaidii kila mtu na kupelekea wanafunzi wetu walioko katika vyuo vya elimu ya juu mbali ya vya nje ambavyo mara nyingi niliviulizia maswali humu ndani, lakini hata hapo kwetu Tanzania Bara tu hapo zile huduma za msingi wanazikosa sasa nataka kujua.

Nimesoma takwimu ambazo Mhe. Waziri katupa katika ukurasa wa 56 wa kitabu chake cha hotuba akielezea kwamba kwa mwaka jana wanafunzi wapya walikuwa 653 tu, lakini kwa jumla hivi sasa serikali ina wanafunzi 1,022 ambao wanasoma katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi. Sasa nataka kujua kwamba hizi *crisis* mnazokabilianano nazo na nadhani Mhe. Waziri kwa sababu ni mwalimu anajua kuwa hakuna kitu kibaya kama mwanafunzi kuwa anakabiliwa na mtihani halafu ndicho kipindi ambacho anakuta hana pesa za uongozi wa chuo, kwamba kama hujalipa basi huwezi kufanya mtihani. Sasa tujaalie kwamba serikali inapokuwa inamuweka katika wakati mgumu mwanafunzi kama yule

Mhe. Mwenyekiti, nataka kupata uhakikisho wake tu katika hili wala sikusudii kuzuia fungu wala kitu chochote nataka kupata maelezo yake tu. Katika kuongezewa lile fungu je, lina lengo la kutatua matatizo ya wanafunzi ambao walipelekwa huko nyuma zaidi ya uwezo wa serikali na kusababisha *crisis* hii au itakwenda kuongeza na wengine wapya kiasi ambacho tatizoi litakuwa linaendelea. Nataka ufafanuzi wake wa kina kwa sababu wakati wa majibu yake sikulisikia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kilichosababisha kuongeza wanafunzi kuwa 653 ni kwa sababu ya hiyo idadi yao ya wingi, kwamba wengi wame-*qualify* kwa hivyo badala ya kuchukua wale tuliowakusudia tu, tumeongeza na tumechukua 653. lakini jitihada gani tumeifanya?

Baada ya kuona kwamba tumeshapeleka zaidi ya wanafunzi wale wambao walikuwepo pale mwanzo hatukuweza kuwaacha hivi hivi tuliona lazima

tuongeze kidogo tumehamisha mafungu yetu ya wizara, *one billion* tumezigawa kutatua hayo matatizo ambayo yako katika wanafunzi walioko sehemu mbali mbali.

Tunashukuru jambo moja, vyuo vinatukubali tunapowaambia tuna matatizo na tukawapelekea barua kuwaambia hali halisi yetu wanatukubalia na kusema basi waache waendelee, lakini tulipeni na tunafanya jitihada tunawalipa. Kwa hivyo, jitihada tunaichukua na tunafanya. Nataka nimwambie tu kwamba, ni kweli tatizo hili limetokezea na hata safari hii hizi bilioni nne zinachoweza kufanya ni kutosheleza wale walioko nje tu, lakini bado tutalazimika kukata baadhi ya mafungu ili angalau na wengine kidogo tuwapeleke wapya isiwe tena ndio hatupeleki kabisa, hiyo jitihada tunafanya ni *challenge* ambayo sisi Wizara ya Elimu tunayo na tunakwenda nayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nafurahi na maelezo ya Mhe. Waziri niseme tu kwamba nai-*appreciate consurn* yake na kama nilivyosema najua mengine haya si yao wameyarithi, lakini nilikuwa naomba kwamba, katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha wajitahidi kukaa karibu na wanafunzi kupitia serikali zao ili haya matatizo yao waweze kuyajua. Kwa sababu wengi hawa wanakimbilia kwetu kulalamika kutokana na *crisis* wanazozipata.

Nataka nimhakikishie Mhe. Waziri pamoja na jitihada zote wanazozifanya lakini bado uongozi wa vyuo mbali mbali wanawaharasi wanafunzi wetu kwa sababu kutoa barua tu kwamba waachwe waendelee na mitihani serikali itawalipia bado mara nyengine haitoshelezi katika baadhi ya vyuo, kila binadamu tunajua na maumbile yake alivyo. Kwa hivyo, nakubaliana na maelezo yake nataka tuendelee lakini nimuombe katika mwaka ujao wawe karibu na serikali za wanafunzi wayajue matatizo ya vijana wetu wanaowapeleka pale matatizo kama hayo. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tulitaka Mhe. Waziri atufafanulie kwa faida ya Baraza lako atwambie tu katika hii Bodi ya Elimu ya Juu wajumbe wetu ni wangapi wanaotuwakilisha kwa upande wa Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara ni wangapi.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naogopa wakati unamalizika, hatuwezi kujirekebisha kabisa.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Kwa kuwa muda wetu uliobakia tuna wasiwasi hatuwezi kumaliza vifungu vyetu. Kwa hivyo, tunakuomba Mwanasheria Mkuu uweke utaratibu ili tuendelee.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki hautoshelezi kupitisha hoja hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako likubali kuongeza muda mpaka tutakapomaliza kupitisha hoja hii ya Mhe. Waziri wa Elimu naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wanaokubaliana na hoja mkono juu. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilimtaka Mhe. Waziri atusaidie kujua hii Bodi ya Elimu ya Juu ni wajumbe wangapi waliopo wa hapa kwetu Zanzibar na wangapi wa Tanzania Bara kwa faida ya Baraza lako na sisi tunataka kujua.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe nataka nimwambie kwamba moja katika sababu zilizosababisha kuanzisha kuanzisha Chuo Kikuu chetu hapa uamuzi ambao ukatusaidia tukaweza kupata Vyuo Vikuu vyengine baada ya kile kimoja tulichokuwanacho, na moja katika sababu iliyosababisha na sisi kuingia katika hili zoezi la kutoa mikopo kwa vijana wetu ni kwa sababu tunataka maendeleo ya vijana wetu haraka.

Hata hivyo, sisi tunapata mara mbili sasa hivi, tunapata kuwapitisha katika bodi yetu na pia tunapata kuwapitisha katika Bodi ya Jamhuri ya Muungano. Kwa bahati katika Bodi ya Jamhuri ya Muungano tuna wajumbe wanne kati ya wajumbe 14 wanaohudhuria katika bodi hiyo.

Sasa kinachotakiwa hapa ni ukakamavu wa wajumbe na hii ndio inayosaidia baadhi ya wanafunzi wetu wanaotoka hapa Zanzibar wanapata kule mikopo na baadhi ya wanafunzi wetu wanapata hapa mikopo kutegemea zile *pass* zao zinavyokuwa zimekaa vizuri katika suala la masomo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndio hali halisi na tuombe Mwenyezi Mungu tuendelee hivyo kule tupate na huku tupate, dogo dogo nyingi yafanya kubwa moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana naye kusema kwamba huku tunapata na kule tunapata, lakini kwa sababu hiki chombo ni taasisi ya Muungano, sasa je, kuwa na wajumbe wanne Mhe. Waziri haoni kuwa ni wajumbe wachache mno. Kama ni wachache je, wizara yake itachukua jitihada gani angalau tupate tena wajumbe wawili, lakini wajumbe 14 tuna wanne ni wadogo mno Mhe. Waziri na wakati hiki chombo ni cha Muungano. Ningemuomba Mhe. Waziri wizara yake ichukue jitihada ili tupate nyongeza angalau kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri ataifuatilia hoja hiyo ya msingi. Tunaendelea.

Kifungu 1408	- Mfuko wa Elimu ya Juu	4,000,000,000
Kifungu 1409	- Bodi ya Upimaji Tathmini	1,482,000,000
Kifungu 1410	- Ofisi ya Mkaguzi	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilizungumza juu ya wananchi kupata tabu kwenda kufuatilia taasisi za elimu ya juu kule Bara kama *NECTA.* Hii *NECTA* iliomba kiwanja na iliwahi kutumia shilingi milioni 15 kukiuza kiwanja kile na kiwanja kile kikafutwa.

Vile vile *Open University* imeomba kiwanja hapa ili kujenga majengo yao na kuweza kutoa huduma kwa karibu zaidi kwa wananchi wetu. Namuomba Mhe. Waziri atuambie jitihada zake zimefikia wapi kuhusu taasisi hizi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Taasisi ya Mitihani *(NECTA)* iliomba kiwanja hapa na mimi wakati ule nakaimu Ofisi ya Waziri Kiongozi ndie niliyechukua jukumu la kuwaita hapa na kuwakabidhi hati ya hicho kiwanja kwamba waende wakajenge. Niliwachukua lakini kiwanja kile kilikaa hatukupata majibu kwa muda wa miaka isiyopungua minne mpaka ikawa kama kwamba kile kiwanja hakina mtu.

Matokeo yake Wizara ya Ardhi ikachukua hatua ya kufuta ile hati ambayo waliitoa na badala yake wamewapa watu wengine. Ndio hicho ambacho sasa hivi wamepewa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya kujenga ofisi yao.

Lakini hata hivyo, sisi tumesema hatuchoki hapo tunaendelea na jitihada tena Wizara ya Ardhi kutafuta kiwanja na kwa wema wetu tumekusudia hata tuwamegee kiwanja ambacho tulikuwa tumekitenga kule Tunguu kwa ajili ya Wairan walitaka kujenga pale chuo kikuu lakini hawakujenga tuwape wajenge. Kwa hivyo, tunangojea kamati zikamilike ili tuwape wajenge. Lakini hizi taasisi zijitahidi zinapopewa viwanja zijenge, haiwezi kukaa ardhi tupu tu hivi hivi ikangoja, sisi wenyewe hapa zinafutwa hati zetu. Sasa ikawa mtu anakuja hapa anakaa na kiwanja hujui hata anafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, juzi wamenijia mimi wakanambia kwamba sasa hivi tumeshakuwa tunataka kujenga, nikawaambia kiwanja kimeshafutwa tutafanya nini sasa hivi, tunakutafutieni chengine. Mhe. Mwenyekiti, swali la pili sina habari kwamba *Open University* waliomba kiwanja kama wameshapewa wamenyang'anywa au vipi angenisaidia. Kama ndio kwanza wanaomba hiyo jitihada ya kwangu inaendelea, lakini najua walionyang'anywa walikuwa ni *NECTA*.

Mhe. Mwenyekiti: Je, Mhe. Waziri kiwanja wamenyang'anywa au wanaomba.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nitampa taarifa kwa maandishi Mhe. Waziri na nashukuru sana kwa maelezo yake mazuri na mimi nakupongeza sana kwa kuwa utayafuatilia haya masuala.

Kifungu 1411	Taasisi ya Elimu	54,000,000
Kifungu 1601	Idara ya Mafunzo ya Ualimu	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilihoji juu ya kupungua mno kwa bajeti ya Idara hii ya Mafunzo ya Ualimu. Tukitumia takwimu ambazo ziko pale pale katika ukurasa wa 323 kwenye jumla ya fungu hili ukiona kwamba imetoka milioni 352 mpaka imefika 130 imekuwa ikipungua. Sasa katika majibu yake Mhe. Waziri alinambia kwamba suala hili zimepungua kwa sababu ziko katika maeneo mengine na moja alilotaja lilikuwa ni sehemu ya fedha za michango ya washirika wa maendeleo na kwenye miradi ya maendeleo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba anisaidie tu kwa sababu nimefungua sehemu ya bajeti ya maendeleo huku nimeona mafungu mengine mengi lakini sikuona

fungu lolote linalohusika na Idara ya Mafunzo ya Ualimu wala katika hayo mafungu mengine sikuona kitu ambacho kinahusiana na mradi wa mafunzo ya ualimu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo ya Mhe. Waziri, hili suala la kutwambia kwamba fedha hizi ziko katika sehemu za miradi ya maendeleo, fedha hizi atusaidie ziko wapi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu namna anavyozilinganisha hizi hesabu za fedha na kutaka kuona kwamba kila mahala kunawekwa fedha za kutosha. Ni *spirit* nzuri sana na kwa kweli imetusaidia sana katika msimamo wake huu. Laitani angekuwa katika Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii mambo yangezidi kuwa mazuri zaidi.

Lakini hata hivyo, namwambia tu kwamba fedha zimepungua kutokana na uhaba wa fedha tulizonazo katika mapato yetu. Mhe. Mwenyekiti, mapato yetu ni madogo hatuwezi kukidhi kila kitu tunachokitaka. Lakini hata hivyo, kilio chake nimekisikia na Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima kama kutakuwa kuna mambo ya kugusika katika hii Taasisi ya Mafunzo ya Ualimu ambayo watayaeleza na tutayakubali basi mwaka ujao mambo yatakuwa mazuri *inshaallah*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa uungwana wa Mhe. Waziri na majibu yake fasaha naomba tuendelee.

Kifungu 1601	Idara ya Mafunzo ya Ualimu	130,000,000
Kifungu 1701	Idara ya Elimu na Sekondari	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia nilisema juu ya ukosefu wa hawa wasaidizi wa maabara na kwa mujibu wa fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kwa sababu elimu ya sekondari hasa ndio inapoanza matumizi ya hawa wasaidizi wa maabara. Kwa kuwa wizara ina mpango mzuri sana wa kusifiwa wa kufungua sekondari 10 hivi karibuni. Je, wizara haioni kwamba bila ya kuwasomesha hawa wasaidizi wa maabara hizo maabara zitashughulikiwa vipi na nani watakaozihifadhi, nani watakaozitunza, mbali ya hizo nyengine tulizonazo.

Lakini kabla Mhe. Waziri hajajibu swali langu kuhusu mpango huo nilikuwa namkumbusha kwamba katika mishahara ya wafanyakazi kuna kifungu kinaitwa *Human Resource Development Levy.*

Je, hawajakiona hichi wakachukua wao wakawasomesha hawa wasaidizi wa maabara, au fedha hizi hawajazidai Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na

Mipango ya Maendeleo. Naomba nipate mambo mawili hayo kwa umoja. Kwanza mpango wao wa kusomesha wasaidizi wa maabara ili kuweza kumudu hizo maabara mpya zinazokuja na nyengine zilizopo. Lakini pia namna gani ya kuzitumia hizi *Human Resource Development Levy* wanazokatwa wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba kwa kweli itakuwa watu wa ajabu ikiwa tunaanzisha maabara chungu nzima na tumeitisha tenda vifaa vya maabara halafu tusitafute wahudumu. Kwa kweli jitihada ya wizara yangu ni kuwatafuta wahudumu wa maabara. Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kujibu siku moja hapa kwamba kuna kijana wetu mmoja yuko Nairobi tunataka aje na tumuweke pale *SUZA* asaidie kutoa mafunzo ya wasaidizi wa maabara ili baadae tuanze kuwapata hawa wasaidizi wa maabara katika maabara zetu mbali mbali ambazo tutazianzisha hapa. Mhe. Mwenyekiti, pia nilisema kwamba tuwaombe na baadhi ya walimu wakubali kuja kuifanya kazi hiyo. Huo mpango tunao na tutawasomesha vijana wetu masuala ya utumishi wa maabara.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi kazungumza juu ya *Human Resource Development Levy*. Nataka nimwambie tu kwamba kama ndio ninayoitambua mimi ni *development levy* ambayo tunakusudia kuitumia kwa ajili ya vijana wetu wa mafunzo ya amali. Tunataka tufike hatua vijana wetu wa mafunzo ya amali wakimaliza pale basi tuwakopeshe pesa anayekwenda kununua patasi, chupa ya gesi, spana, ili ziweze kuwasaidia kwa ajili ya kuanzisha miradi yao. Hiyo sasa hivi ndio tuko katika kuifanyia kazi ili tuone kwamba *development levy* ile inakuja moja kwa moja kwenye mafunzo ya amali kama ndio hiyo ninayoitambua mimi. La kama nyengine atanifahamisha yeye Mhe. Mwakilishi. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwamba hili suala ameliona. Lakini tunaomba kwamba bajeti ijayo ajitayarishe vizuri zaidi ikiwa tukipita kwenye maabara za maskuli zinasimamiwa na walimu kwa sababu walimu hawaziwezi maabara lazima wawepo wasaidizi wa maabara. Vyenginevyo tutatumia fedha za wafadhili vibaya na maabara zitamaliza siku mbili tu. Naomba tuendelee.

Kifungu 1701	Idara ya Elimu na Sekondari	160,000,000
Kifungu 2001	Idara ya Mipango na Sera Pemba	70,095,000
Kifungu 2201	Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pemba	8,531,135,000
Kifungu 2301	Idara ya Elimu Pemba	14,365,000
Kifungu 2501	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	10,143,000
Kifungu 2801	Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba	19,884,000

Kifungu 2901 Idara ya Elimu Sekondari Pemba	19,615,000
Kifungu 2902 Idara ya Teknolojia ya Habari	57,000,000
Kifungu 3001 Idara ya Teknolojia ya Habari Pemba	10,000,000
Jumla ya Fungu	**45,308,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 23 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	45,305,054,000
Kifungu 0703 Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar	200,000,000
Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	5,150,000,000
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	100,000,000
Kifungu 1402 Chuo cha Kiislam Pemba	50,000,000
Kifungu 1406 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar	6,105,000,000
Kifungu 1501 Idara ya Mafunzo ya Amali	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kumpongeza tu Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba ndio waziri pekee ambaye katika bajeti yake ya maendeleo kaomba fedha zote matumizi yake kutoka Baraza kupata idhini yake na fedha ambazo zilitolewa kwa ajili ya maendeleo. Naomba nimpongeze sana swahiba. Ahsante. *(Makofi)*

Kifungu 1501 Idara ya Mafunzo ya Amali	400,000,000
Jumla ya Fungu	**57,310,054,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja iamuliwe wale wanaokubali hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012 wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa mashirikiano mazuri kazi ya tangu asubuhi mpaka hivi sasa tumekamilisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na jioni tukijaaliwa tutakuja kumkaribisha Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwa hivyo, tuje mapema ili kuisikiliza hotuba yake. Lakini kabla sijaahirisha nina matangazo mawili. Wenzetu taasisi ya uchapaji wamechapa Katiba zetu za Zanzibar zipo hapo nje wanauza shilingi elfu tano. Kwa hivyo, anayetaka anaweza kwenda kununua. Ni katiba mpya zinazokwenda na wakati ambayo hata yale marekebisho ya 10 pia yamo.

Tangazo la pili tulipewa dodoso na wenzetu wanaofanya mazoezi fulani, sasa dodosi zile tumeshakaa nazo muda mrefu wenyewe wanazitaka ili watimize malengo yao. Kwa hivyo, naomba waliokuwa hawajarejesha jioni wamletee Katibu ili waweze kukabidhiwa wenyewe. Baada ya hayo nawashukuru tena naahirisha kikao hichi hadi saa kumi na moja za jioni.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 7:13 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012.
Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu kuwasilisha Hotuba ya Wizara yangu tukiwa wazima wa afya na tukiwa kwenye hali ya usalama, amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Kupitia Baraza lako tukufu napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambao ulifanyika kwa amani na utulivu. Hii ni uthibitisho kwamba wananchi wa Zanzibar wana imani na uongozi wake ambao kwa kweli umeanza kutoa matumaini kwa wananchi wa Zanzibar kwa kipindi hiki kinachokaribia mwaka mmoja. Jitihada zake zinaonekana wazi na zinalenga katika kuimarisha uwajibikaji na ufanisi katika utendaji wa serikali itayopelekea kuleta maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuendeleza amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, tunampongeza Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Ushindi wake unaonesha kwa dhati imani na upendo walionao wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwake. Ni ushindi unaodhihirisha uwezo mkubwa alionao kuongoza wananchi wake. Aidha, heshima kubwa aliyoijengea Tanzania ndani na nje ni kielelezo cha wazi kwa uongozi wake uliotukuka.

Mhe. Spika, **n**apenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo na kwa mashirikiano wanayotupa katika utekelezaji wa majukumu yetu chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Miongozo yao imesaidia kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili tukufu. Bila ya shaka yoyote, hii inatokana na uzoefu, umahiri na umakini ulionao katika kuliendesha Baraza hili katika misingi ya hekima, busara na uadilifu. Uongozi wako makini katika kuliendesha Baraza hili, umewezesha kutekeleza shughuli za Serikali kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru kipekee Rais Mstaafu wa awamu ya sita Dk. Amani A. Karume kwa kazi ya kupigiwa mfano aliyoifanya miaka 10 ya uongozi wake katika sekta zote. Aidha, pongezi maalum kwa kusimamia na kubadilisha hali ya kisiasa Zanzibar; kurejesha amani, upendo na mshikamano; na kujenga msingi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mazungumzo yao ya mwezi Novemba 2009 na Katibu Mkuu wa CUF ndiyo matokeo ya maelewano haya tunayoyaona ya kujenga Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu inayoongozwa na Mhe. Asha Bakari Makame kwa ushirikiano na maelekezo wanayotoa kwa wizara yangu. Miongozo na ushauri wao kwa masuala yanayohusu wizara yangu naithamini sana kwani ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi ndani ya Baraza hili na nina matumaini makubwa kuwa miongozo na michango watakayoitoa kwa Wizara yangu itasaidia kuimarisha na kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu tuliyojipangia.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kunichagua kwa kipindi cha tatu mfululizo kuwa mwakilishi wao. Naomba waendelee kunichagua kila nitakapowaomba hivyo. Pia napenda kumshukuru Mhe. Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Naahidi kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar kwa uwezo wangu wote Mwenyezi Mungu atakaonijaalia.

Mhe. Spika, Hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imezingatia mipango na mikakati mikuu ya Serikali ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar wa mwaka 2010 - 2015 (MKUZA II), pamoja na Malengo ya Milenia, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015, Sera husika za kisekta na Mpango Mkakati wa Wizara. Haya yote yanalenga katika kuweka mazingira mazuri ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kukuza ajira, kuweka mazingira bora ya kazi ili kupunguza umasikini na kuleta maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Saba imeamua kuunda Wizara maalum ya kusimamia na kuratibu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, ipo haja ya kutoa ufafanuzi ili kila mmoja wetu aweze kuielewa vyema dhana hii ya uwezeshaji. **Kiambatanisho Nambari 1** cha hotuba hii kimetoa ufafanuzi huo ili wajumbe wa Baraza lako hili tukufu la kutunga sheria waweze kuwa na ufahamu mzuri wa dhana hii.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ina jukumu la kusimamia na kuratibu programu zinazolenga katika kukuza ajira na kunyanyua kipato cha wananchi, hususan wale wenye kipato cha chini, ili waweze kumudu maisha yao ya kila siku, na hivyo kuwapunguzia makali ya umasikini. Masuala ya kukuza ajira ni miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele katika mipango mikuu ya kitaifa (Dira 2020 na Mpango wa

Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar) pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, Dira ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni kuwa na jamii ya Wazanzibari yenye fursa za kutosha za ajira na kipato endelevu. Dhamira ya Wizara ni kuwezesha upatikanaji wa ajira zenye heshima na utekelezaji wa programu za uwezeshaji ili kuhakikisha maisha bora kwa wananchi wa Zanzibar.

MALENGO MAKUU YA WIZARA

Mhe. Spika, Wizara kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 imejipangia kutekeleza malengo makuu ambayo yamo katika Mpango Mkakati wa Wizara 2011 – 2014 kama ifuatavyo:

1. Kuendeleza na kutanua programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi;
2. Kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira kwa wananchi;
3. Kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa pamoja na utekelezaji na uratibu wa sera, sheria, mipango na programu; na
4. Kuimarisha uwezo wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2010/2011 NA MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, Kimuundo Wizara hii ina jumla ya Idara saba, Kamisheni moja na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
3. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Idara ya Ushirika;
5. Idara ya Mikopo;
6. Kamisheni ya Kazi;
7. Idara ya Ajira;
8. Idara ya Usalama na Afya Kazini; na
9. Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, kutokana na uundwaji upya wa Wizara hii zipo Idara ambazo ni mpya kabisa na pia zipo Idara za zamani ambazo zimerithiwa kutoka katika Wizara zilizokuwepo kabla. Idara zilizorithiwa ni Idara ya Ushirika ambayo

ilikuwa chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira pamoja na Kamisheni ya Kazi na Idara ya Mfuko wa Kujitegemea (ambayo kwa sasa inaitwa Idara ya Mikopo) ambazo kwa pamoja zilikuwa chini ya iliyokuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Hivyo, utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 kwa idara ambazo ni mpya utaanzia pale zilipoundwa mwezi wa Januari 2011 hadi Juni 2011.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ndio kiungo kikuu cha uendeshaji wa shughuli za Wizara, jukumu lake la msingi likiwa ni kuratibu uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo, pamoja na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake. Hii ni pamoja na kuratibu tafiti mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu zitakazosaidia katika uandaaji wa mipango na utoaji wa maamuzi sahihi kuhusiana na majukumu ya msingi ya Wizara.

Idara hii pia ina jukumu la kuratibu mahusiano na washirika wa maendeleo; uingizwaji wa masuala mtambuka yakiwemo UKIMWI, jinsia, utawala bora, mazingira, masuala yanayohusu watu wenye ulemavu na mengineyo, katika mipango na shughuli za kila siku za Wizara; na uandaaji taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kuwasilisha kwenye mamlaka husika, zikiwemo taasisi mbalimbali za Serikali.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka uliopita wa 2010/2011, Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Wizara; na

2. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara imekuwa ikiratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Mashirika ya Umoja wa Mataifa kwa nguzo ya kwanza (JP5). Programu hii iliyoanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwezi wa Mei, 2008 ililenga kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umasikini kwa njia ya kuongeza ajira, kujenga uwezo kwa taasisi za Serikali na Binafsi katika kutekeleza sheria za kazi, kutoa mafunzo kwa

wajasiriamali, kuweka mfumo imara wa hifadhi ya jamii kwa wote nchini na kujenga uwezo kwa taasisi husika katika utekelezaji wa Sera ya Ajira na Mpango wa Kukuza Ajira kwa Vijana. Programu hii imemalizika rasmi mwezi wa Juni 2011.

Mhe. Spika, Programu imetekeleza shughuli zifuatazo:

- Imekamilisha ujenzi wa Kituo cha kutoa taarifa kwa waomba kazi na wajasiriamali. Kituo hicho kimepatiwa vifaa muhimu vikiwemo kompyuta na samani za ofisi. Kitakapoanza kufanya kazi rasmi, kituo hichi kitawawezesha vijana na wajasiriamali kufahamu fursa za ajira zilizopo ndani na nje ya nchi ili waweze kuomba nafasi hizo na kupata ajira.

  Aidha, kitawasaidia wajasiriamali kutambua fursa za masoko kwa bidhaa wanazozalisha, kutangaza na kuuza bidhaa zao kirahisi kwa njia ya kisasa kupitia mtandao. Pia Kitengo cha Kutoa Taarifa za Soko la Ajira kimeanzishwa na kimepatiwa vyombo vya usafiri na vifaa vya kufanyia kazi. Jumla ya vespa tatu zimenunuliwa kwa ajili ya kitengo hicho na watendaji sita (wanaume 3, wanawake 3), wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa kitengo hicho.

- Kupitia Progaramu hii Kanuni mbili za sheria ya Uhusiano Kazini Nambari 1 ya mwaka 2005 zimekamilika. Kanuni moja inahusiana na

  usuluhishi na utatuzi wa migogoro na ya pili inahusu Kamati ya Utatu. Kukamilika kwa kanuni hizi kutasaidia kuweka mazingira mazuri katika utatuzi wa migogoro ya kazi.

- Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Kazi umetayarishwa. Mpango huo ndio dira ya kutekeleza shughuli mbali mbali zinazohusu masuala ya ajira na kazi nchini. Kuwepo kwa mpango huo kutasaidia kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Ajira nchini na kutekeleza kwa ufanisi Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini. Sambamba na mpango huo, pia Mpango Mkakati wa Wizara umetayarishwa ambao ni dira ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Mpango huu utaiwezesha Wizara kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake kuhusiana na usimamizi wa masuala ya kazi; ukuzaji wa ajira zenye heshima; uendelezaji na uratibu wa programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi; utoaji mikopo na uimarishaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, Wizara imeandaa miradi mikubwa miwili kwa lengo la kutekeleza Sera ya Ajira na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar. Mmoja kati ya miradi hiyo unalenga kuijengea uwezo Wizara katika kutekeleza shughuli zake ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi na kuwapatia mafunzo wafanyakazi, pamoja na kuweka mazingira ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, ikiwemo kuanzisha vituo vya kuendeleza ujuzi na mbinu mbalimbali za uzalishaji zitakazosaidia wananchi kujiajiri na kuleta ufanisi na tija zaidi katika shughuli zao za uzalishaji na ujasiriamali.

Mradi wa pili unalenga kuwawezesha wananchi kupitia mafunzo ya ujasiriamali; kuongeza ajira au uwezo wa kujiajiri kupitia fursa za mikopo nafuu; kuwajengea ubunifu katika biashara zao ili waweze kuhimili ushindani na kupanua soko la bidhaa zao; na kunyanyua uwezo wao wa kutumia teknolojia bora ya uzalishaji. Utekelezaji wa miradi hii unategemea kuanza rasmi mara tu baada ya upatikanaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo na Serikali.

Malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Wizara;

2. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar;

3. Kuimarisha mfumo wa uratibu, tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Wizara;

4. Kuratibu utayarishaji wa Sera na tafiti kuhusiana na masuala mbalimbali kulingana na majukumu ya Wizara; na

5. Kuhakikisha masuala mtambuka yanazingatiwa katika shughuli za Wizara.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Mipango,Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Tano (T.Shs.75,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi zikiwemo sheria na kanuni za utumishi, mafunzo, maslahi na maendeleo ya wafanyakazi kwa jumla kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Pia Idara hii ina jukumu la kuandaa mazingira bora yatakayorahisisha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha Idara inaratibu shughuli mbalimbali za kitengo cha Ofisi ya Waziri. Kwa mwaka 2010/2011 Idara ilipangiwa kutekeleza yafuatayo:

1.) Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi watendaji wa Wizara ili kuwaongezea uwezo na ujuzi wa kazi zao; na

2.) Kukiimarisha kitengo cha habari ili kuendelea kukusanya habari na kutoa taarifa za maendeleo ya wizara.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara imetekeleza yafuatayo:

- Imewapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi wafanyakazi 20 katika fani mbali mbali za kitaaluma. Kati ya wafanyakazi hao kumi (10) ni wanawake na kumi (10) ni wanaume kama inavyoonekana katika **Kiambatanisho Nambari 2;**
- Imesimamia zoezi la uchambuzi wa mahitaji ya ujengaji uwezo wa Wizara na uandaaji wa Mpango wa Kujenga Uwezo;
- Imesimamia uundwaji wa Kamati za Wizara zilizoainishwa kwenye sheria mbali mbali. Pia imesimamia uundwaji wa Kamati ya Michezo ya Wizara. Kamati hii itasimamia kuwepo kwa michezo tofauti ili kujenga afya za wafanyakazi. Aidha, kupitia michezo, Wizara na vitengo vyake itaweza kufikisha ujumbe kwa wananchi Unguja na Pemba kuhusu dhana nzima ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;
- Imeratibu utayarishaji wa muundo wa Wizara; na
- Katika kuzingatia masuala mtambuka, viongozi wa Wizara na wafanyakazi kwa kushirikiana na uongozi wa Shehia ya Melinne walishiriki kufanya usafi na kupanda miti katika eneo la ofisi, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Ofisi ya Waziri

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Ofisi ya Waziri imepokea wageni kutoka nchi, taasisi na mashirika mbali mbali ikiwemo Jamhuri ya Czech, Slovakia, Oman, Marekani, India, China, Misri, Iran, Benki ya Dunia, British Council, Shirika la Kazi Duniani, South Caroline State University, Youth Microfinance Bank na Zantel. Pia imepokea ujumbe wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi, Jumuiya ya Waajiri, Baraza la Watu Wenye Ulemavu na Jumuiya ya Wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Zanzibar .

Aidha, Mheshimiwa Waziri amefanya ziara na kuhudhuria mikutano katika nchi za Qatar, Burundi, Oman, *UAE*, Uswizi na Equitorial Guinea kwa lengo la kujifunza ili kuijengea wizara uwezo zaidi. Ziara hizo zinategemewa kuleta mafanikio mazuri ya kuwapatia vijana ajira na misaada mbali mbali.

Malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kujenga uwezo wa utendaji kwa kusimamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi kulingana na kazi wanazozifanya;

2. Kuimarisha na kujenga mazingira mazuri ya kazi;

3. Kukiimarisha Kitengo cha Habari na Mawasiliano ili kiweze kutekeleza vyema majukumu yake;

4. Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na mahusiano mema kazini; na

5. Kuratibu na kusimamia kitengo cha Ofisi ya Waziri kwa kuendeleza na kuimarisha mahusiano na mashirikiano ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Themanini na Mbili (T.Shs. 382,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UENDELEZAJI NA URATIBU WA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, Idara hii ni mpya na ina jukumu la kubuni programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kutafuta nyenzo kwa ajili ya programu hizo.

Pia Idara hii ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini programu za uwezeshaji, ikiwemo kufanya tafiti ili kubaini hali halisi juu ya programu za uwezeshaji, maeneo mapya yanayoweza kutoa fursa za kuwawezesha wananchi kiuchumi, hali ya masoko pamoja na kuwezesha upatikanaji wa taarifa zitakazosaidia kupanga mipango mbalimbali ya uwezeshaji wananchi.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara imetekeleza yafuatayo:

- Imetayarisha dodoso la kukusanya taarifa zitakazowezesha kufahamu vikundi vya ujasiriamali vilivyopo, shughuli wanazozifanya na ujuzi walionao katika kutekeleza shughuli zao. Ufahamu huu utakuwa kigezo cha kupanga na kupima utekelezaji wa mipango ya uwezeshaji kupitia programu mbalimbali;
- Imefanya ziara ya kutembelea vikundi vya wananchi vilivyowezeshwa kitaaluma kupitia miradi ya ASSP na ASPD-L chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Ziara hii imeonesha kuwa wananchi wakiwezeshwa kitaaluma wanaweza kujikomboa kutoka kwenye umasikini; na
- Imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi 30 wa Unguja kwa kuanzia ili waweze kufanya biashara kwa umahiri.

Malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kufanya uchambuzi wa mahitaji ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;
2. Kupanga na kuendesha mafunzo ya kuongeza ujuzi wa ujasiriamali;
3. Kutayarisha Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kuandaa na kuendesha Mikutano ya Kamati za Uwezeshaji za Wilaya na Taifa;
5. Kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kufanya tafiti katika maeneo muhimu ya kiuchumi ili kubaini fursa zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi;

6. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi ili waweze kupanga, kuratibu na kusimamia vyema programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi; na
7. Kuandaa mapendekezo ya miradi ili kutafuta rasilimali fedha na misaada ya kitaalamu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja (T.Shs. 100,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIKOPO

Mhe. Spika, Idara hii hapo kabla ilijulikana kama Idara ya Mfuko wa Kujitegemea; ina jukumu la kusimamia utoaji mikopo nafuu ili kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umasikini. Lengo ni kuwawezesha wananchi waweze kujiajiri na kujipatia kipato halali na endelevu ili kumudu maisha yao.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia utekelezaji wa sera, kanuni na miongozo ya utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuzingatia ukuaji wa ajira kijinsia ili kuimarisha mifuko kuwa endelevu;

2. Kuendelea kuratibu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (JK/AK) kupitia mikopo yenye masharti nafuu na kuongeza ajira;
3. Kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja na Ishirini (T.Shs.120,000,000/=) kwa wananchi wasiokuwa na ajira wenye uwezo wa kufanya kazi kupitia Mfuko wa Kujitegemea;

4. Kuendelea kutoa mafunzo ya upatikanaji na matumizi bora ya mikopo, ujasiriamali, ufundi stadi, uzalishaji mali na kujikinga na maambukizo ya UKIMWI kwa wateja;
5. Kuimarisha utendaji kazi wa Idara; na

6. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa katika kuwanyanyua wajasiriamali nchini.

Mhe. Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (JK/AK) unaendeshwa na Benki ya Watu wa Zanzibar na utekelezaji wake unahusisha Kamati za Uratibu za Wilaya/Shehia. Wizara ina jukumu la kuratibu na

kufuatilia ili kuona kuwa lengo kuu la Mfuko huu la kuwawezesha wananchi kiuchumi linatekelezwa ipasavyo.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mikopo

Mhe. Spika, Katika kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa malengo ya Mfuko wa JK/AK, shughuli za uratibu zifuatazo zilitekelezwa kwenye kipindi cha mwaka 2010/2011:

- Wizara iliitisha Kikao cha Kamati ya Kisekta ya Kusimamia Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Mfuko wa JK/AK ambacho, pamoja na mambo mengine, kilitoa maelekezo juu ya kuimarisha usimamizi wa Mfuko huo ikiwa pamoja na suala zima la kukabiliana na changamoto zilizopo katika marejesho ya mikopo;

- Wajasiriamali wa Shehia zote 52 za Unguja na Pemba zilizopata fursa ya mkopo wa Mfuko wa JK/AK wametembelewa kwa madhumuni ya kuhamasishwa juu ya urejeshaji wa mikopo;

- Idara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na Benki ya Watu wa Zanzibar imefanya mikutano miwili (Unguja na Pemba) ya kutathmini uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (JK/AK). Mikutano hiyo ilishirikisha Kamati za Uratibu za Wilaya, baadhi ya wakopaji na masheha; na ilijadili masuala mbalimbali ikiwemo changamoto za urejeshaji wa mikopo. Kupitia mikutano hiyo maoni mbalimbali yalitolewa ya kusaidia kuimarisha utoaji na urejeshaji wa mikopo;

Mhe. Spika, Kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (JK/AK), hadi kufikia mwezi wa Mei 2011, jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Sitini na Tatu, Laki Sita Arobaini Elfu (Tshs. 1,463,640,000/=) zimetolewa kwa watu binafsi 660, vikundi 58 na SACCOS 10 Unguja na Pemba. Kati ya hizo, Unguja zimetolewa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Kumi na Mbili, Laki Nne na Ishirini Elfu (T.Shs. 1,012,420,000/=) na Pemba Shilingi Milioni Mia Nne na Hamsini na Moja, Laki Mbili na Ishirini Elfu (T.Shs. 451,220,000/=). Miongoni mwa watu binafsi waliopatiwa mikopo, 267 ni wanawake (Unguja 215 na Pemba 52) na 393 ni wanaume (Unguja 241 na Pemba 152).

Aidha, marejesho ya mikopo kwa Mfuko wa JK/ AK ni Shilingi Milioni Mia Sita na Tisa, Laki Mbili Hamsini na Sita, Mia Sita na Kumi na Senti Sabini na Tano (T.Shs. 609,256,610.75). Kati ya hizo Unguja ni Milioni Mia Nne Kumi na Tisa, Laki Tano Tisini na Nne, Mia Sita Tisini na Nane, Senti Sabini na

Tano (T.Shs. 419,594,698.75) sawa na asilimia 69 na Pemba ni Shilingi Milioni Mia Moja Themanini na Tisa, Laki Sita Sitini na Moja, Mia Tisa na Kumi na Mbili (T.Shs. 189,661,912/=) sawa na asilimia 31 kama inavyoonekana katika **Viambatanisho Nambari 3a, 3b na 3c marejesho ya JK/AK.**

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Mikopo kupitia Mfuko wa Kujitegemea imetoa mikopo yenye thamani ya jumla ya Shilingi Milioni Thamanini na Tatu na Laki Nane (T.Shs. 83,800,000/=). Kati ya hizo, jumla ya Shilingi Milioni Arobaini na Nane na Laki Saba (T.Shs. 48,700,000/=) zimetolewa kwa Unguja na Shilingi Milioni Thelathini na Tano na Laki Moja (T.Shs. 35,100,000/=) zimetolewa kwa upande wa Pemba kama inavyoonekana kwenye **Kiambatanisho Nambari 4a.**

Aidha, fedha za marejesho ya mikopo zilizokusanywa ni Shilingi Milioni Thamanini na Tatu, Ishirini na Nane Elfu, Mia Mbili Hamsini (T. Shs. 83,028,250/=). Kati ya hizo Unguja ni Shilingi Milioni Hamsini na Tano, Laki Moja ishirini na Nane, Mia Mbili Hamsini (T.Shs. 55,128,250/=) ambazo ni sawa na asilimia 66 na kwa Pemba ni Shilingi Milioni Ishirini na Saba na Laki Tisa (T.Shs. 27,900,000/=) ambazo ni sawa na asilimia 34 kama inavyoonekana katika **Kiambatanisho Nambari 4b.**

Mhe. Spika, Idara ya Mikopo hutoa mafunzo yanayoelezea njia na taratibu za kuweza kupata mikopo pamoja na uandishi wa barua. Mafunzo haya hutolewa kabla na baada ya kutolewa mkopo. Katika kutoa mafunzo hayo muongozo maalumu hufuatwa. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 mafunzo yametolewa kwa wananchi 80, ikiwa Unguja 53 na Pemba 27. Mada kuu za mafunzo hayo ilikuwa ni pamoja na taratibu za uombaji na urejeshaji wa mikopo.

Mhe. Spika, Katika kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa ili kuwanyanyua Wajasiriamali, Idara imeshiriki katika matayarisho ya maonesho ya Afrika Mashariki ya JUA KALI /NGUVU KAZI, yaliyofanyika Arusha na Dar es salaam. Jumla ya wajasiriamali 28 kutoka Zanzibar walishiriki katika maonesho hayo.

Mhe. Spika, Idara imeratibu ziara ya Wabunge 14 kutoka Bunge la Norway ambao walitembelea Zanzibar. Wabunge hao pamoja na watendaji wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) waliwatembelea wajasiriamali katika maeneo yao ya kazi na baadae kuangalia maonesho yaliyofanyika Beit el Ajaib, Forodhani. Ziara hiyo ya Wabunge wa Norway ilifanywa kwa ajili ya kufuatilia shughuli za vikundi mbali mbali vilivyonufaika na misaada ya Shirika la Kazi Duniani. Vikundi hivyo ni Amani na Utulivu, Waridi *SACCOS*, *ZAPHA+*, Kikundi cha

Watu Wenye Ulemavu, *ZASPO*, *AMISUFI*, *AZZHAV* na *Nia Safi Women Group.*

MALENGO YA IDARA YA MIKOPO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, Katika kipindi cha 2011/2012, idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na kutoa mikopo ipatayo 1,000 (kutegemeana na upatikanaji wa fedha) kwa mwaka kwa kuzingatia ukuaji wa ajira kwa makundi yote;
2. Kusimamia na kufuatilia marejesho ya mikopo kwa wakati uliopangwa, ili kwenda sambamba na malengo ya mikopo ya uwezeshaji kwa kukuza ajira nchini;

3. Kuanzisha maeneo mapya ya ukopaji, kuhakikisha taratibu za mikopo zinakuwa bora zaidi, mikopo inatolewa kwa wakati na kushirikiana na asasi nyengine katika kuimarisha huduma kwa wakopaji;

4. Kutunisha Mfuko wa Uwezeshaji kwa kuhamasisha wenye uwezo kuchangia, ili kuongeza utoaji wa mikopo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi;

5. Kuimarisha utendaji kazi wa Idara kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi; na

6. Kuendeleza mashirikiano na taasisi za kitaifa na kimataifa katika kuwaimarisha walengwa pamoja na kuangalia namna bora za kuongeza uwezo wa kifedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mikopo iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya shilingi 110,000,000/= kwa matumizi ya kawaida ikiwemo na mishahara.

IDARA YA USHIRIKA

Mhe. Spika, idara hii ina jukumu la kuihamasisha jamii, kusimamia uundwaji wa Vyama imara vya Ushirika, kuviendeleza na kuvijengea uwezo. Pia Idara ya Ushirika ina jukumu la kuimarisha mashirikiano na taasisi mbali mbali na kufanya utafiti, ili kupata taarifa za kuandaa mipango ya kimaendeleo kwenye Sekta ya Ushirika.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Ushirika ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuhamasisha na kusimamia uundwaji wa vyama vya ushirika 171 Unguja na Pemba;

2. Kukagua mahesabu ya Vyama vya Ushirika 150 na kuchunguza maendeleo ya vyama 1,500;

3. Kuendeleza na kujenga uwezo wa vyama 120 kwa mafunzo na huduma za kiutaalamu;

4. Kujenga uwezo wa idara na watendaji kwa kuwapa mafunzo na vitendea kazi;

5. Kukusanya mapato ya shilingi 4,000,000/=; na

6. Kukamilisha utayarishaji wa sera ya Maendeleo ya Ushirika.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ushirika:

Mhe. Spika, Jumla ya Vyama vya Ushirika 177 (84 Unguja; 93 Pemba) vimesajiliwa. Lengo lilikuwa ni kusajili vyama 171. Kiwango cha utekelezaji wa zoezi la usajili ni asilimia 103, yaani tumevuka lengo Mhe. Spika. Vyama vilivyosajiliwa vimejumuisha vya huduma na miradi mbali mbali ya kiuchumi, vyama vya uzalishaji, kazi za mikono, *SACCOS*, na vyama vya kilimo na ufugaji. Utekelezaji huu umeongeza takwimu na idadi ya vyama mbali mbali vilivyo sajiliwa kufikia 5,581.

Mhe. Spika, Jumla ya vyama 107 (Unguja 47, Pemba 60) vimepatiwa huduma ya ukaguzi wa mahesabu. Zoezi hilo la ukaguzi limehusisha pamoja na kutoa maoni huru juu ya hali ya kifedha na hali ya maslahi ya wanachama kwa vyama vilivyokaguliwa. Maoni ya ujumla ya ukaguzi huo yameonesha maendeleo, ukuaji wa mitaji ya vyama na kuongezeka kiwango cha utawala bora kwenye vyama hivyo kama inavyoonekana katika *Kimbatanisho Nambari 5*.

Mhe. Spika, jumla ya vyama 422 vimefanyiwa upekuzi hadi kufikia mwezi Mei 2011; kati ya hivyo Unguja ni 234 na Pemba 188. Upekuzi huo umelenga kubaini na kuona mafanikio yaliyopatikana kwenye vyama katika utunzaji wa mahesabu na kumbukumbu mbali mbali, uendeshaji wa vikao na ushiriki wa viongozi na wanachama kwenye shughuli za ushirika wao pamoja na

changamoto zinazovikabili vyama hivyo. Matokeo ya upekuzi kwa jumla yameonesha kuwepo kwa maendeleo yanayoridhisha.

Hata hivyo changamoto kwenye utaalamu wa uongozi na uendeshaji, mitaji dhaifu ya vyama na hamasa ndogo ya wanachama na viongozi bado zipo kwenye vyama vingi vilivyopitiwa. Hatua za utoaji elimu na mafunzo kurekebisha kasoro hizo zimeanza kuchukuliwa.

Mhe. Spika, jumla ya vyama 204 vilipatiwa mafunzo ya uongozi wa vyama vya ushirika. Mafunzo hayo yalitolewa kwa viongozi na wanaushirika 8,002 (Wanaume 2,641 na Wanawake 5,361) kwa Unguja na Pemba. Mada zilizofundishwa zilijumuisha dhana, falsafa na kanuni za ushirika, uanzishaji na uendeshaji wa vyama, uwekaji wa kumbukumbu za vikao na utunzaji wa mahesabu ya vyama.

Idara imefanya ufuatiliaji, ili kujua athari ya mafunzo na matokeo ya tathmini hiyo imeonesha maendeleo mazuri. Viongozi wameweza kuyatumia mafunzo hayo kwa kiasi kikubwa, ambapo wengi wanaendeleza utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu na uandishi wa kumbukumbu za mikutano.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB* Tawi la Zanzibar iliendesha mpango wa kuimarisha vyama vya Akiba na Mikopo kuviwezesha kutoa huduma za kibenki '*SACCOS Banks'*. Lengo lilikuwa ni kuanzisha "*SACCOS Banks*" 14 kwa Unguja na Pemba. Matokeo ni kwamba jumla ya "*SACCOS Banks*" 11 zimeanzishwa na kuzinduliwa, sawa na asilimia 79 ya lengo.

Aidha uwezo wa utoaji mikopo wa "*SACCOS Banks*" hizo umeongezeka hadi kufikia shilingi bilioni tatu, milioni thelathini na nne, elfu sita, mia sita arobaini na nane (3,034,006,648/=) ya mikopo iliyo mikononi mwa wanachama wakopaji. Kati ya fedha hizo benki ya *CRDB* imechangia shilingi bilioni mbili, milioni mia moja sitini na saba, laki sita hamsini elfu (2,167,650,000/=) ambayo ni sawa na asilimia 71.4. Ripoti za awali za ufuatiliaji zimeonesha "*SACCOS Banks*" tisa (9) zimeweza kusimamia urejeshaji wa mikopo kwa kiwango kinachokubalika na "*SACCOS Banks*" mbili hazijafanya vyema kwenye urejeshaji wa mikopo.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika imeimarisha mashirikiano na taasisi mbali mbali zikiwemo Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kwa lengo la kuimarisha Sekta ya Ushirika Zanzibar. Kupitia mashirikiano hayo, *ILO* imeisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuandaa Sera ya Maendeleo ya Ushirika, kufanya mapitio ya Sheria Namba 4 ya mwaka 1986 inayoongoza shughuli za ushirika Zanzibar

pamoja na kusaidia kuandaa kanuni za uendeshaji (*Cooperative Regulations*). Nyaraka zote hizo ni nyenzo muhimu za kuongoza na kuelekeza taratibu za uendeshaji shughuli za ushirika nchini, kuleta ufanisi wa vyama vya ushirika, kuimarisha utoaji huduma na tija kwa wanachama kwa kuongeza vipato vyao na hatimae kuwapunguzia umasikini.

Mhe. Spika, idara kwa kushirikiana na *ILO* pia imeanza kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji taarifa kwa kutumia teknolojia ya kompyuta. Mfumo wa kuhifadhi taarifa (*database*) zinazoonesha mahitaji mbali mbali na uwezo uliopo kwenye sekta ya ushirika, unaandaliwa na utaanza kutumika mara tu baada ya kukamilisha taratibu za kiufundi. Hatua hii itasaidia kutambua mchango halisi wa sekta ya ushirika katika kuongeza ajira, kipato na kupunguza umaskini.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kulishukuru kwa dhati Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kwa misaada mbali mbali wanayotupa ikiwemo vifaa na utaalamu. *(Makofi)*

Malengo ya Idara ya Ushirika kwa Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2011/2012, idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuanzisha nafasi 3,500 za ajira kupitia Sekta ya Ushirika;

2. Kukamilisha taratibu za kuidhinisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria, kanuni na sheria ndogo ndogo za Vyama vya Ushirika;

3. Kusimamia usajili wa Vyama vya Ushirika 175;

4. Kukagua mahesabu ya vyama vya Ushirika 150 na kuanzisha Taasisi ya Ukaguzi inayojitegemea;

5. Kufuatilia na kuvipatia ushauri wa kitaalamu Vyama vya Ushirika 2,000;

6. Kutoa mafunzo kwa wanachama na viongozi 3,000, kutoka Vyama vya Ushirika 400;

7. Kuanzisha "*SACCOS Banks*" 14 na kuimarisha zilizopo; na

8. Kuendeleza mashirikiano na taasisi mbali mbali ili kusukuma maendeleo ya Sekta ya Ushirika.

Mhe. Spika, ili Idara ya Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 73,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 40,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

KAMISHENI YA KAZI

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi ina jukumu kubwa la kuratibu na kusimamia masuala yote ya kazi na ajira katika Sekta za Umma na Binafsi nchini.
Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kamisheni ya Kazi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Ajira kwa kufanyia marekebisho baadhi ya sheria za kazi, pamoja na kuanzisha na kuzijengea uwezo Kamati za kisekta za kukuza ajira katika Mikoa na Wilaya;

2. Kuanza mchakato wa kutayarisha Sera ya Hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na washirika wengine;

3. Kuimarisha masuala ya utatu na kuongeza uwezo wa wafanyakazi na waajiri kuhusu majadiliano ya pamoja sehemu za kazi;

4. Kuziimarisha na kuziendeleza taasisi za kazi;

5. Kuimarisha masuala ya usalama na afya sehemu za kazi;
6. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza Ajira za Watoto;

7. Kuimarisha ukaguzi na kusimamia sheria za kazi pamoja na uundwaji wa kanuni za sheria za kazi; na

8. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Kazi za Tanzania Bara pamoja na kukuza ushiriki katika mikutano ya Kimataifa, Kikanda na Afrika Mashariki.

Utekelezaji wa Malengo ya Kamisheni ya Kazi:

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kamisheni ya Kazi imewapatia maafisa watatu mafunzo ya msingi katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhusu namna bora ya kukusanya taarifa za ajira, ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri. Lengo ni kukiwezesha Kituo cha Kutoa Taarifa za Ajira kwa wanaotafuta kazi kifanye kazi kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi katika kuendeleza mashirikiano na taasisi za kazi za Tanzania Bara pamoja na kukuza ushiriki katika mikutano ya Kimataifa, Kikanda na Afrika Mashariki imetekeleza mambo yafuatayo:-

- Maafisa wanne wa Kamisheni ya Kazi wameshiriki katika mikutano minne iliyoandaliwa na Jumuia ya Afrika Mashariki; ikiwemo ile iliyohusu majadiliano juu ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Aidha maafisa wawili walishiriki katika mikutano miwili iliyoandaliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu masuala ya kazi na ajira;

- Maafisa watatu wameshiriki katika mkutano ulioandaliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mkutano huo ulikusanya maoni yatakayosaidia kufanya mapitio katika baadhi ya Sheria za Tanzania (Sheria ya Ardhi na Sheria ya Kazi), ili kuondoa kasoro zilizopo kwa kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki;

- Maafisa wawili wa Kamisheni ya Kazi wameshiriki katika kikao kilichoandaliwa na Shirika la Kazi Duniani kilichojadili maeneo ya vipaumbele yatakayozingatiwa kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza Mpango wa Pili wa Tanzania kuhusu Kazi za Heshima. Utekelezaji wa mpango huu utasaidia kuhakikisha kuwa wazalendo wanafanya kazi zenye heshima na zinazokubalika;
- Afisa mmoja wa Kamisheni ya Kazi ameshiriki katika mkutano wa uzinduzi wa mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Ajira na kuwawezesha wazalishaji wadogo wadogo hasa wanawake na vijana, ili kufikia kazi za heshima. Mkutano huo uliandaliwa na Shirika la Chakula Duniani (*FAO*);

- Waziri, Kamishna wa Kazi na mjumbe mmoja kutoka Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi walishiriki katika Mkutano Mkuu wa kila mwaka wa Shirika la Kazi Duniani huko Geneva,

ambao ndio unaojadili na kupitisha maazimio juu ya taratibu mbali mbali kuhusiana na Sekta ya Kazi.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Kamisheni ya Kazi katika kuimarisha kitengo cha usuluhishi wa migogoro ya kazi, usalama na afya kazini na Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, imetekeleza mambo yafuatayo:-

- Imewapatia mafunzo maafisa wa Kitengo cha Usuluhishi na Utatuzi wa Migogoro ya kazi juu ya uwekaji wa kumbukumbu za migogoro ya kikazi kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) chini ya mradi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi; na

- Imesajili chama kimoja kipya "*Association of Public Sector Unions" (APSU).* Aidha Kamisheni ya kazi imefanya ukaguzi wa vyama 16 na kutoa ushauri, ili vifanye shughuli zao vizuri zaidi na kuwasaidia wafanyakazi na waajiri katika masuala yao ya kazi pamoja na kuishauri serikali kupitia vikao mbali mbali vilivyoundwa kisheria; kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Nambari 6.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Kamisheni ya Kazi kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani, ilifanya utafiti wa kuangalia hali halisi ya mishahara katika taasisi mbali mbali za kazi. Rasimu ya ripoti ya utafiti huo imekamilika na imewasilishwa kwa wahusika wa masuala ya kazi kwa kutoa maoni yao. Hivi sasa wataalamu wanaendelea na kazi ya kuweka mapendekezo ya wahusika hao, ili kuiwasilisha kwa kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi imeanza mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria ya Ajira Nambari 11 ya mwaka 2005 kwa kuainisha maeneo yenye kasoro, ili yarekebishwe. Maeneo hayo ni pamoja na;

- Utaratibu wa fursa za ajira kwa wageni wanaooa au kuolewa na wazalendo; *(Makofi)*

- Utaratibu wa wakala binafsi katika kushughulikia ajira kwa wananchi wanaotafuta kazi ndani na nje ya nchi; *(Makofi)*

- Utaratibu wa kuwafahamu wazalendo wanaofanya kazi nje ya nchi na kuwa na taarifa zao zinazohusiana na ajira na mikataba yao; na

- Eneo linalohusu aina za kazi na mikataba ya kazi ya muda mfupi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha masuala ya usalama na afya kazini, wakaguzi kazi watatu na mkaguzi mmoja wa usalama na afya sehemu za kazi walipatiwa mafunzo maalumu juu ya njia bora za kufanya ukaguzi, yaliyofanyika Dar es Salaam na kuendeshwa na Shirika la Kazi Duniani. Pia afisa mmoja wa Idara ya Usalama na Afya kazini alipatiwa mafunzo ya usalama na afya kazini katika Chuo cha Shirika la Kazi Duniani, Turin nchini Italia.

Mhe. Spika, katika kuendeleza ukaguzi kwa kusimamia Sheria za Kazi na utayarishaji wa Kanuni za Kazi, Kamisheni imetekeleza mambo yafuatayo:-

- Imezikagua taasisi 79 za kazi Unguja na Pemba kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria za Kazi. Katika ukaguzi huo zimeonekana kasoro katika mikataba ya wafanyakazi na haki zao pamoja na kutokuwepo kwa vifaa vya kinga na usalama. Maelekezo yalitolewa ili kurekebisha kasoro hizo;
- Imetoa elimu juu ya Sheria za kazi. Jumla ya vipindi viwili vimekuwa vikirushwa hewani kwa mwezi kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar na kurejewa mara mbili. Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa mashirikiano yao makubwa ambayo wanatupa wizarani kwetu. Aidha taasisi 15 zilipatiwa taaluma juu ya elimu ya sheria za kazi na utekelezaji wake, ili waajiri na wafanyakazi waweze kutekeleza majukumu na wajibu wao ipasavyo. Maelezo zaidi yanapatikana katika Kiambatanisho Nambari 7;

- Maafisa Kazi sita (wanawake 2 na wanaume 4) walipatiwa mafunzo maalum juu ya uandishi wa ripoti za utekelezaji wa mikataba ya Shirika la Kazi Duniani. Mafunzo hayo yaliyofanyika Morogoro yaliendeshwa na Shirika la Kazi Duniani; na
- Kanuni mbili za Sheria za Kazi zinazohusu usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya kazi na Kamati ya Utatu zimetayarishwa na zinaendelea na taratibu za kisheria ili ziweze kutumika.

Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Kamisheni ya Kazi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuzipitia baadhi ya Sheria za Kazi za Zanzibar, ili zikidhi mahitaji;

2. Kuendelea kutoa elimu juu ya sheria na kanuni za kazi na miongozo ya kazi;

3. Kuimarisha Vitengo vya Kamisheni ya Kazi;

4. Kuimarisha masuala ya Utatu na majadiliano ya pamoja sehemu za kazi;

5. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa zinazohusiana na masuala ya kazi pamoja na kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kitaifa na kimataifa yanayohusiana na Sekta ya Kazi.

Mhe. Spika, ili Kamisheni ya Kazi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 110,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 50,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA AJIRA

Mhe. Spika, idara hii ni mpya na ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ajira, Mpango wa Kuzalisha Ajira, pamoja na kubuni na kusimamia mipango na taratibu za soko la ajira, zitakazohakikisha fursa za ajira zinapatikana kwa usawa na kwa watu wote wanaohitaji.

Pia idara ina jukumu la kufanya tafiti kwa ajili ya kuendeleza sera, mikakati na mipango mbali mbali ya ajira; kuanzisha na kusimamia mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na uwekaji wa taarifa za soko la ajira; na kusimamia ajira kwa wataalamu wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11 idara hii imefanya yafuatayo:-

- Imefanya semina ya kuhamasisha jamii katika Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja juu ya kutumia fursa za ajira katika sekta ya utalii;
- Imefanya warsha kwa wahusika mbali mbali kuhusu uanzishwaji wa Kamati za Mikoa na Wilaya za Kuzalisha Ajira kwa Unguja na Pemba; na

- Kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa husika, idara imefanya uzinduzi na imetoa mafunzo kwa kamati za kuzalisha ajira kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na wilaya zake na Kusini Pemba na wilaya zake, ili kuzijengea uwezo na kuzielewesha majukumu yao.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wakuu wa Mikoa hiyo miwili kwa mashirikiano makubwa waliyotupa. *(Makofi)*

Malengo ya Idara ya Ajira kwa Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kukusanya taarifa za wafanyakazi walioajiriwa katika taasisi mbali mbali zilizoko Zanzibar;

2. Kuongeza fursa zaidi za ajira kwa wazalendo;

3. Kushirikiana na Kamati za Ajira za Kitaifa, Mikoa na Wilaya katika kujenga mikakati ya kutengeneza na kuwapatia ajira Wazanzibari;

4. Kukiimarisha na kukipatia taarifa, Kitengo cha Kukusanya na Kutoa Taarifa za Ajira;

5. Kutoa elimu kuhusu ajira kupitia njia mbali mbali;

6. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala yanayohusu ajira; na

7. Kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira ya Tanzania Bara, Shirika la Kazi Duniani pamoja na washirika wa masuala ya kazi na ajira katika kutekeleza Programu ya Tanzania Kuhusu Kazi za Heshima.

Mhe. Spika, ili Idara ya Ajira iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 65,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Mhe. Spika, idara hii ni mpya na ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Kazini Nambari 8 ya mwaka 2005, ikiwemo kuzifanyia ukaguzi sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria kuhusiana na masuala ya usalama na afya zinafuatwa.

Pia idara hii ina jukumu la kutoa maelekezo kwa Taasisi za Umma na Binafsi kuhusu masuala ya usalama na afya katika sehemu zao za kazi; kuzitambua, kuzisajili na kuweka kumbukumbu za usalama na afya katika sehemu za kazi kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 idara imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- Imezikagua jumla ya taasisi 74 kwa madhumuni ya kuangalia hali ya usalama na afya katika sehemu zao za kazi;

- Imeanza matayarisho ya awali ya kusajili sehemu za kazi kwa masuala ya afya na usalama kazini; na

- Imetembelea taasisi mbali mbali zinazofanya kazi zinazohusiana na masuala ya usalama na afya kazini kwa lengo la kuimarisha mashirikiano ili kuleta ufanisi.

Malengo ya Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kufanya marekebisho na kuimarisha mpango wa ukaguzi kwa ajili ya kutathmini hali ya usalama na afya katika sehemu za kazi;

2. Kuijengea uwezo Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa kuipatia vifaa vya kisasa na utaalamu, ili kwenda sambamba na viwango vya kitaifa na kimataifa;

3. Kutayarisha Sera ya Usalama na Afya Kazini;

4. Kutekeleza mpango wa usajili wa sehemu za kazi;

5. Kukuza ushirikiano wa kazi na taasisi nyengine ndani na nje ya nchi;

6. Kufuatilia kwa karibu zaidi matukio ya ajali, maradhi na madhara yanayotokana na ajali kwenye sehemu za kazi; na

7. Kuweka utaratibu bora wa wafanyakazi kuchunguzwa afya zao.

Mhe. Spika, ili Idara ya Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 75,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za wizara kwa upande wa Pemba. Katika mnasaba huo, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya ofisi hiyo kwa mwaka 2011/2012 ni kama ambavyo yameshaelezwa katika maelezo ya kila idara ambayo yanahusisha pia na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, ili Ofisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 90,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa kazi za kawaida.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, wizara yangu ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 58,288,000/= kupitia Kamisheni ya Kazi na Idara ya Ushirika. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011 jumla ya shilingi 79,738,850/= zilikusanywa, ambayo ni sawa na asilimia 136.8 ya lengo lililowekwa (Angalia Kiambatanisho Nambari 8). (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa vile wizara hii ni mpya, taarifa juu ya fedha zilizotolewa kwa matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni kwa kipindi cha kuanzia mwezi wa Januari 2011 wakati wizara ilipopata *vote* yake (*Vote* 27) hadi Juni 2011 ni karibu kipindi cha miezi sita.

Katika kipindi hicho, wizara imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi milioni 456,221,995/= kwa shughuli za kawaida. Hivyo, kati ya hizo, shilingi 248,751,579/= ilikuwa kwa ajili ya mishahara na maposho ya wafanyakazi na shilingi 207,470,416 kwa matumizi mengineyo kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho Nambari 9.

Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, wizara imeingiziwa jumla ya shilingi 102,350,000/=, kati ya hizo shilingi 35,000,000/= zilitolewa na Serikali kwa Mradi wa Maendeleo ya Ushirika na shilingi 67,350,000/= zilitolewa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa kupitia mradi wa *JP5*.

SHUKRANI

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali, ambazo

zilishirikiana na wizara yangu katika kutekeleza majukumu ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Zanzibar ni pamoja na:

Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), *Secretariat* ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki, Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*), Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*), *CRDB*, Jumuia ya Waajiri Zanzibar (*ZANEMA*), Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (ZATUC), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), *Vodacom*, Shirika la Bima la Zanzibar, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*), *Imani Clinic* na *Zanzibar Petroleum*. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa shukurani kwa Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mhe. Nassor Salim Ali (Aljazira) na Bi Naila Jidawi kwa michango yao ya vifaa vya michezo kwa Timu ya Wizara inayojuliakana kama Timu ya Uwezeshaji, ili kuwahamasisha wananchi waweze kujiandaa na kujipanga vizuri na waweze kujikwamua na umasikini. Vile vile napenda pia kuushukuru Uongozi wa Shehia ya Melinne kwa mashirikiano uliotoa katika usafishaji wa eneo la wizara wakati wa Kampeni za Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari zikiwemo televisheni, redio na magazeti kwa mchango wao mkubwa katika kuhamasisha, kutangaza na kuelimisha jamii juu ya masuala na matukio mbalimbali yaliyotekelezwa na wizara yangu yakiwemo masuala ya ajira, usalama na afya kazini, ushirika na uwezeshaji wananchi kiuchumi. *(Makofi)*
Mhe. Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi wote, Afisa Mdhamini na wafanyakazi wa ngazi zote kwa kufanya kazi kwa bidii katika kutekeleza malengo ya wizara. *(Makofi)*

Aidha, nawaomba wazidishe juhudi zaidi katika kutekeleza malengo yetu ya mwaka huu, ili kufikia kwa kiwango kikubwa zaidi na kutekeleza kivitendo azma ya serikali ya kuwawezesha wananchi wake kiuchumi na kupunguza kiwango cha ukosefu wa ajira.

HITIMISHO

Mhe. Spika, ili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wapokee na kujadili, kutoa ushauri na maelekezo na hatimaye kuidhinisha

matumizi ya jumla ya shilingi 1,545,000,000/= kwa kazi za kawaida, kati ya hizo shilingi 465,000,000/= kwa mishahara na posho la wafanyakazi na shilingi 1, 080,000,000/= kwa matumizi mengineyo.

Vile vile naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 90,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya shilingi 68,500,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1: ***Dhana ya Uwezeshaji***

DHANA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Uwezeshaji ni nini?

Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ni dhana pana na inagusa maeneo mengi ya maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa jumla.Dhana hii inatafsiriwa kwa namna mbili;

1. Kuwasaidia watu kutambua na kuongeza uwezo wao wa ubunifu na uzalishaji.

2. Kutoa motisha na nafasi, na kutengeneza mazingira yanayofaa kwa ajili ya kuongeza fursa za ajira na kufanya biashara au shughuli yoyote ya kiuchumi.

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi unajumuisha mipango, mikakati, sera na hatua zote zinazochukuliwa ili kufikia lengo, kwa kuhusisha sekta ya umma, binafsi na taasisi za kiraia.

Katika kufafanua majukumu ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunalichukulia suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi kuwa linajumuisha vitendo na hatua za makusudi zinazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kukuza na kuimarisha ujuzi, ustadi, umahiri wa kiuchumi na maarifa ili kuwawezesha walengwa kupata

ajira na kuzalisha tija itakayowezesha kunyanyua kipato chao na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi kwa lengo la kuinua maisha yao.

Kwa nini uwezeshaji?

Lengo kuu la uwezeshaji wananchi kiuchumi ni kumsaidia mtu mmoja mmoja na vikundi kutambua uwezo wao wa ubunifu na uzalishaji na kuleta ukuaji endelevu wa kipato na kunyanyua uchumi wao ili kuweka uwiano na kuondoa utofauti mkubwa wa hali za maisha baina ya wananchi.

Kwa ujumla dhamira ya uwezeshaji kiuchumi inaendana na lengo la kwanza la milenia (Kutokomeza umasikini uliokithiri na njaa) na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA).

Nani awezeshwe?

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unalenga katika kusaidia wananchi kubuni, kukuza na kuendeleza shughuli zao za kila siku ikiwa za uzalishaji au utoaji huduma ambazo huleta mabadiliko ya uzalishaji mali na kutoa huduma na kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na hatimaye katika uchumi kijumla. Shughuli hizo hufanywa na wananchi wa matabaka makuu matatu:

i.) Wenye kipato cha chini wakiwemo wakulima, wavuvi na wafugaji wadogo wadogo;
ii.) Wenye shughuli katika sekta isiyo rasmi na biashara ndogo sana, ndogo na za kati;
iii.) Wataalamu kwenye fani za kilimo, matibabu ya mifugo, uvuvi, uhandisi, usanifu majengo, sheria, uhasibu na nyenginezo.

Ili kupata faida kikamilifu kwenye uwezeshaji wa makundi yaliyotajwa hapo juu na yale yanayoonekana kuwa nyuma (*marginalized*) kiuchumi, itahitaji kwenda sambasamba na "uwezeshaji wa wajasiriamali wa kati na wakubwa" kwani hawa wanatarajiwa kuwapa msukumo wale walio dhaifu kiuchumi. Kwa kufanya hivyo, itasaidia wale wazalishaji wadogo wadogo kuweza kuunganishwa katika mtandao wa uzalishaji na utoaji huduma kwa vile masoko ya bidhaa zao yatakuwa ni wenye viwanda vya kati na vikubwa.

Maeneo ya uwezeshaji

Uwezeshaji wananchi kiuchumi una mahusiano ya moja kwa moja na ajira na kipato cha mtu mmoja mmoja, hivyo basi unaweza kugawanywa katika sehemu tatu kuu:

i. Miradi ya kiuchumi inayofanywa na wananchi wenyewe (iko katika hatua tofauti) na pia ile iliyoanzishwa na serikali kusaidia juhudi zao ;
ii. Kutoa huduma za kiuchumi au miundombinu ya kuendeleza juhudi za wananchi katika kujikomboa kiuchumi (*soft infrastructure, supportive services and logistics*); na
iii. Kuwawezesha kifedha na upatikanaji wa mikopo.

Katika juhudi za kuwanyanyua, kuwasaidia na kuwaendeleza wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma kuna haja ya kuangalia maswali ya msingi yafuatayo, kwa uzito wake:

Kutengeneza nafasi za kazi

- Hali gani ya sasa ya ajira kwenye sekta za uzalishaji na utoaji huduma?
- Namna gani ajira zinaweza kuzalishwa kwa wingi katika sekta mbalimbali (rasmi na zisizo rasmi)?
- Shughuli zipi zitazalisha ajira kwa wingi (kulingana na uwezekano na rasilimali)?
- Wahusika wakuu katika kuzalisha ajira ni nani (waliopo na wanaotarajiwa)?

Kuzalisha kipato

- Kipato cha wastani cha walio wengi ni kiasi gani?
- Ni makundi gani yaliyo katika hali duni zaidi kimapato na hivyo yatapaswa kupewa kipaumbele?
- Jinsi gani kipato cha walio wengi kinaweza kuongezeka?
- Vyanzo vipi vya kipato ni endelevu (kulingana na umuhimu)?

Shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Kwa ujumla, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazosaidia juhudi za wananchi kujikomboa kiuchumi zimekuwa zikifanya jitihada mbali mbali katika kufanikisha azma hiyo. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo, kiwango na nafasi ya shughuli hizo katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi hakijaweza kutathminiwa na kutambulikana kwa ufasaha. Pia hakujawa na mfumo muafaka wa kuratibu juhudi hizo.

Katika hali kama hiyo, juhudi hizi zinaweza kutoleta matunda yanayokusudiwa. Changamoto inayojitokeza ni kuainisha michango ya hizo shughuli na kutambua nini nafasi ya hizi shughuli moja moja katika utaratibu mzima wa uwezeshaji na namna ambavyo zinaweza kuratibiwa kwa ufanisi zaidi. Kwa kufanya hiyo, matatizo, vikwazo na changamoto katika shughuli hizo ambazo wananchi wamekuwa wakikumbana nazo, zinaweza kubainishwa na hatua za kiutendaji za kurekebisha hali hiyo kuchukuliwa haraka.

Kitaalamu, kuchambua shughuli za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa sasa inaweza kuwa ni ngumu, hata hivyo shughuli hizi tunaweza kuzigawa katika makundi makubwa yenye vipengele ndani yake kama ilivyoainishwa hapo chini.

a) Marekebisho ya kimiundo na kitaasisi

i. Kurekebisha miundombinu ya kisera, kisheria na kitaratibu katika kujenga mazingia bora ya uzalishaji mali na utoaji huduma;
ii. Urasimishaji wa mali na biashara;
iii. Utafutaji masoko ndani na nje ya nchi;
iv. Mabadiliko ya mitazamo ya sekta ya umma na ya sekta binafsi (*mindset change*);
v. Upatikanaji wa huduma za kuendesha biashara (*supportive services*).

b) Mafunzo na Elimu

i. Utoaji elimu ya ujasiriamali, ufugaji wa kisasa na kilimo bora;
ii. Utoaji elimu ya kutunza hesabu za biashara na umuhimu wa bima ya biashara;
iii. Kutoa elimu ya usimamizi na ufuatiliaji kwa watendaji;
iv. Elimu juu ya utunzaji wa hifadhi za misitu na vyanzo vya maji; na
v. Mafunzo kwa vikundi maalum (kutegemea na aina ya ujuzi utakaohitajika).

c) Kilimo na Ufugaji

i. Uendelezaji wa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku;
ii. Utoaji wa zana za kilimo na pembejeo kwa wakulima;
iii. Uendelezaji kilimo cha umwagiliaji;
iv. Huduma za ugani (*extension services*) kwa wakulima na wafugaji; na
v. Utoaji wa chanjo na elimu ya magonjwa ya mifugo na mimea.

d) Viwanda, Biashara, Masoko na Uwekezaji

i. Uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo;
ii. Usindikaji mazao na ufungaji vifurushi;

iii. Ufungaji mikataba ya biashara na usimamizi wake;
iv. Utoaji habari za biashara na masoko;
v. Utoaji wa maeneo ya kufanyia biashara na viwanda; na
vi. Kutenga maeneo ya uwekezaji na kuvutia wawekezaji toka ndani na nje ya nchi.

e) Maliasili na Utalii
i. Uendelezaji wa shughuli za utalii wa kimazingira (*eco-tourism*);
ii. Kulinda na kuimarisha misitu; na
iii.Utumiaji wa nishati mbadala.

f) Mikopo, Mitaji na Huduma za Fedha
i. Kuanzisha na kuimarisha *SACCOS*;
ii. Kuwezesha upatikanaji wa mikopo;
iii. Kukopesha vikundi vya uzalishaji na uchumi; na
iv. Utoaji mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

g) Miundombinu ya Utoaji Huduma
i. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kilimo na mifugo;
ii. Uanzishwaji wa miradi ya kukuza uchumi katika maeneo ya wananchi;
iii) Uanzishaji na uendelezaji wa vituo vya kutotoa wajasiriamali (business incubators);
iv). Kutengeneza barabara za vijijini; na
v). Kuimarisha na kupanua miundombinu ya kutoa huduma.

h) Mazingira na Huduma za Jamii
i. Usafishaji wa mazingira;
ii. Kuainisha matatizo na kubuni mbinu za kutatua matatizo kwa kushirikisha jamii;
iii.Kutambua, kuainisha na kutenga Maeneo ya Hifadhi

i) Uratibu na Usimamizi
i. Uendelezaji wa tafiti mbali mbali zitazosaidia kuimarisha na kuleta ubunifu katika shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
ii. Ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya uwezeshaji; na
iii. Kuanzisha na kuimarisha mahusiano na taasisi za Serikali, sekta binafsi na taasisi za kiraia ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na masuala ya uwezeshaji.

Kwa ujumla, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni suala mtambuka (*cross-cutting issue*) na linahusisha sekta zote za kiuchumi na kijamii. Hivyo Wizara

inayohusika na masuala ya uwezeshaji itahitaji kufanya kazi kwa karibu sana na Wizara na taasisi nyengine katika kufanikisha malengo yake.

Kiambatanisho Nambari 2: ***IDADI YA WAFANYAKAZI WANAOENDELEA KUPATIWA MAFUNZO HADI JULAI 2010 – JUNI 2011.***

Nam	JINA	JINSI		IDARA	KIWANGO	FANI
		ME	KE			
1	Fatma Moh'd Juma		x	Mipango, Sera na Utafiti	Shahada ya Pili	Uchumi
2	Iddi Juma Khamis	x		Kamisheni ya Kazi	Stashahada ya Uzamili	Uhusiano wa Kimataifa.
3	Khalil Thuwein Haji	x		Uendeshaji na Utumishi	Shahada ya kwanza	Manunuzi
4	Wardat Hassan Ali		x	Kamisheni ya Kazi	Stashahada	Rasilmali watu
5	Hawana Ramadhan Juma		x	Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	Sheria
6	Sarah Ali Abdalla		x	Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	Utawala wa umma
7	Juma Vuai Ameir	x		Kamisheni ya Kazi	Stashahada	Rasilmali watu
8	Asha Khalid Salum		x	Kamisheni ya Kazi	Stashahada	Teknolojia ya mawasiliano
9	Khamis Ali Omar	x		Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	Uchumi
10	Msemo Omar Iddi		X	M/Ushirika	Stashahada	Sheria
11	Kessi Issa Abdalla	X		M/Ushirika	Shahada ya Pili	Sheria
12	Machano Kh. Ame	X		M/Ushirika	Stashahada	Ushirika
13	Fatma S. Ramadhan		X	M/Ushirika	Shahada ya kwanza	Uhasibu
14	Nassor Said Masoud	X		M/Ushirika	Stashahada	Sheria
15	Salum Abdalla Salum	X		M/Ushirika	Stashahada	Ushirika
16	Mbarouk S. Mbarouk	X		M/Ushirika	Shahada ya kwanza	Uhasibu
17	Haji Khamis Haji	X		Kamisheni ya Kazi Pemba	Cheti	Rasilimali watu
18	Jamila S. Jabir		X	Mipango	Shahada ya kwanza	Utawala
19	Rauhia A. Gharib		X	Kamisheni ya Kazi	Shahada ya Pili	Rasilimali watu

20	Shuwena Hamad		**X**	Afisi Kuu – Pemba	Stashahada	Uchumi
JUMLA		**10**	**10**			

Kiambatanisho Nambari 3a: ***TAARIFA YA JUMLA YA MIKOPO YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ILIYOTOLEWA HADI KUFIKIA TAREHE 30 JUNI, 2011 – UNGUJA***

MKOA	**WILAYA**	**IDADI YA WALIOKOPA**	**FEDHA ZILIZOKOPWA**
Kaskazini	Kask "A"	56	98,800,000
	Kask "B"	54	146,800,000
Jumla ndogo		**110**	**245,600,000**
Kusini	Kati	23	53,700,000
	Kusini	87	133,100,000
Jumla ndogo		**110**	**186,800,000**
Mjini Magharibi	Magharibi	156	378,770,000
	Mjini	141	201,250,000
Jumla ndogo		**297**	**580,020,000**
Jumla Kuu		**517**	**1,012,420,000**

Kiambatanisho Nambari 3b: ***TAARIFA YA JUMLA YA MIKOPO YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ILIYOTOLEWA HADI KUFIKIA TAREHE 30 JUNI, 2011 – PEMBA***

MKOA	**WILAYA**	**IDADI YA WALIOKOPA**	**FEDHA ZILIZOKOPWA**
Kaskazini	Wete	46	99,270,000
	Micheweni	49	84,500,000
Jumla ndogo		**95**	**183,770,000**
Kusini	Mkoani	38	60,100,000
	Chake	78	207,350,000
Jumla ndogo		**116**	**267,450,000**
Jumla Kuu		**211**	**451,220,000**

Kiambatanisho Nambari 3c: UTOAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO KITAASISI YA MFUKO *WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (JK/AK) HADI TAREHE 30 JUNE 2011 KWA UNGUJA NA PEMBA.*

Taasisi	**Idadi ya waliokopa**	**Fedha zilizokopwa**	**D e n i**	**MAREJESHO**
Watu Binafsi	660	1 178 440 000.00	704 639 199.10	473 800 800.90
Saccos	10	117,700,000.00	66,962,697.60	50,737,302.40
Vikundi vya kiuchumi	58	167,500,000.00	82,781,492.55	84,718,507.45
Jumla	**728**	**1 463 640000.00**	**854 383389.25**	**609 256610.75**

Kiambatanisho Nambari 4a: ***MUHTASARI WA UTOAJI WA MIKOPO KUPITIA MFUKO WA KUJITEGEMEA JULAI 2010 - JUNI 2011 (UNGUJA NA PEMBA)***

MWAKA	**IDADI YA MIKOPO**	**IDADI YA WALIONUFAIKA**			**IDADI YA FEDHA**		**JUMLA YA FEDHA**
		W'KE	**W'ME**	**JUMLA**	**W'KE**	**W'ME**	
M/MAGH	15	15	3	18	11,500,000.00	5,000,000.00	16,500,000.00
KASK (U)	23	10	13	23	5,800,000.00	16,800,000.00	22,600,000.00
KUSINI (U)	10	6	8	14	5,300,000.00	4,300,000.00	9,600,000.00
Jumla ndogo	***48***	***31***	***24***	***55***	***2,600,000.00***	***26,100,000.00***	***48,700,000.00***
KASK (P)	15	5	14	19	3,450,000.00	15,800,000.00	19,250,000.00
KUSINI (P)	33	42	15	57	6,500,000.00	9,350,000.00	15,850,000.00
Jumla ndogo	***48***	***47***	***29***	***76***	***9,950,000.00***	***25,150,000.00***	***35,100,000.00***
JUMLA KUBWA	**96**	**78**	**53**	**131**	**32,550,000.00**	**51,250,000.00**	**83,800,000.00**

Kiambatanisho Nambari 4b: ***MAREJESHO YA MIKOPO YA MFUKO WA KUJITEGEMEA***.				
MWEZI	**UNGUJA**	**PEMBA**	**JUMLA**	**JUMLA MIEZI 3**
JULAI	3 048 500.00	1 625 000.00	4 673 500.00	
AGOSTI	5 592 000.00	2 384 000.00	7 976 000.00	
SEPTEMBA	3 440 450.00	2 855 500.00	6 295 950.00	18 945 450.00
OKTOBA	2 876 600.00	2 275 500.00	5 152 100.00	
NOVEMBA	6 207 600.00	2 058 000.00	8 265 600.00	
DISEMBA	5 533 450.00	2 362 500.00	7 895 950.00	21 313 650.00
JANUARI	5 320 500.00	2 864 500.00	8 185 000.00	
FEBUARI	5 419 300.00	2 587 000.00	8 006 300.00	
MACHI	4 126 400.00	2 639 000.00	6 765 400.00	22 956 700.00
APRIL	3 641 000.00	1 906 500.00	5 547 500.00	
MAY	6 500 000.00	2 600 000.00	9 100 000.00	
JUNE	3 422 450.00	1 742 500.00	5 164 950.00	19 812 450.00
JUMLA	**55 128 250.00**	**27 900 000.00**	**83 028 250.00**	**83 028 250.00**

Kiambatanisho Nambari 5:
UKUAJI WA 'SACCOSS BANK'KWA KIPINDI CHA DISEMBA 2010- MACHI 2011

MAELEZO	**2010**	**30-3-2011**	**ONGEZEKO LA WANACHAMA**
Ongezeko lwanachama: Wanaume			77 (5%)
Wanawake			36 (1.7%)
Jumla ya wanachama			**113 (3.1)**
I WA MITAJI			
Michango ya Hisa	49	)8	3. 40%
Ukuaji wa Amana za Wanachama	548,382,318	)28	17. 30%
I WA MIKOPO			
Ongezeko la mikopo iliyotolewa kwenye vyama	2,343	3,865,117,418	31.9%
Ongezeko la marejesho ya Mikopo	,687	770	12. 90%

Kiambatanisho Nambari 6: ***VYAMA VYA WAFANYAKAZI NA WAAJIRI VILIVYOFANYIWA UKAGUZI JULAI 2010 – JUNI 2011***

Nam	**JINA LA CHAMA CHA WAFANYAKAZI**
1.	Zanzibar Trade Union Congress - ZATUC
2.	Zanzibar Tourism, Hotel, Conservation, Domestic and Allied Workers Union - ZATHOCODAWU
3.	Zanzibar Union of Public and Health Employers - ZUPHE
4.	Telecommunication Workers Union of Tanzania Zanzibar - TEWUTA
5.	Zanzibar Financial Industrial, Consultant and Commercial Workers Union - ZAFICOWU
6.	Zanzibar Legal Government Workers Union - ZALGWU
7.	Researchers, Academicians and Allied Workers Union – RAAWU (Z)
8.	Communication Transport Workers Union of Zanzibar – COTWU (ZNZ)
9.	Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers – TUICO (Z)
10.	Zanzibar Plantation and Industrial Workers Union – ZPAWU
11.	Tanzania Seamen's Union, Zanzibar - TASU – Z
12.	Zanzibar Teachers Union – ZATU
13.	Zanzibar Employers Association – ZANEMA
14.	Zanzibar Federation of Public Services Union – ZAPSU
15.	Hotel Restaurants and Allied Union – HORAU
16.	Association of Public Sector Unions, East Africa – APSU – EA. ***(Chama kipya)***

Kiambatanisho Nambari 7: ***TAASISI ZILIZOPATIWA TAALUMA JUU YA SHERIA ZA KAZI NA UTEKELEZAJI WAKE JULAI 2010 – JUNI 2011***

Nam	**JINA LA TAASISI**
1.	Hoteli ya Bwawani
2.	Hoteli ya Kempiski
3.	Hoteli ya Mazsons
4.	Infornia Academy
5.	Skuli ya Alhuda
6.	Skuli ya Bilal
7.	Skuli ya Sufa
8.	Fundu Lagoon
9.	Hamisa Village
10.	Manta Resort
11.	Mpapindi Resort
12.	Pemba Island
13.	Pemba Lodge
14.	Pemba Paradise
15.	Swahili Diver

Kiambatanisho Nambari 8: ***MAKUSANYO YA MAPATO KUPITIA KAMISHENI YA KAZI NA IDARA YA USHIRIKA KWA MWAKA 2010/2011***

MAPATO YALIYOKUSANYWA KUANZIA JULY 2010 - JUNE 2011

Idara	**Kasma**	**Maelezo**	**Makadirio**	**Fedha Zilizokusanywa**	**Asilimia**
Kamisheni ya Kazi	37060	Malipo kwa Wataalam wa Kigeni	52,288,000.00	74,687,850.00	142.84
	37061	Malipo ya Ukaguzi Katika Sehemu za Kazi	2,000,000.00	2,196,000.00	109.8
Idara ya Ushirika	35015	Ada ya Uandikishaji Vyama	2,000,000.00	1,740,000.00	87
	35016	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	2,000,000.00	1,115,000.00	55.75
JUMLA KUU			**58,288,000.00**	**79,738,850.00**	**136.80**

Kiambatanisho Nambari 9: *MAPATO/FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA MWEZI WA JANUARI HADI JUNI 2011*

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA							
MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA 2010/2011							
Kasma	***Maelezo ya Matumizi***	***Pemba***	***Mipango***	***Mikopo***	***Kamisheni***	***Ushirika***	***Jumla 2010/2011***
11001	*Waajiriwa wa Kudumu wa Serikali*	*17,309,998*	*25,541,202*	-	*113,134,520*	*57,741,618*	*213,727,338*
12012	*Posho maalum*	-	-	-	*16,537,200*	*414,000*	*16,951,200*
13002	*Matumizi ya Ofisi*	*600,000*	-	-	-	-	*600,000*
13003	*Gharama za Simu*	-	*1,198,600*	-	*250,000*	*400,000*	*1,848,600*
13008	*Gharama za Telex,Telefax*	-	-	-	*250,000*	*75,000*	*325,000*
13009	*Gharama za Posta*	-	-	-	*150,000*	*135,000*	*285,000*
13011	*Gharama za Vifaa vya Uchapishaji*	*2,700,000*	-	-	-	*556,000*	*3,256,000*
13013	*Huduma za Mtandao*	-	-	-	*500,000*	*200,000*	*700,000*
14002	*Gharama za Petrol*	*833,669*	*2,000,000*	-	*1,902,400*	*5,831,015*	*10,567,084*
14004	*Gharama za Vilainishaji*	-	-	-	*375,000*	*325,000*	*700,000*
14005	*Gharama za Disel*	*4,000,000*	-	-	*300,000*	*5,556,160*	*9,856,160*
15003	*Vifaa vya Kuandikia*	*3,500,000*	*1,600,000*	-	*1,650,300*	*1,746,000*	*8,496,300*
15006	*Vifaa vya computa*	*300,000*	-	-	*700,000*	*2,690,000*	*3,690,000*
16002	*Matengenezo ya Madogo ya Ofisi*	-	-	-	-	*521,000*	*521,000*
16003	*Matengenezo ya Majengo*	-	-	-	*600,000*	-	*600,000*
17013	*Ununuzi wa Komputa*	*1,700,000*	-	-	-	*1,500,000*	*3,200,000*
17019	*Ununuzi wa Friji na A/C*	*1,000,000*	-	-	-	-	*1,000,000*
18003	*Ununuzi wa Honda,Vespa na Ciao*	-	-	-	*2,500,000*	*2,270,046*	*4,770,046*
20009	*Safari za Ndani*	*6,000,000*	*9,983,391*	-	*4,117,020*	*2,255,000*	*22,355,411*
20010	*Safari za Nje*	-	-	-	*10,993,000*	*365,000*	*11,358,000*
21004	*Mafunzo ya Ndani*	*3,750,631*	*5,000,000*	-	*1,800,000*	*7,184,000*	*17,734,631*
21005	*Mafunzo ya Nje*	-	-	-	-	*1,400,000*	*1,400,000*
21006	*Vifaa vya Mafunzo*	-	-	-	-	*1,208,000*	*1,208,000*
22009	*Msaada wa Wanafunzi*	*415,700*	-	-	-	-	*415,700*
23001	*Chakula na viburudishaji*	-	-	-	-	*162,000*	*162,000*
23002	*ununuzi wa zawadi*	*150,000*	-	-	-	*600,000*	*750,000*
23003	*Viburudishaji*	-	-	-	*1,500,000*	*150,000*	*1,650,000*
24002	*Gharama za Umeme*	*1,100,000*	*1,693,581*	-	*2,300,000*	*1,757,000*	*6,850,581*

25033	*Usimamizi wa sera sharia*	*-*	*-*	*-*	*-*	*4,953,430*	*4,953,430*
25030	*Gharama za Ushauri Nasaha*	*-*	*500,000*	*-*	*-*	*-*	*500,000*
25045	*Mfuko wa Jk na Ak*	*-*	*17,112,186*	*-*	*-*	*-*	*17,112,186*
26001	*Matengenezo ya Magari*	*2,000,000*	*-*	*-*	*416,000*	*1,500,000*	*3,916,000*
26004	*Vifaa vya Magari*	*800,000*	*-*	*-*	*-*	*936,000*	*1,736,000*
27007	*Ununuzi wa Samani,meza, viti na kabati*	*500,000*	*-*	*-*	*-*	*2,400,000*	*2,900,000*
28001	*Mchango wa Mfuko wa Hifadhi*	*1,730,402*	*2,554,116*	*-*	*9,197,065*	*4,591,458*	*18,073,041*
29029	*Mfuko wa Kujitegemea*	*-*	*-*	*47,626,728*	*-*	*-*	*47,626,728*
40002	*Safari za Likizo*	*650,000*	*-*	*-*	*900,000*	*150,000*	*1,700,000*
40005	*Malipo baada ya saa za Kazi*	*1,000,000*	*-*	*-*	*1,168,559*	*297,000*	*2,465,559*
40011	*Ununuzi wa Sera*	*-*	*-*	*-*	*261,000*	*-*	*261,000*
40001	*Posho la Vikao*	*-*	*3,000,000*	*-*	*7,000,000*	*-*	*10,000,000*
Jumla Kuu		***50,040,400***	***70,183,076***	***47,626,728***	***178,502,064***	***109,869,727***	***456,221,995***

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari) Mhe. Spika, Sifa njema zote zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu Bwana wa viumbe vyote ambaye ametujaalia kuwa na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa ili kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, Nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa msimamo wake imara na kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Halikadhalika, tunawashukuru watendaji wake

wote kwa ushirikiano mwema waliouonesha katika kujadili Bajeti hii kwa ngazi ya Kamati.

Mhe. Spika, Kamati yetu imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa kuijadili bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa umakini na umahiri mkubwa. Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mohammed Said Mohamed	-	M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Assaa Othman Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
5.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	-	Mjumbe
6.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Mjumbe
7.	Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
8.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu
9.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu

Mhe. Spika, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha kutoa taarifa kwa waomba kazi na wajasiriamali na kukipatia vitendea kazi kama kompyuta na samani za Afisi. Kukamilika kwa kituo hiki kutawapa fursa vijana wetu wenye uwezo wa kufanya kazi kuelewa kwa urahisi ni wapi wanaweza kupata kazi zanye kulinda heshima zao na zenye maslahi kwao. Aidha, watendaji wa kituo hicho wamepatiwa mafunzo juu ya uendeshaji wa kituo hicho.

Mhe. Spika, Tunaipa heko Wizara kwa kutayarisha mpango mkakati wa Kamisheni ya Kazi ambao ndiyo dira ya kutekeleza shughuli zote za Kamisheni. Mpango huu umetayarishwa makusudi kwa kukuza uchumi, kuongeza ajira kwa vijana na hatimaye kuwajengea uwezo wa kujitegemea

wenyewe. Pia, mpango mkakati wa Wizara nzima nao umeandaliwa kwa lengo lilelile la kuwainua wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa mno na fungu lililotengwa kwa ajili ya ununuzi wa samani kwa Afisi Kuu ya Wizara iliyoko Pemba kwa mwaka huu wa fedha ambalo ni jumla ya shilingi za Kitanzania 8,100,000/=. Mhe. Spika, Wizara hii ni changa na mpaka wakati Kamati yetu ilipoitembelea mwezi wa Febuari mwaka huu, ilikuwa haina hata jengo la makao makuu. Kwa mnasaba huu basi, Wizara hii inahitaji samani zote za Afisi mara baada ya kupata jengo. Kamati yetu ina wasiwasi mkubwa kwamba shilingi 8,100,000/= hazitokidhi mahitaji hayo.

Mhe. Spika, Tunaishukuru Wizara kwa kuendelea kuratibu vyema mfuko wa AK na JK ambao ni tegemeo kwa wananchi wanyonge wa Taifa hili. Ingawa kuna kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza, Idara ya usimamizi wa mikopo imetoa semina elekezi kwa Kamati ya Usimamizi wa mfuko huu ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kukabiliana na changamoto zilizopo ili kuzifanya hali zao kuwa bora zaidi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ukubwa wa riba, mikopo kutopatikana kwa wakati na kiwango kidogo cha fedha zinazokopeshwa. Pamoja na changamoto hizo, Wizara inatarajia kuanzisha maeneo mapya ya ukopaji na kuhakikisha mikopo hiyo inatolewa kwa wakati ili kuwanufaisha zaidi wananchi.

Mhe. Spika, Rasimu ya marekebisho ya Sheria namba 4 (1986) inayoongoza shughuli za Ushirika hapa Zanzibar iko katika hatua za mwisho za maandalizi. Tunaipongeza sana Wizara kwa hili kwani sheria hii itaviwezesha vyama vya ushirika na *SACCOS* mbalimbali kufanya shughuli zao kwa misingi imara itakayowawezesha wanachama wa vikundi hivyo kukuza uchumi wao na kupunguza umasikini wa kipato.

Mhe. Spika, Matumizi ya teknolojia ya kisasa yametiliwa mkazo sana na Wizara hii ambapo hadi sasa Wizara imefanikiwa kuanzisha mfumo wa kuhifadhi taarifa *(data base)* zinazoonesha mahitaji na uwezo wa sekta ya ushirika. Teknolojia hii itawawezesha wananchi kupata taarifa za kiushirika kwa wepesi zaidi na hivyo kupata muamko zaidi katika shughuli zao.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi kwa kuwapatia maafisa wake watatu mafunzo ya msingi kuhusu namna bora ya kukusanya taarifa za ajira ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika inastahili pongezi maalum kwa kuwapa fursa watendaji wake kushiriki katika mikutano ya Kitaifa na ile ya Kimataifa. Maafisa wawili wa Kamisheni ya Kazi wameshiriki kwenye kikao cha kujadili maeneo ya vipaumbele muhimu vya kuzingatia wakati wa kutekeleza mpango wa pili wa Kazi za staha nchini Tanzania ulioandaliwa na shirika la kazi duniani *(ILO)*, maafisa watatu wameshiriki katika mkutano wa kufanya mapitio katika baadhi ya sheria za Tanzania ambao umeandaliwa na Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, Tunaipongeza sana Kamisheni ya Kazi kwa kumpatia mafunzo Afisa mmoja wa kazi juu ya mambo yanayohusu usalama na afya kazini huko Italia. Pia, elimu juu ya sheria za kazi imetolewa na Wizara hii ambapo jumla ya vipindi viwili kwa mwezi vinarushwa na Sauti ya Tanzania Zanzibar.

Aidha, katika jitihada za kwenda sambamba na Jumuiya za Kimataifa, Wizara imewapatia maafisa wake sita mafunzo ya uandishi wa ripoti za utekelezaji wa mikataba ya Shirika la Kazi duniani. Hatua hii ni muhimu kwani itaiweka Zanzibar katika ukurasa wa nchi zinazokwenda sambamba na Mashirika ya Kimataifa ili hatimaye kufaidika na misaada inayotolewa na Mashirika hayo.

Mhe. Spika, Serikali imeweka milango wazi kwa wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha miradi yao mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa fursa mbalimbali za ajira kwa vijana wetu. Pamoja na msimamo wa kuwataka wawekezaji kutoa kipa umbele zaidi kwa wazalendo wenye sifa katika suala la kuwapatia ajira, bado kuna wawekezaji wanaokaidi amri hiyo. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwafuatilia kwa makini wawekezaji kutoka nje wenye tabia hiyo na kuwachukulia hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, Kutokana na hali mbaya wanayokumbana nayo wajasiriamali walioko katika masoko, Kamati imewashajiisha wafanyabiashara hao waunde ushirika au *SACCOS* katika maeneo yao ya kazi ili waweze kupata maendeleo zaidi ya kiuchumi kutokana na kufaidika na fursa za mikopo watakayopatiwa.

Aidha, kupitia vyama hivyo wataweza kuyatatua matatizo mbalimbali yanayowakumba kwa vile vyama hivyo vitakuwa na nguvu na sauti kutokana na kusajiliwa na kutambuliwa kisheria. Kufanya hayo pia kutachangia kwa kiasi kikubwa kufanikiwa kwa azma muhimu ya Serikali hii ya awamu ya saba ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kamati pia imewaagiza watendaji wa Wizara kupitia Idara ya vyama vya ushirika kuonana na wafanyabiasha waliopo katika masoko ili kuwapa taaluma na maelekezo ya kina ya uundaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika na *SACCOS*

Mhe. Spika, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara hii kutoa kipaumbele zaidi katika kuviimarisha na kuviendeleza vikundi vya ushirika na *SACCOS* zilizopo. Imeonekana kuwa vikundi vilivyopo vinadhoofika kutokana na wanachama wake kuanzisha vikundi vyengine na kuwa na uanachama wa vikundi vingi kwa wakati mmoja. Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara kwa kutayarisha dodoso la kukusanya taarifa zitakazowezesha kufahamu vikundi vya ujasiriamali vilivyopo, shughuli wanazozifanya na ujuzi walionao katika kutekeleza shughuli zao. Taarifa hii itakuwa kigezo cha kupanga na kupima utekelezaji wa mipango ya uwezeshaji kupitia programu mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kusajili vyama vya Ushirika 177 (84 Unguja; 93 Pemba), kiwango ambacho kimevuka lengo la kusajili vyama 171. Kiwango cha utekelezaji wa zoezi la usajili ni asilimia 103. Vyama vilivyosajiliwa vimejumuisha vya huduma na miradi mbali mbali ya kiuchumi, vyama vya uzalishaji, kazi za mikono, *SACCOS*, na vyama vya kilimo na ufugaji. Utekelezaji huu umeongeza takwimu na idadi ya vyama mbali mbali vilivyo sajiliwa kufikia 5,581.

Mhe. Spika, Kamati inaiagiza Wizara kutekeleza kikamilifu sheria namba 8 ya mwaka 2005 (*Occupational Safety and Health Act*) inayohusu usalama na afya kazini kwa kuwawezesha kiutendaji wakaguzi wa Idara ya Usalama na Afya kazini ili watekeleze ipasavyo kazi zao za kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya kazi yakiwemo masoko ili kuona kuwa sehemu hizo ziko katika mazingira mazuri kiusalama na kiafya.

Aidha, kutokana na sehemu nyingi za kazi kukosa vifaa vya kuzimia moto, Kamati inaiomba Wizara kuwasisitiza wakuu wa masoko pamoja na wa sehemu nyengine za kazi (ziwe za kiserikali au watu binafsi) juu ya umuhimu wa kuweka vifaa vya kuzimia moto katika taasisi wanazoziongoza sambamba na utoaji wa wa elimu ya matumizi ya vifaa hivyo muhimu ili sehemu hizo ziwe na usalama wa kutosha.

Mhe. Spika, tunaipongeza sana Wizara kwa kuwapeleka Maafisa watatu katika mkutano ulioandaliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mkutano huo ulikusanya maoni yatakayosaidia kufanya mapitio katika baadhi ya sheria za Tanzania (sheria ya ardhi na sheria ya kazi) ili kuondoa kasoro zilizopo kwa kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Hatua hii ni muhimu sana kwa mustakbali wa Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, Kamati ina wingi wa furaha kutoa pongezi zake kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kuvuka lengo la makusanyo yaliyokadiriwa Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 ambayo ni Shilingi Milioni Hamsini na Nane, Laki Mbili Themanini na Nane Elfu (Shs. 58,288,000/=) ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2011 jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Tisa, Laki Saba Thelathini na Nane Elfu, Mia Nane na Hamsini (Shs. 79,738,850/=) zilikusanywa, ambayo ni sawa na asilimia 136.8 ya lengo lililowekwa.

Mhe. Spika, Kamati imetoa maelekezo kwa uongozi wa Soko la kuku Darajani na soko la Mwanakwerekwe kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa mbogamboga waliopo katika masoko hayo wanarejeshwa tena katika maeneo yao mara baada ya matengenezo kukamilika.

Kamati pia inaiomba mamlaka husika kuzipitia upya kodi zinazotozwa kwa wafanyabiashara hususan wafanyabiashara wachache waliobakia katika soko la Mombasa kwani kodi hizo zinaonekana kuwakandamiza kiuchumi hasa kwa vile mapato yao katika soko hilo ni kidogo mno.

Mhe. Spika, vikundi vingi vya ushirika vinaonekana kukosa elimu ya ushirika kwa wanachama wake ikiwa ni pamoja na kutojua haki na wajibu wao. Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna mashirikiano madogo baina ya vikundi vya ushirika na serikali na kuishauri wizara kupitia idara ya vyama vya ushirika kuwa karibu sana na vikundi hivyo ili kutambua matatizo yao na kuyapatia ufumbuzi. Aidha, utaratibu maalum wa elimu na ushauri uandaliwe kwa vikundi hivyo juu ya uendeshaji wa vikundi vya ushirika na *SACCOS*.

Aidha, kutokana na ukosefu wa taaluma ya kilimo na mifugo kwa vikundi vya ushirika, serikali kupitia taasisi husika inapaswa kueneza taaluma hiyo nchi nzima ili tuweze kuzalisha bidhaa wenyewe na kuwawezesha wananchi kujiendesha kiuchnumi, kibiashara na kuchangia pato la taifa.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwepo tatizo la ukosefu wa mitaji na ukosefu wa taarifa sahihi na za kutosha juu ya fursa za mikopo kwa vikundi vya ushirika. Vikundi huwa vinakosa mitaji ya kuendesha shughuli zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosekanaji wa taarifa sahihi juu ya fursa za kupata mitaji. Hali hii huvifanya vikundi vingi kubaki na umasikini wakati fursa za kuwezeshwa kiuchumi zipo.

Hivyo, kamati imeitaka wizara kushirikiana kikamilifu na Serikali za Wilaya kuhakikisha kuwa taarifa za upatikanaji wa mikopo zinawafikia walengwa kwa usahihi na kwa wakati. Aidha, wizara inapaswa kuhakikisha kuwa mikopo

inayotolewa inawafikia walengwa na kutumika kama ilivyokusudiwa. Mkazo uwekwe kuwezesha vikundi kielimu, kiuchumi, na hata kufanyiwa ziara za kimafunzo.

Mhe. Spika, Shukuzani za dhati tunazitoa kwa fungu lililotengwa kwa ajili ya Kamisheni ya Kazi ambalo ni jumla ya shilingi 222,000,000/=. Ni dhahiri kuwa mgao huo umefanywa kutokana na majukumu makubwa inayobeba Kamisheni hii.

Mhe. Spika, Kamati inaiomba Wizara ifanye jitihada za kuwawezesha wanawake hususan walioko vijijini kupata miradi watayoweza kuimudu kwani kuna baadhi ya miradi ya kinamama hao inaonekana kuwatesa kama vile mradi wa mwani ambapo faida inayopatikana haiendani na nguvu zinazotumika.

Vilevile, Kamati inaiomba Wizara kuwafikria sana watendaji wa Idara ya mikopo kwa kuwapatia usafiri ili waweze kuwafuatilia wadaiwa sugu wa mikopo hiyo.

Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo, niwaombe sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 1,545,000,000/= kwa kazi kawaida, shilingi 465,000,000/= kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 1,080,000,000/= kwa matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 12.1 tu ya mahitaji halisi ya Wizara.

Kadhalika, nawaomba Waheshimiwa kuiunga mkono bajeti ya Wizara hii kwa upande wa kazi za maendeleo ambayo ni jumla ya shilingi za Kitanzania 90,000,000/= kwa miradi miwili ambayo inatarajiwa kutekelezwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mwisho Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunivumilia wakati wote nilipokuwa nikisoma hotuba hii, pia natoa shukurani kwa wawakilishi wenzangu watukufu kwa kunisikiliza kwa makini ili waweze kuichangia hotuba hii ya bajeti vilivyo.

Sitosahau kabisa kutoa shukurani kwa wananchi wangu wote wa Jimbo la Mtambwe kwa imani yao waliyonipa kwa muda mrefu sana ya kuniamini kuweza kuwatumikia, ishaalla naamini nitawatumikia kwa misho wa uhodari wangu, Mwenyezi Mungu atujaalie Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa aipe baraka ya uwezo na kuweza kufanikisha yale yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Abdalla Juma Abdulla: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya mwanzo kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Rais nimpongeze kwa dhati kwa kutanabahi kwamba kuna haja ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, nafikiri kafanya hivi kwa sababu anajua wananchi wa Zanzibar ni wanyonge na wanahitaji kuwezesha.

Lakini la pili nimpongeze kwa kuunda hii Wizara ambayo ni maalum kwa kazi hiyo, pia nimpongeze sana kwa kumchagua Mhe. Haroun Ali Suleiman kuwa Waziri wa Wizara hii, mimi naamini Mhe. Waziri ana uwezo mkubwa kwa sababu ni mchapa kazi namjua sana, lakini nimpongeze zaidi Mhe. Waziri kwanza kwa kuchaguliwa lakini nilipoangalia hiki kitabu chake nilifurahi sana maana hiki kitabu kina sifa kubwa, kwanza nimeona chati ya uongozi hapa lipo hapa kwenye ukurasa wa mwanzo kabisa kitu ambacho sijaona kwenye vitabu vyengine.

Nafikiri ni jambo zuri la kuiga kwa sababu unapata kuona wale wakurugenzi wote hapa, Makatibu wa kuu na wengine, na nilipoangalia chati la uongozi ndio nikasema kuna faida kubwa nimepata kuona kwamba ishu imezingatiwa sana, kati ya wakurugenzi hawa kumi wanne ni wanawake Mhe. Spika, jambo zuri sana. Lakini pia hata kitabu ukikiangalia humu ndani sijui kenda kakichapisha wapi maana yake safi kabisa na kinaonekana vizuri sana, nilikuwa naomba na Mawaziri wengine waige huku alikokwenda kuchapisha Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba Wazanzibari ni sawa na binaadamu wengine wowote duniani binaadamu akiwezeshwa anaweza, ndio maana nikasema namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuunda Wizara hii na kuona kama kuna haja ya kulifanyia uratibu suala la uwezeshaji. Kule Japan watoto wadogo ukenda kila mtu ana kiosk chake anafanya kazi za ufundi ndogo ndogo tu ambazo kwa kweli ni ajira tosha, makampuni makubwa yale yanaunda gari wao kazi yao ni kufunga tu ile gari lakini kazi zote huwa wanazigawa kwa wataalam wadogo wadogo, kuna kiwanda kuna mtu kazi yake yey ni kutengeneza bolti tu tena za saizi fulani, kuna mtu kazi yake kutengeneza nati tu. Sasa hizi ni ajira ambazo wamewezeshwa kupata ule utaalam wakawezeshwa kupata vijimashine vya kuunda sasa wanaweza na wanaendesha mauisha yao, kwa hivyo na sisi Wazanzibari tukiwezeshwa kwa kweli tunaweza kufika pahali kama hapo.

Lakini jambo jengine ambalo nataka niseme Mhe. Spika, huwezi kufanya jambo lolote bila ya kuwa na sera, nimeona Mhe. Waziri kaipa umuhimu sera

katika kitabu chake hii sera ni muhimu sana kwa sababu ndio itakayotoa dira, na itakayoweza kutoa muongozo tuanze wapi, tupite wapi tunakusudia kufika wapi ni sera, kwa hivyo sera iharakishwe sana kutengenezwa waletewe waheshimiwa wajumbe hapa waichangie halafu ifanyiwe kazi.

Mhe. Spika, unaposema uwezeshaji wananchi kiuchumi mimi tafrisi yangu ni ajira kwa sababu ajira ziko za aina nyingi, kuna ajira ambazo zinatoka serikalini moja kwa moja, kuna ajira zinatoka kwenye makampuni binafsi lakini na sehemu kubwa sana ya ajira ambayo mimi naitilia maanani zaidi ni *private sector*. Hii ina mambo mengi sana na ndio inamaliza kundi lote ambalo halikupata ajira kazini au kwenye makampuni binafsi, lakini wote ni sawa sawa na kwamba wako katika *private sector*, wengine wako kwenye biashara wengine wana kazi zao za ufundi, wengine wako kwenye kilimo, kwenye uvuvi zote hizo ni aina za ajira ambazo nilikuwa namshauri sana Mhe. Waziri uratibu wake zaidi uelekee huko.

Mhe. Waziri mimi nataka niseme yeye ni mratibu tu wa uwezeshaji kwa sababu suala la uwezeshaji ni suala mtambuka, linagusa sekta nyingi sana za nchi kwa hivyo yeye kama awe mratibu au mshauri jamani tufanyeni hivi na hivi, jana tulikuwa na semina moja katika jambo ambalo mimi niliona linanigusa mara kwa mara ni kuona tunatayarisha ajira zile ambazo zina soko katika nchi, tulikuwa tunazungumzia mambo ya uvuvi jana tulikuwa tunazungumza sana, sasa hatuwezi kuwafikisha wananchi kwenye uvuvi.

Kwa kweli asilimia kubwa ya wananchi wetu kwa sababu wamezungukwa na bahari basi tuliwatarajia zaidi wajiajiri wenyewe katika uvuvi. Lakini siwezi kukurupuka tu Mhe. Spika, nikenda nikavua ni lazima nitayarishwe na nipewe taaluma za uvuvi. Siku za nyuma tulikuwa tunao utaratibu wa kusomesha mambo ya uvuvi. Ni muhimu sana ule utaratibu tuurejeshe na sio uvuvi tu hata masomo ya biashara kwa sababu ndio kazi zenyewe hizo, masomo ya kilimo. Nakumbuka Fidel Castro ilikuwa kazi yake ni kutayarisha watu kwa kilimo tu, Lumumba ikitayarisha watu kwa ajili ya mambo ya uvuvi tu. Kuna mikunguni mambo ya kapenta na mambo ya umeme (ufundi).

Hivi vyuo kwa wakati wetu wa sasa hasa kwa sekta hii ya uwezeshaji ni muhimu sana. nilikuwa nadhani serikali iyaangalie upya na wala tusianze pale kwenye sekondari. Mimi nafikiri mambo haya tuyaweke kwa sababu ni mambo muhimu. Tuyaweke katika mitaala yetu hata kwenye skuli za msingi. Kuna mitaala ya kilimo, kuna mitaala ya uvuvi, mitaala ya biashara. Watoto wetu wakikuwa wawe na taaluma ya kutosha.

Sasa yule utakapofika pahali ukampa mkopo basi mkopo wako haupotei wala huwi na wasi wasi kwamba anaweza kurejesha ule mkopo au harejeshi. Kwa sababu tayari kwa upande mmoja umekwisha kumuwezesha kuwa taaluma ya kukitumia vizuri kile ambacho utamkopesha. Hili ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, katika kupita pita na Kamati tumekutia watu wana vikundi vya ushirika. Ni vizuri kujikusanya katika vikundi vya ushirika lakini wana ushirika wanapewa mikopo. Mimi nimeiyangalia mikopo katika mitazamo miwili. Mkopo unaweza kumuwezesha mtu kiuchumi ikiwa utakuwa na sifa mbili. Sifa ya kwanza ule mkopo wenyewe uwe unalingana na lile ambalo unataka kulifanya unakidhi haja.

Pili yule ambaye unampa ule mkopo awe na taaluma ya lile analolifanya. Ikiwa anao utaalamu wa kutosha wa kuvua ukimpa mtaji wa kutosha wa kuvulia basi huyo atazalisha kweli kweli, atajiajiri yeye na ataajiri na wengine. Ikiwa mkopo ni mdogo hautoshi halafu ukenda ukampa mtu, ukanipa mimi Abdalla Juma ukanambia nenda kavue. Mhe. Spika, pesa zile nitazipiga kuni na mkopo sitorejesha tena kwa sababu siuzalishia. Hatimaye mimi nitashtakiwa nimekopa sikulipa, kwa hivyo badala ya kunisaidia itakuwa nimerudi nyuma sana kiuchumi.

Sasa nadhani tuangalie mambo mawili zaidi kwanza mikopo iwe yenye kiwango kidogo. Mhe. Spika, sasa hivi wewe ukitafuta ajira ambayo utajituma kwa nafsi yako kwa nguvu zako mwenyewe utatia mle ili jioni ikifika upate Shs. 10,000/- za watoto basi hazitapungua milioni 10 ndio ufike hapo. Sasa huwezi kumpa mtu shilingi laki tano halafu ukamwambie mtu jioni apate kijio hapati. Nilikuwa naona hapa Mhe. Waziri ana changamoto kubwa kweli kweli. Kwa sababu maisha yanabadilika sasa hivi, faida inayokuja ni ndogo sana, ili usishuke basi uwe na mkopo kidogo uliokuwa unatizamika.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nataka niseme ni kuhusu Idara ya Ajira, nimeiyona humu na kazi zake ukurasa wa 53 ukiangalia pale utakuta. Idara hii ina changamoto nyingi. Kuna mambo mengi sana ya kufuatilia. Kwanza nimeona kazi yake moja ni kushughulikia ajira na kuangalia zaidi wazalendo.

Mhe. Spika, wajumbe wako wamekuwa wakilalamikiwa sana namna ajira zinavyotolewa katika nchi. Kuna Makampuni haya ya kitalii, yanakuja hapa yanapewa maeneo ya wazalendo, ardhi kubwa ambayo na sisi tuna migogoro mitupu. Wakishakuwekeza wanasahau kama alikuwa ana makubaliano na serikali, awaangalie zaidi wazalendo.

Yeye anatafuta jamaa zake huko kama katoka Kenya ataleta Wakenya wenzake mpaka wale wa kuosha vyoo na kufagia, utafikiri hapa Zanzibar hakuna watu ambao wanaweza kufanya kazi hiyo. Wananchi wamenyang'anywa ardhi zao kama walikuwa wanalima pale hawalimi tena. Walidanganywa watapatiwa ajira hawakupatiwa. Sisi waheshimiwa tunapata tabu sana kwa kushtakiwa mambo kama hayo. Sasa nilikuwa naomba sana idara hii ifatilie kwa karibu sana ajira za wazalendo.

Jambo jengine kuna ajira zinatolewa na Sekta ya Muungano na hasa katika sekta za ulinzi Niliwahi kusema nilipokuwa nachangia Wizara ya Utumishi wa Umma kwamba wananchi wananung'unika sana kwamba zile ajira zikija zinakuwa zimepigwa mafungu kabisa. Kwa mfano Wizara ya Mambo ya Ndani inaweza ikasema mara hii tunaajiri askari 4,000 nchini, lakini hawa 3,000 watakuwa Watanzania Bara, 1,000 itakuwa ya Wazanzibari. Ile ya Wazanzibari ikifika hapa wanasema kwa mfano 600 ni watu kutoka kisiwa cha Unguja 400 kutoka kisiwa cha Pemba.

Kama utaweza kutoa ajira za aina hiyo zinawasaidia sana watu. Lakini kinachosikitisha hizi ajira hawazipati hawa walengwa. Tunahuu utaratibu wa kwamba mtu unamtoa Mtwara anakuja kufanya kazi Zanzibar basi na zile fursa za Wazanzibari zote anazichua yeye sasa. Ataleta vijana wake kutoka huko kwa mfano kama ni Kamanda wa Polisi zimekuja ajira katika Mkoa wake 20 au 30 pale anaagiza vijana kutoka huko, wanakuja hapa wanajaza fomu hapa kama ni Wazanzibari, wanapewa ajira zile matokeo yake wale wazalendo wa hapa hawapati ajira.

Kule Pemba siku wanaokaa foleni watu kutaka ajira za polisi, ukenda ukiwasalimia tu utashangaa, mbona sio hawa. Inasikitisha sana kwa kweli. Mambo haya yanafanyika kwa polisi na jeshi. Sasa nilikuwa naona hii ni changamoto sana nchini kwetu, kwa sababu watu wetu ni wanyonge na wanahitaji hizi ajira. Sasa watu wameshapewa zao na zetu wazichukue. Inasikitisha kwa kweli. Nilikuwa naomba sana Idara hii ya ajira ifuatilie kwa karibu kweli kweli.

Mhe. Spika, nilipigiwa simu niliulizwa nipo hapa Unguja kwenye Kikao cha Bajeti. Mwenzangu wa huko nyumbani, akanipigia akanambia bwana weee, tunasikia kuna watu wanaandikishwa hapa wanakwenda kuajiriwa nje ya nchi. Mimi sikujua wapi. Lakini sijasikia kitu kama hicho, nikamwambia si kweli, maana sijasikia miye. Akanambia bwana lifuatilie isijekuwa lipo hilo.

Mimi nikawatania jamani kuweni na tahadhari na mambo hayo. Kuna mtu alikuja hapa akasema anataka kutoa ajira ana *NGO's*. Tukachanga pesa, mimi

peke yangu nilitoa laki tano. Kwa sababu kila mpiga kura wangu ananijia bwana weee kuna ajira hebu nipe 30,000 mara huyu nipe kiasi fulani. Mimi natoa najua kuna ajira. Jamaa katia pesa mfukoni halafu kakimbia.

Siku hiyo nikamkuta kwenye boti tunatoka Dar-es-Salaam kwa sababu namfahamu. Nikamwambia wewe bwana umeniibia pesa nyingi na sikubali nitakushtaki. Akanambia huwezi kunishtaki mimi hapa nilipo natoka Nachingweya natoka kuroga hamnambii chochote. Huyo ni kijana wa Kipemba lakini kaiba pesa nyingi, nashangaa kuwa mpaka leo hakushtakiwa. Sasa nikamwambia kuweni na hadhari na mambo haya. Wakanambia liulizie.

Mhe. Spika, mimi nikachukua hatua ya kuulizia wenzangu, nikasikia kuwa hili jambo lipo. Kuna vijana wanaandikishwa halafu wanasafirishwa sijui wanapelekwa nchi gani, kuna ajira huko sijui za miaka miwili sijui za nini.

Sasa nilikuwa naona kwa mujibu wa kitabu hiki nilipoangalia hii Idara ya Ajira inahusika na mambo haya. Sasa kama lipo kweli basi lisiwe la siri ni vyema serikali ikalitangaza wananchi wakajua masharti yake, wakajua kila kitu. Hili linaweza kuwasaidia vijana wetu kwenda kupata miaka miwili ya kufanya kazi pengine wakirudi hapa watapata msingi wa kufanyia shughuli zao nyengine.

Mhe. Spika, sina manemo mengi, nafikiri mimi binafsi nimevutiwa sana na mipango ya wizara hii. Kwa sababu ni mpya mimi naunga mkono mia juu ya mima Mhe. Spika. Inawezekana mwakani kama Mhe. Waziri atakuwa hajafanya vizuri sana nikaja nikapita buti lakini kwa mara hii sipiti buti naunga mkono. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia na mimi kidogo kuhusiana na Wizara hii mpya.

Mhe. Spika, namshukuru Allah kutupa uhai, uzima na taufiq ya kuzungumza katika Baraza lako. Mimi napenda nimuunge mkono mwanzo kabla ya mwisho. Naunga mkono hoja mia juu ya mia. Lakini natumia lugha ya kisheria kwa masharti kwamba atakubaliana na suala zima la uongozi bora. Yaani utawala bora.

Mhe. Spika, hii wizara ina mtihani kwa hivyo Mhe. Waziri namuomba sana yapatikane mambo manne kwanza.

1. Kuwe na uwazi katika shughuli zake za kazi.

2. Shughuli ziwe zinatabirika kwa maana kama kuna uwezeshaji ikiwa kwa njia ya mkopo au kwa njia ya *guarantee*, yule ambaye anakamilisha zile sharti iwe anajua kuwa moja kwa moja mimi nitaingia katika mkumbo huu.

3. Kuwe na uwiyano wa kuwezeshwa. Mambo mengi yanaingia dosari pale uwiyano utakapokuwa mdogo wa Kikanda, Kiwilaya au Kivisiwa. Bila shaka pale ambapo *population* kubwa utategemea kwamba uwezeshaji nao uwe ni mkubwa.

4. Kutokana na *survey* hii inayofanywa ya (*HBS) House Hold Budget Survey* inaonesha kwamba kuna maeneo ni magumu zaidi na ni yana umasikini zaidi kuliko maeneo mengine na wao iwe ni *priority* kubwa zaidi kuweza kuwezeshwa.

Hayo mambo manne ambayo miye nahisi akiyaangalia sana Mhe. Waziri yanaweza yakasaidia sana katika kuipeleka mbele hii wizara na kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi.

Jambo jengine ambalo mimi ninalo ni kuhusu Idara hii ya Ajira. *Concern* yangu hiyo italingana vile vile na Kamisheni ya Kazi. Mimi ningelihisi tungepambanua baina ya ajira ya sekta ya serikali na ajira ya sekta binafsi. Kwa sababu sekta ya serikali ajira zake zimefungika. Ukiachilia kada ya ualimu ambayo unaweza uka *predict* kwamba kwa mujibu wa *ratio* ya walimu ilivyo basi mahitaji ya walimu yapo. Hata mtu wa kawaida anaweza akaieleza wizara kwamba kuna upungufu huu wa walimu.

Lakini ndani ya maofisi si rahisi mwananchi wa kawaida kujua kwamba kuna upungufu kadhaa wa kadha. Lakini katika ajira za binafsi ni ajira ambazo zinakuja na ukuaji wa uchumi. Uchumi ukikuwa na ajira zinaongezeka *automatically*. Kwa sababu watu wanahitaji kufanya shughuli zilizopo. Nakusudia uchumi ni pamoja na harakati zenyewe za kiuchumi kama kuna ujenzi kwa mfano. Idara yenu au wizara yenu ilikuwa ijue kwamba ujenzi huo unaokuja utawanufaisha nani? Kunakuja makampuni yanataka kufanya labda tafiti. Kwa hivyo tafiti hizi zinazofanywa zitawanufaisha nani.

Mimi nafikiria lile suala la ajira hata hizi ajira za muda pia nazo zina faida yake. Kwa sababu vinachangamsha ule uchumi uliyopo. Lakani kama hatukujipanga vizuri hata hizo ajira za muda zinaweza zikatumiwa vibaya.

Kuna ajira zinazopigiwa kelele sasa hivi zinazotokana na Muungano za kawaida. Pia nazo zingelifaa zichunguzwe kweli wanaopata ndio wanaostahiki.

Lakini tunapotembelea katika kazi za Kamati na hususan vile vitengo ambavyo vina miradi mbali mbali na hivi vitega uchumi. Utaona kuna baadhi ya vitengo vinakwama katika shughuli zake kwa sababu ya urasimu wa maeneo fulani, kama ambavyo tunazungumza kila siku katika Baraza.

Sasa kama mradi ule ulikuwa u -*take of* 2010 kwa mfano. Lakini unapewa urasimu mpaka una -*take of 2013-2014.* Mimi nafikiri kesi kama hizi angelichukua nafasi ya kuzisikiliza, wale ambao wanakwamisha katika sekta binafsi kutoa ajira.

Idara hii ya ajira isijikite katika kutafuta tu, lakini hata zile ajira zilizokwama nazo pia iwe ni kichocheo katika kuwawezesha wananchi. Ikiwa kuna muwekezaji pengine wa ndani ya nchi lakini kakwamishwa kwa njia moja au nyengine na anaweza akatoa ajira 100, 200, kwa vijana wetu na nyie mchukua nafasi kama yumo ndani ya sheria ni mkwamo gani aliyokwama ili aweze kukwamuliwa.

Tunakusudia wakurugenzi wetu wasiwe ni *office oriented.* Waweze kuangalia ni pahali gani ambapo mambo yetu yanaweza yakaendelea kwa lugha ya kiingereza wawe *aggressive* katika mambo yao wakusudie kuwakwamua watu kupata ajira. Lakini tukikaa ofisini tukaanza kutafuta *data base* na hivi na hivi, hatuingii katika *field* itakuwa mambo ni yale yale, tunangojea pesa za mkopo, tunangojea pesa za nini kumbe ajira zipo.

Mhe. Spika, kuna hoteli nyingi tu na nyengine zinakuja. Lakini *surprise* yake haitoki Zanzibar na mambo mengine yanaweza yakazalishwa hapa. Mimi nafikiri wizara hii vile vile iwe kama kitengo cha Mipango Sera na Utafiti. Baadhi ya utafiti uliofanywa utizamwe ni *job creation* gani zinaweza zikafanywa ndani ya nchi.

Sasa mara hii tunakupa kama maelekezo, lakini mimi binafsi Ishallah kipindi kijacho cha bajeti baada ya mwaka mmoja masuala yote hayo niliyokupa miongozo nitakuja kuuliza moja baada ya moja, hili ulifika wapi na hili umefika wapi, uhakikishe hilo tukijaaliwa.

Mimi nilikuwa nina suala moja. Juzi tulipitisha sheria ya utumishi wa umma. Sheri kubwa na ina mambo mengi. Hapa kuna Kamisheni ya Kazi ambayo umesema itashughulikia sekta ya umma na sekta binafsi. Sasa mimi nauliza si utakuwa mgongano huu. Kwa sababu tayari Sheria ya Sekta ya Umma imeshatayarishwa na kuna Wizara kamilii, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mimi nafikiria mnge – *compromise* kila mmoja akachukua sehemu moja. Ile Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikachukua sekta ya umma

peke yake ikaishughulikia kikamilifu na Wizara hii ikawa ni sekta binafsi. Huwenda ikawa ajira zile wanaita rasmi na isiyorasmi, lakini ni zile sekta binafsi.

Sasa *coordination* ni suala la mawizara, wizara zote ni lazima ya *coordinate* katika kuendesha mambo yao. Lakini ukimeza na wewe hapa Mhe. Spika Waziri akimeza na hili ina maana anawacha pengo huenda kuna jambo lisishughulikiwe, kila moja atasema fulani atalishughulikia hili na matokeo yake wote ikawa hawakulishughukia. Lakini kila Wizara ikajikita na sekta yake ya Utumishi wa Umma na Utawala ikachukua sekta ya Umma moja kwa moja. Wizara hii ikachukua sekta binafsi *in totality*, *coordination* ndio kawaida mawizara yote yanatakiwa ya *coordinate*.

Kwa hivyo yeye yule akizidiwa ikiwa *pool* ya waliosoma au wanaotafuta ajira wamezidi yeye atazungumza na watu wa utumishi wa umma. Vipi wanaweza ku- *accommodated* na Utumishi wa Umma wakiona wengi wana *coordinate*. Lakini taasisi mbili kuzipa jukumu moja kwa kweli kuna mgongano utatokezea na utakuwa sio kwa maslahi ya nchi. Katika ukurasa wa 43 Mhe. Waziri ameandika hivi:-

Kifungu 54 “Mhe. Spika, Kamisheni ya Kazi ina jukumu kubwa la kuratibu na kusimamia masuala yote ya kazi na ajira katika sekta za umma na binafsi nchini. “

Sasa hapa mimi naona ni *contradiction* na ile Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa ufupi mimi nafikiria aje atujibu. Ikiwa kuna lolote la kufanyika basi lifanyike ili kusije kukatokezea sio migongano lakini hata kuyaachia baadhi ya mambo. Pengine akiachiwa hili tu Mhe. Waziri au akijipa jukumu hili moja la sekta binafsi litashughulikiwa uzuri zaidi kuliko kujiingiza tena katika shughuli za sekta ya umma.

Mhe. Spika, labda tuje kwenye suala la Vyama vya Ushirika, kuhusu uendeshaji wa vyama vya ushirika. Hebu Mhe. Waziri aje na *new concept* aende akatizame huko ulimwenguni, akatizame sehemu mbali mbali. Maana huu ushirika ulikuwa na *donations* mbaya hapa kutokana na kufeli sana. Labda hivyo vyama vya ushirika ambavyo vimeshasajiliwa waweze kupatiwa mafunzo maalum ya kisasa katika kuendesha ushirika wa kisasa.

Mimi namuomba Mhe. Waziri akija kutoa majumuisho hapa atueleze yeye katika kuvishughulikia vyama vya ushirika atakwenda na mkondo aliotoka nao huko nyuma tu basi, wawe wanasajiliwa au wameletwa wapya katika kuviendesha hivi vyama ya ushirika. Kwa sababu historia ya vyama vya

ushirika hapa imefeli na mashirika mengi yame *collapse*. Sasa bado tunang'ang'ania kwamba tuwe na vyama vya ushirika, kuna vyengine vimeanzisha *NGO's*, kuna *SACCOS*, lakini vyama vya ushirika bado vipo. Je, kuna utazamaji mpya uliyonao?

Mhe. Spika, kuna baadhi ya Wizara tulitajiwa karibuni hivi kama wizara itakapokuja labda itajieleza wenyewe, maana ilitajwa nafikiri katika semina, wanawake, watoto, kuna nafasi zimekuja zinazofanana na hivyo vikundi vya kusaidia vijana. Sasa zikija nafasi kama hizi nakusudia kwamba kuna uhusiano gani na hii Wizara ya Uendeshaji. Nafasi kama hizo zinapokuja zikafikia katika wizara nyengine. Maana yake inawezekana ikiwa hakuna uhusiano na ushirikiano kukatokezea *duplication* hawa wameshasaidiwa na uwezeshaji na wale wale wakasaidiwa na Wizara ya Wanawake na Watoto, wakaachwa wengine kule. Ndio nakusudia kwamba hapa pametajwa siku moja na pengine katika wizara itakapokuja itatajwa.

Mimi nakikumbuka kitu kama hicho kwamba kuna *fund* zimetoka sijui katika nchi gani lakini za kusaidia mambo ya vijana na mambo mengine. Lakini yote ni mambo ya uwezeshaji na sisi tunayo Wizara ya Uwezeshaji. Sasa kama hakuna *coordination* hapo panaweza pakawa na wengine wakapata kutokana na Wizara hii ya Uwezeshaji na wakapata huko huko kutokana na nyazifa zao au mambo mengine. Mimi nahisi kwamba hata katika ngazi ya wizara yangezungumzwa kwamba je, uwezeshaji huu unatokezea wapi katika *level* zote iwe kitengo ni kimoja tu. Au wale wakisaidia kutokana na masharti yao basi wa *coordinate* na wizara hii, ili wale watakaosaidiwa wawe wengine.

Mhe. Spika, kuna wananchi wengi wa visiwa hivi wanataka kujiendeleza hususan katika mambo ya ufugaji na uvuvi. Ingawa Wizara ya Uvuvi ipo lakini wa kuwezesha ni huyo huyo, Wizara ya Uwezeshaji. Lakini tumefanya *research* ya kile kiwango tunachowapa wale watu kinawasaidia, kwa sababu nilipata kusikia humu mtu anapewa shilingi 50,000 ndio kumuwezesha. Mhe. Spika, kwa kweli shilingi 50,000 hivi sasa ndio kumuwezesha mtu, hebu tuwe *serious* kidogo tufanye kiwango ambacho anaweza yeye akafanya jambo likawa.

Mhe. Spika, la mwisho ninalotaka kusema ni kwamba kwa sababu wawezeshaji ni serikali kwa kuwapa wananchi wake, mbona nyinyi serikali mkikopeshwa mnapewa *grass period* kwa kujitayarisha kulipa kama miaka miwili, miaka mitano mnapewa. Lakini nyinyi mkiwakopesha leo kesho asubuhi alipe, ata ule unga hajaununua tayari alipe. Mhe. Spika, angalau basi mngefanya *discussion* mkatizama kwa wananchi wetu na kiwango hiki tulichawapa basi tuwastahamilie kwa muda gani, sio lazima hiyo miaka miwili itakuwa

ameshazimaliza, lakini basi angalau tuseme miezi mitatu. Mhe. Spika, suala la kumpa leo kama huyu anayekopeshwa katika mshahara wake halafu akulipe basi akipata mshahara atakulipa, lakini mtu huyu wewe unampelekea pesa hizi za kumkopesha kwa ajili ya kumuwezesha kufanya mradi alionao.

Kwa hivyo, mimi namalizia hapa Mhe. Spika, kusema kwamba yote watizame na uwezo wa wananchi wetu na wawaachie kidogo angalau miezi mitatu waweze kujisukuma halafu ndio tena wataanza kulipa. Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba Mhe. Waziri ni mpya katika wizara hii namuamini sana kwani moyo anao, uwezo anao tunachompima moja tu atakuwa muadilifu. Ahsante sana Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja hii.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa wazima, salama na amani na kuweza kufika hapa leo kuendelea na shughuli hizi. Lakini pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuunda wizara hii na baada ya kwishakuinda wizara hii akamuachia Maalim Haroun Ali Suleiman ili aweze kuiasisi na kwenda nayo na kufanya kama yale ambayo amekwishayafanya ndani ya Wizara ya Elimu alipokuwa katika wizara ile.

Mhe. Spika, katika salamu zake za shukurani hapa Mhe. Haroun alinitaja nikiwa natokea katika Jimbo la Rahaleo, tusimlaumu sana lakini inatokana na mazoeya alizoea kuniona Michenzani pale na pale wakati huo ilikuwa ni Jimbo la Rahaleo lakini sasa hivi niko Kilimani katika Jimbo la Kikwajuni. Na kama ungelikuwa Mheshimiwa unapiga kura Kikwajuni basi ingelikuwa wewe ni mmoja kati ya wapiga kura ndani ya jimbo langu.

Mhe. Spika, sasa nije katika mada ambayo nataka kuichangia, mimi mchango wangu ni mdogo sana. Mchango wangu ilikuwa nataka kuelezewa tu jinsi ya utaratibu wa huu wa mfuko wa AK na JK. Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa nilizopewa ndani ya jimbo langu ni kwamba mfuko huu wa AK na JK katika mwaka uliopita kuna maombi 360 ambayo yalikuja kuomba katika mfuko huu. Maombi ambayo yalikuwa yamekubaliwa ni 22.

Lakini kinachonishtusha na mpaka wananchi wa maeneo yangu wamepigwa na mshangao ni kuona utaratibu wa ugawaji wa huu mfuko wenyewe. Kwa sababu ndani ya Jimbo la Kikwajuni kuna shehia 6, lakini hii miradi 22 ambayo imekubalika yote yametokea katika shehia moja. Kwa hivyo, jambo hili

limeleta utata kidogo katika eneo langu, ndio maana kabla sijafika hapa leo viongozi na wananchi mbali mbali walifika kuja kuleta malalamiko yao haya ili niweze kuja kufanya kazi hii ya kuwaulizia waweze kupata jawabu, utaratibu wa ugawaji wa ruzuku hii unakuwa uko vipi. Kwa wale ambao walikuwa wamekosa sijui Mhe. Waziri unawaahidi nini?

Mhe. Spika, baada ya maelekezo haya nimesema kwamba sina mengi sana kwa sababu nilitaka kuzungumzia suala la kazi ambalo Mhe. Rashid Seif Suleiman ameshalizungumza hapa wacha tuwaachie na wenzetu na wao wapate nafasi ya kuchangia kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa ujumla wao, baada ya kwishapata maelekezo hayo juu ya namna ya utaratibu naunga mkono hoja kwa asilimia kwa mia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi, Kiuchumi na Ushirika kutoka kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman. Kwanza nina furaha sana kumpongeza Mhe. Waziri kwa nafasi kubwa aliyoipata ya kutoa nafasi hii kwa wananchi hasa kwa watu wa chini ambao tunaita wajasiri amali. Kwa kweli wengi wa watu hawa wanatoka katika majimbo yetu sisi ambao hivi sasa tayari wameshajitayarisha kufanya kazi zao kwa bidii.

Mhe. Spika, ni kwamba hivi sasa vijana wengi tayari wanamsubiri Mhe. Waziri ili aweze kuwawezesha. Mimi nitafurahi sana akianza na mipango mipya sio ile yakutoa ng'ombe mmoja kuwezesha kikundi kizima au kuwezesha mbuzi wawili kwa kikundi kizima. Hivi sasa kama kweli anataka kuwezesha ahakikishe kwamba wananchi wote wanamsikia na jinsi anavyowatangazia kuwa atawawezesha.

Mhe. Spika, hivi sasa wananchi wengi wanajitayarisha kwa mambo ya ushoni na uvuvi, jana tulikuwa katika semina moja tulisema kwamba tunataka bahari kuu ili tuweze kuingia huko. Kwa hivyo, wananchi kama kweli wanachangiwa katika uwezeshaji mimi ningelimuomba ajitayarishe kutafuta maboti ili aweze kuyapeleka hasa katika maeneo yangu ya Uzi Ng'ambwa kule ndio vijana wengi hivi sasa kutokana na hali ya uchumi wanajishughulisha sana na mambo ya uvuvi. Mhe. Spika, kama tutaweza kupata boti angalau mbili kubwa zikawa katika jimbo lile wakagawana kama moja itakuwa iko Uzi Ng'ambwa moja ikiwa Unguja Ukuu nzima tutafurahi sana kwa vijana wetu kuwa hivi tayari wameweza kuezeshwa kama walivyotarajia.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Rashid isiwe tu kumpa kijana huyo msaada baada ya mwezi mmoja unamwambia arejeshe hata huko baharini atakuwa

hajarudi kwenye dago. Kwa hivyo, vijana wapewe angalau kuanzia miezi sita ndio waweze kurejesha hizo fedha na sisi wawakilishi wa majimbo tutazisimamia hizo fedha ili ziweze kuzalishwa, na ziweze kumea katika jimbo mpaka na wao waweze kujitegemea.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu unakwenda zaidi na mpango wa kilimo, hivyo itakuwa vizuri sana vijana wangu wakaweza kupata trekta angalau mbili kwa ajili ya kuwawezesha.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa leo sitokuwa na mchango mkubwa isipokuwa bajeti hii mimi naikubali mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani asilimia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Mhe. Spika, nina imani kwamba yeyote atakayesimama hapa atakuwa hana kubwa la kusema bali ni kumpongeza Mhe. Waziri kwa sababu ni mtu ambaye anaeleweka, anajuulikana na utendaji wake wa kazi. Mhe. Spika, mimi nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kupewa kazi hii ya uendeshaji kwa kuwawezesha wananchi kiuchumi, mimi nasema Mhe. Rais hapa amepata mahali ndipo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri pamoja na timu yake ambayo imeoneshwa katika kitabu hiki, timu hii nina imani kwamba katika kipindi hiki cha 2011/2015 basi wananchi wetu wataondokana na umasikini na watainuka kimaisha katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na wao wenyewe kwa ujumla. Kwa sababu Katibu Mkuu wake ni mtendaji mzuri nina imani kwamba na Wakurugenzi wote ulionao ni watu wazuri hivyo mambo yatakuwa mazuri katika wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema mimi nataka kuchangia machache katika ukurasa wa 30 kuhusu malengo ya idara na mikopo. Mhe. Spika, mambo ya mikopo katika kipindi kilichopita wananchi wengi ambao walipata mikopo hii hasa ya AK na JK ni kwamba kumetokezea matatizo kidogo, na pia urudishaji wa mikopo hiyo imekuwa ni tatizo kubwa.

Lakini kwa Mhe. Waziri nina imani kwamba mambo yatakwenda mazuri na wale ambao hawajapata mikopo hii hasa katika Jimbo la Rahaleo ningemuomba sana Mhe. Waziri akalifikiria sana jimbo hili kwa sababu wananchi wake bado hawajapata mikopo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba ukaliangalia sana Jimbo la Rahaleo na wao waweze kupata mikopo hii, pia na wewe mwenyewe Mhe. Waziri kwa bidii yako na uwezo

wako ulionao kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Zanzibar waondokane na umasikini walionao wananchi wetu.

Mhe. Spika, niliwahi kutembea katika Wilaya ya Micheweni na sote tunajua kwamba Wilaya hiyo ni Wilaya ambayo wananchi wake ni masikini. Lakini ukiangalia tathmini ambayo imepatiwa mikopo katika Wilaya hiyo ni kidogo kutokana na hali yao ilivyo na serikali inafahamu hali yao. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri akawaangalia sana wananchi wale wa Micheweni kwa hii ni aibu kila siku inatajwa Micheweni tu. Mhe. Waziri mimi nakuomba sana uwaangalie wenzetu wale ili waondokane na umasikini.

Mhe. Spika, mbali na Wilaya hiyo pia kuna Wilaya mbali mbali ambazo hali zao ni duni. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri mikopo hiyo iwaangalie wale wananchi ambao hali zao ni duni, kwani wananchi wetu ni masikini hasa huko vijijini. Mhe. Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri uliangalie hilo, timu uliyonayo ni nzuri sana nina imani kwamba tukija katika bajeti ya mwaka 2012/2013 basi tayari wananchi wetu hata kama ni asilimia 25 wataondokana na umasikini baada ya kupata mikopo hii ya AK na JK na mikopo mengineyo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi kama nilivyosema awali namuamini sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono kwa asilimia mia mbili. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, kunipa ruhusa hii na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake iliyokamilika. Hotuba ambayo ni nzuri tu lakini vile vile wizara hii ni mpya kwa hiyo kila mmoja atakuwa anataka kutoa ushauri kidogo tu maelekezo.

Mhe. Spika, kwanza mimi nianze katika ukurasa 36 niwapongeze Idara ya Ushirika kwa lengo la kusajili vyama 177 badala ya vyama 171, hii nikuonesha wazi jinsi ya wananchi walivyojitokeza kushirikiana na waziri wao ili kupata kujiendeleza katika uzalishaji.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye ukurasa wa 38 ni kwamba Mhe. Waziri kasema imetolewa elimu kwa vikundi vya ushirika, lakini mimi nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri ingawa imetolewa elimu kwa vikundi vya ushirika, lakini bado migogoro ya vikundi vya ushirika vijijini imo. Mhe. Spika, inafikia hadi vikundi kutokuelewana na pia kutokuviendeleza vikundi hivyo kutokana na kutokuwa na elimu ya ushirika na pia kutokuwa na utunzaji wa kumbukumbu. Mhe. Spika, jambo hili namuomba Mhe. Waziri alifikirie sana ili aweze kuvipitia vikundi vilivyoko vijijini aweze kutoa elimu kwa

washirika. Mhe. Spika, pia namuomba Mhe. Waziri aweze kuwapatia semina wana vikundi vya ushirika ili waweze kujiendeleza zaidi.

Mhe. Spika, jengine nije katika ukurasa wa 29 juu ya kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi wa JK na AK ni kwamba katika Wilaya yangu ya Kusini ni kuwa idadi ya mikopoi 33 imetolewa na wanawake ni 42 na wanaume ni 15 jumla ni 57. Mhe. Spika, mimi namwambia Mhe. Waziri pesa hizi zote zinazotelewa kwa wananchi, lakini Mhe. Spika, tunaona mabilioni ya pesa yanayotolewa lakini wamo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa hawajui ni vikundi gani vinavyopewa pesa hizi. Kwa sababu mabilioni ya pesa hizi zinazotolewa na vikundi vinavyopewa hatuvielewi ni vikundi gani vinavyopewa mabilioni ya pesa hizo.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri uliangalie kwa makini jambo hili, mimi nadhani Mhe. Waziri inapotolewa mikopo hii ni kuwashirikisha vizuri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliomo katika Wilaya zao au kwenye majimbo yao ili na wao waweze kuona ile mikopo inayotolewa ni kweli. Mhe. Spika, vile vile hata kwenye kitabu ukisema kama Mhe. Mwanajuma nimemshirikisha katika mkopo huu na alikuwepo na akaona mikopo iliyotolewa, naamini utakuwa uhakika upo na nitasema ni kweli kama Mhe. Waziri alitoa mkopo huu.

Mhe. Spika, vile vile nije katika ukurasa wa 56 unaosema kwamba Idara ya Usalama wa afya kazini. Mhe. Spika, hili ni suala muhimu sana na ni suala ambalo lakupewa kipaumbele kwa sababu kazi yeyote ile ikiwa hapana afya inakuwa haiendi. Kwa hivyo, naomba wafanyakazi wote waliomo katika wizara yako waangaliwe kwa kina yanapotokezea matatizo na hata kupewa fursa yakwenda kutibu hali zao nje. Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi yakuweza kuchangia japo kidogo kwenye hii Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara maalum ambayo lengo lake wizara hii ni kuwasaidia wananchi kiuchumi, kwa hiyo kama lengo ni hilo lakuwasaidia wananchi kiuchumi hatuna budi kumwambia Mhe. Waziri ana kazi kubwa sana ambayo imemkabili, kwa sababu hali za wananchi wetu tunazijua ni hali duni na wananchi watakuwa wote wako chini ya wizara yake kuona na wao wanapata maendeleo haya ya kiuchumi, na kuweza kuwakomboa katika umasikini. Kwa hivyo, nikusema kwamba wizara hii ni wizara ambayo

inajitengea kazi maalum kwa wananchi ambayo tunaitegemea watu kuweza kupata ajira ndani yake.

Mhe. Spika, wizara hii itakuwa baada ya kukuza ajira vile vile itakuwa inaweza kunyanyua kipato cha wananchi hasa wale wenye kipato cha chini ambao nasema kwa Mhe. Waziri kazi hii haitakuwa ndogo itakuwa ni kubwa sana. Mhe. Spika, pia tunahitaji kuweka mazingira bora ya wafanyakazi wetu kwa hiyo ni juu ya Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba mazingira mazuri ya wafanyakazi wetu yanapatikana.

Mhe. Spika, tuna idara hizi ambazo zilizoundwa kama Idara ya Ushirika, idara hii kwa kweli ukiitizama kihistoria utakuta ushirika umeanza muda mrefu. Mhe. Spika, suala la ushirika halikuanza leo wala halikuanza jana, lakini limeanza muda mrefu. Lakini utakuta ushirika nyingi zinazofanywa zinakuwa hazimaliziki kwa usalama, mara nyingi mashirika mengi yanavunjika.

Kwa hivyo, hatujui malengo ya mashirika haya si barabara au malengo yao huwa sio mazuri, lakini utakuta baada ya watu kukaa pahala pamoja wakafanya mashirikiano katika mambo basi utakuta haitimii muda mrefu mashirika yale yanavunjika. Kwa hivyo, hapa tumuombe Mhe. Waziri katika masuala haya ya Idara hii ya Ushirika aweze kuisimamia vizuri na wale ambao watakaoingia katika ushirika haki zao ziwe zinapatikana na zinasimamiwa vizuri na hapo ndipo watu watakapoweza kujua kwamba wizara hii imeweza kusimamia mashirika yao vizuri.

Mhe. Spika, pia katika wizara hii inasimamia mambo ya mikopo, hivyo suala hili ni muhimu sana kwa Mhe. Waziri kutenda haki. Mhe. Spika, kwa sababu watu wanahitaji mikopo na ni lazima wakati wa mikopo Mhe. Waziri awe makini sana kuhakikisha kwamba mikopo hii inayotolewa inapatikana kwa wakati na inarudishwa kwa wakati na wale wanaotaka mikopo wapewe haki zao za kuweza kukopa.

Mhe. Spika, tuna hii Kamisheni ya Kazi vile vile ni muhimu kuweza kuangalia maendeleo ya wafanyakazi wake, pia kuweza kuangalia afya za wafanyakazi. Kwa sababu tunaona kwamba ni jambo muhimu sana kuwa afya za wafanyakazi kuweza kuangaliwa, kwa sababu tunaona watu wanafanyakazi sehemu mbali mbali lakini pengine afya zao hazishughulikiwi. Mhe. Spika, ukenda katika mahoteli au ukenda katika sehemu nyengine za wafanyakazi inakuwa hazishughulikiwi afya zao. Kwa hivyo, kama hii wizara inashughulikia na wafanyakazi katika afya zao, basi ningelimuomba Mhe. Waziri aweze kushughulikia mambo yanayohusika na afya za wafanyakazi.

Mhe. Spika, kwa sababu hii ni wizara mpya na hatuwezi kuisema sana katika wizara hii, kwa sababu mchango wake ni mdogo na kwa vile haijaweza kufanya jambo lilokuwa kubwa ili tukaweza kulizungumza ndani yake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa hayo machache nasema ahsante sana nashukuru kwa niaba ya wananchi wangu naunga mkono hoja hii.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni kwa kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika Mhe. Haroun Ali Suleiman. Kwanza nampa pongezi Mhe. Haroun pamoja na wizara yake nzima kwa sababu wizara hii ndio kwanza mpya, lakini kwa uzoefu wake imekuwa kama wizara iliyokuwa na miaka 20 kwa hiyo mimi nampongeza na nawapongeza wafanyakazi wa wizara hii kwa kitabu hiki kizuri.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara ya uwezeshaji wa wananchi kwa hiyo na mimi leo natoa mchango wangu mfupi kwa sababu wizara yetu ni changa. Kwa hivyo, ilivyokuwa ni changa kama tutaichangia sana inaweza ikateteruka kidogo, lakini tuichangie kidogo ili waweze kujipanga.

Mhe. Spika, wizara yetu ni wizara inayoitwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na sisi katika majimbo yetu mengi ni masikini sana, hasa majimbo yetu kama kule Matemwe bado tuko masikini. Kwa hivyo, kwanza ningelimuomba Mhe. Waziri aiangalie Matemwe na aiwezeshe mapema.

Pili ningelimuomba Mhe. Waziri awawezeshe na wafanyakazi wake katika wizara. Kwa sababu mfanyakazi akimuwezesha katika wizara mapema basi mfanyakazi yule atakuwa na hamu ya kufanya kazi, wakati atakapostaafu atakuwa haijambo vipi ameweza kujitegemea kuliko mfanyakazi amestaafu baadae aje aombe tena kibarua. Kwa sababu wakati amefanya kazi miaka mingi lakini wizara yake haikumuwezesha na wizara inaitwa Wizara ya Uwezeshaji.

Tatu, kuna mikopo Mhe. Spika, ya kuwapa wananchi, ningelipenda kumuomba Mhe. Waziri kabla ya kupeleka mikopo katika shehia zetu wakawaelimisha wananchi vipi kuitumia mikopo ile.

Mhe. Spika, wananchi wetu wengi wanapopewa mikopo wanafilisika. Kwa sababu hawana elimu nayo halafu zile nyanja za kufanyia kazi hawana. Kwa hivyo, napendekeza kwamba, wizara ziwakopeshe wananchi vifaa vya kufanyia kazi. Kwa mfano, kama wananchi watakopeshwa mashine za kusagia nafaka, vyarahani na vitu vyenginevyo basi wanaweza kujikomboa upesi kuliko kuwapa fedha, kwa sababu ukiwapa fedha aidha wale wanaozipeleka

hawazifikishi au ndani ya shirika lile lile anakula mtu mmoja inakuwa basi, wakati wa kulipa hazilipiki na wala hazionekani ziko wapi. Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, napendekeza wananchi wawezeshwe kwa vifaa vya kufanyia kazi.

Mwananchi kama utampa mashine ya kusagia nafaka kwa mfano kinu cha kusagia mpunga basi ataweza kujikomboa upesi kuliko kumpa pesa, sababu mashirika mengi waliyopewa wananchi yamefilisika kwa kupewa pesa. Naiomba wizara hii ya uwezeshaji kama itakuwa uwezekano upo wananchi wapewe vifaa kamili, ikiwa wanakopeshwa gari basi wakopeshwe gari, ikiwa vyarahani basi wakopeshwe vyarahani, kama viwanda vidogo vidogo wakopeshwe viwanda vidogo vidogo ndivyo vitavyowainua wananchi.

Kwa mfano mimi Jimbo langu la Matemwe kuna shehia iliambiwa itapewa mkopo wa JK, shehia moja hii wamekuja wamepewa watu watano na kule waliambiwa watapewa 50. Sasa pesa zile za watu 50 hazikufika wamepewa watu watano arubaini na tano zimekwenda wapi, hazikuonekana. Lakini ukija huku katika sheria ya kukopeshwa utasema wananchi wa Matemwe washakopeshwa, lakini katika 50 wamepewa watu watano je, fedha za watu 45 ziko wapi? Watu wale bora wangelipewa vyarahani 10 basi tungejua wako wapi kuliko kupewa hizo pesa zikarejeshwa. Pesa zimerejeshwa na kati ya watu 50 wamepewa watu watano, bada ya kuuliza wanaambiwa watu hawa hawana vipaji sasa vipaji vya kukopeshwa vinatoka wapi?

Kwa hivyo Mhe. Spika, wananchi wetu wanakoseshwa mikopo bure kwa kuambiwa hawana sifa sasa sijui hizo sifa za kukopeshwa ziko wapi. Kwa hivyo, naiomba wizara au serikali itueleze sifa za mkopeshaji zinatakiwa ziwe zipi, mtu masikini ataambiwa wewe weka nyumba anayo? Ataambiwa aweke dhamana ya gari anayo? Sasa mikopo yenye masharti magumu wananchi hawaiwezi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba wananchi wapewe mikopo ile wanayoiweza. Kwa sababu mwananchi ukimwambia weka dhamana ya gari atakuwanayo, weka dhamana ya nyumba atakuwanayo, dhamana ya nyumba anaambiwa shilingi 50 elfu au laki moja huu utakuwa si mkopo iutakuwa hatari.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali iwakopeshe wananchi mikopo ili wajigomboe, mkopo wa dhamana wa nyumba mwananchi masikini hatauweza kwa sababu nyumba sasa hivi inayotakiwa itimie shilingi 20 milioni, sasa pesa hizo tena ndio anataka kukopa huyo! Mwananchi akopeshwe mikopo ambayo ataimiliki ndio tutaweza kuwakomboa, lakini ukimwambia mwananchi nakukopesha lakini uweke dhamana ya nyumba au gari, shamba wengine hawana shamba, kutwa nzima shilingi elfu mbili hapati ataweza nyumba, akiweka nyumba

umemdai hakukulipa unamfilisi sasa baada ya kumuinua anafukarika na wizara ya uwezeshaji itakuwa si wizara ya uwezeshaji itakuwa wizara ya ufukarishaji.

Mhe. Spika, tunaomba mimi napendekeza kwamba wananchi wapewe mikopo bila ya masharti ili wasomeshwe zile biashara na kujua biashara gani wafanye mdai ahakikishe huyu anakwenda kumdai pesa sio amuwekee dhamana ya nyumba. Mwananchi akiweka dhamana ya nyumba akishindwa kulipa kafilisika, ukimfilisi sasa aanze tena wapi atakwenda kutafuta nyumba ile, hiyo nyumba kaijenga kwa miaka 50 halafu akaitafute tena miaka 50 yuko duniani mtu tu mtu huyo? Tutawazika wengi na hatuwanufaishi chochote.

Mhe. Spika, naiomba wizara ihakikishe inawezesha watu masikini, idadi ya wananchi wetu wengi ni masikini, idadi ya majimbo yetu mengi ni masikini. Kwa hivyo, serikali wakileta mikopo ilete mikopo bila ya masharti magumu, masharti magumu wananchi wetu hawayawezi na ndio ukaona vikundi vingi vimekopeshwa pesa lakini kulipa hawawezi kwa sababu ya masharti magumu.

Mtu unamkopesha pesa uchuuzi wake nazi, nazi zenyewe anachuuza kwa baskeli unamwambia weka nyumba si unataka kumfilisi kirai, badala yakumuwezesha unataka kumnyang'anya. Kwa sababu hawezi akachuuza nazi za shilingi elfu kumi akaweka aliyoipigania kuanzia umri wake wa miaka 20 mpaka amefikia miaka 70 anajenga nyumba hiyo haijamaliza tofali wala choo, lakini pale kwa kutaka kukopeshwa anaweza akaweka rehani, lakini ikiwa hakuweza kuilipa ananyang'anywa kafilisika sasa badala ya kutajirika anafilisika.

Kwa hivyo Mhe. Spika, wizara yetu ni changa hatuwezi kuichangia sana kama alivyosema mwenzangu, lakini naiomba serikali na wizara kwamba, wakati wananchi watapokopeshwa wakopeshwe masikini wasikopeshwe ndani ya utajiri. Ukimwambia mwananchi weka nyumba, weka gari, weka nini hiyo inakuwa unamkopesha tajiri na nchi yetu hawapo watu kama hao, ukiwakopesha kwa masharti kama hayo hakuweza kulipa unamfilisi na ukimfilisi umemfukarisha.

Jengine niende kwenye ajira. Wizara yetu ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi na Ushirika hapa tunao vijana wengi sana wanazurura ovyo hawana kazi ya kufanya. Kwa hivyo, naiomba wizara hii hususan katika majimbo yetu, majimbo yetu mengine kama vile Matemwe ni majimbo ya kimasikini. Kwa hivyo, naiomba wizara ifanye ziara makusudi hasa kuja kututembelea na kuona vijana na watu waliokuwa hawana ajira ili wawafanyie ajira au wawafanyie nyanja za kuwakopesha fedha na vifa vya kufanyia kazi.

Aidha, wanaweza kuwakopesha fedha lakini kwa kuhakikisha kwamba tunakopesha fedha kwa kununua kifaa fulani na tunakukabidhi kifaa fulani, pale ukimuwezesha namna ile unahakikisha kuwa umempa kifaa na anafanyia kazi na analetewa mabingwa wa kumfahamisha, lakini tukiwakopesha fedha vijana watazila na hawalipi, ndio maana kwamba vijana wengi au wananchi wengi wanaokopeshwa baadae hawawezi kulipa kwa sababu nyanja zile za kufanyia hawana sasa inakuwa zile pesa anachukua tu, anaondoka pale anakwenda kuuza maandazi siku mbili tatu maandazi yamefilisika ameanguka.

Lakini kama tutawapa vifaa vya kufanyia kazi na vya huduma. Kwa mfano, kule Matemwe, Matemwe kuna wavuvi na kama watapotiwa maboti na nyavu za uhakika au vifaa vya uhakika vya kufulia wakikabidhiwa watajiendesha, lakini mvuvi ukimpa fedha anakwenda kula changu badala ya kwenda kuvua changu anakwenda kununua changu, itakuwa kafilisika hakuwezeshwa. Kwa hivyo, naomba wavuvi wangu wa Matemwe wanunuliwe maboti wapelekewe wakishapewa watafanya kazi, ninahakikisha kama watapatiwa nyanja za kufanyia kazi na hakikisha Wizara ya Uwezeshaji itapata fedha zake zilizotoa kuliko kwenda kuwapa fedha wakazitafuna.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nampongeza tena Mhe. Waziri na namwambia aje Matemwe aangalie wananchi wa Matemwe awawezeshe mapema ili waondoke katika umasikini. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Pia naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naona muda uliobakia ni mchache sana tuna dakika kama saba tu, nafikiri hazimuwezeshi Mhe. Mjumbe kuweza kuchangia. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru na sasa niahirishe kikao hiki hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:38 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 19/07/2011 saa 3:00 asubuhi)